ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe

15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18.Mhe. Mansoor Yussuf Himidi	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Kiembesamaki
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
31.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe

32.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
33. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais
51.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
52.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
53.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
54.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile

55.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

56.Mhe. Mohammed Said Mohammed Jimbo la Mpendae

57.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak Nafasi za Wanawake

58.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

59. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

60.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

61.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

62.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

63.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

64.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Rashid Seif Suleiman Jimbo la Ziwani

66.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

67.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

68.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

69.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

70.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

71.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

72.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe

75.Mhe. Shawana Bukheti Hassan Jimbo la Dole

76.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni

77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde

78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake
Ndugu Yahya Khamis Hamad	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Thalathini na Sita – Tarehe 3 Agosti, 2012

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani hati ya Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa mwaka wa fedha 2012/2013, naomba kuwasilisha.

Mhe. Abdalla Moh'd Ali (Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo): Mhe. Spika, naomba kuwasilisha Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kuhusu Makadirio na Mapato ya Matumizi ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa mwaka 2012/2013, naomba kuwasilisha.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2012/2013 – Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kabla hatujaendelea na majadiliano na leo tuna wageni wachache ambao wageni hawa wanamhusu Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, Mhe. Thuwayba Edington Kissasi wakiwa ni watoto wake, lakini pia na uongozi wa vijana wa jimbo lake la Fuoni. Kwa hivyo, wageni wetu wa leo ni watoto wawili wa Mhe. Thuwayba E. Kissasi ambaye ni Jamila Kassim na Sara Kassim. Vijana karibuni muone shughuli zetu.

Pia uwakilishi wa uongozi wa vijana kutoka Jimbo la Fuoni ambao ni Mwenyekiti na Katibu wake naomba pia wasimame. Nafikiri vijana hawa ndio timu inayomfanyia kazi Mhe. Thuwayba. Waheshimiwa Wajumbe hao ndio wageni wetu kwa leo karibuni vijana na Waheshimiwa Wajumbe karibuni sana. Baada ya hapo basi tuendelee na majadiliano na nafasi ya kwanza kwa asubuhi ya leo inakwenda kwa Mhe. Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum, Mhe. Machano Othman Said na baadae Mhe. Mwanasheria Mkuu.

UTARATIBU

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima nilikuwa naomba au ninashauri kutokana na uzito wa bajeti hii ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano na leo siku ya Ijumaa nina wasiwasi tukaja tukakosa swala ya Ijumaa. Sasa naomba muongozo wako Mhe. Spika, na ushauri wangu kwamba wangeliendelea kuchangia Waheshimiwa Mawaziri baadae tukamuacha Mhe. Waziri wa Biashara akasoma hotuba yake halafu masuala ya vifungu

au majibu ya maswali yetu na vifungu tuje tupitishe siku ya Jumatatu ili tuweze kwenda vizuri. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Ombi au hoja hiyo hatuwezi kuiamua maana hata *quorum* ya kufanya uamuzi huo haipo. Mhe. Machano Othman Said uendelee kujadili na baadae Mhe. Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Waziri Asiye na Wizara Maalum (Machano Othman Said): Mhe. Spika, awali ya yote kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai, uzima Ijumaa hii ya leo, lakini pia Mhe. Spika, niruhusu nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano.

Mhe. Spika, nianze kwa kumpongeza Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano kwa uteuzi wa uwaziri alioupata wiki iliyopita. Ni matarajio yangu kwamba atakabiliana na changamoto na matarajio yetu kwamba atafanikiwa katika kuliendeleza gurudumu hili.

Pili Mhe. Spika, nimpongeze Mhe. Naibu Waziri wa wizara hii na watendaji wote wa wizara. Mhe. Spika, kwa kuwa leo ni Ijumaa na bado uamuzi wako hujatoa mimi nitachangia kidogo sana ili tuweze pia kupitisha vifungu kama ambavyo ratiba yetu ipo.

Mhe. Spika, mimi nitazungumzia maeneo kama matatu, kwanza eneo la usafiri baharini, pili ujenzi wa barabara na nitamalizia uimarishaji wa uwanja wa ndege. Mhe. Spika, nchi yetu ya Zanzibar ni visiwa na hata hapo zamani tulikuwa na utaratibu wa kuwa na meli za serikali, na kwa bahati nzuri kwa miaka yote serikali imekuwa ikinunua meli. Meli za mwisho mwisho ni mwaka 1980 kwa kununuliwa M.V. Maendeleo na M.T. Ukombozi. Lakini pamoja na kwamba serikali ina azma hiyo hata kwenye ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010/2015, jambo hili linazungumzwa waziwazi kuimarisha usafiri wa baharini. Kwa hivyo, tamko la Mhe. Rais wetu la kuiagiza Wizara ya Fedha na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano; la kuhakikisha kwamba serikali inanunua meli mpya ni jambo la fahari sana na hatuna budi kumpongeza Mhe. Rais wetu.

Mhe. Spika, mchakato wa kutafuta meli ulianza zamani sana, bahati nzuri mimi nilikuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais ambaye nilikabidhiwa dhamana ya kushughulikia mawasiliano na uchukuzi. Mwaka 2009 tulipata tatizo la Meli ya Fatihi kuzama na abiria sita pamoja na wafanyakazi walifariki, baada ya kadhia ile serikali ilikaa kitako na kuamua kununua meli, lakini mchakato wake ni mrefu sana, walianza Shirika la Meli, Bodi ya Shirika la Meli wakapitia wakaleta wizarani tukapeleka serikali kuu, lakini kwa bahati mbaya muda nao ulikuwa umekwenda sana.

Baada ya Mhe. Rais Dr. Ali Mohammed Shein kuingia madarakani wazo hili ameendelea nalo na hatimaye sasa ametoa agizo rasmi kwamba serikali ifanye kila inaloweza meli inunuliwe, na bahati nzuri vyanzo na mipango ya fedha vipo na tayari zimethibitishwa na Baraza la Mapinduzi. Kwa hivyo tunatarajia sasa hatutorudi nyuma katika ununuzi wa meli mpya ambayo itachukua abiria wetu.

Mhe. Spika, kadhia ya usafiri baharini ni matatizo ya muda mrefu, serikali baada ya kuachia soko huria tulianza na Ras Nungwi hapa nafikiri wengi tunakumbuka, Ras Nungwi ilikuwa ndio

boti ya haraka zaidi lakini hatimaye zikaja boti nzuri zimeendelea na bado tunawashukuru wawekezaji kwamba wanaendelea kuwekeza katika sekta hii ya baharini. Sasa mimi niombe na wananchi kwamba pamoja na kuwa serikali itaagiza meli lakini bado tutaendelea na kutumia sekta binafsi katika usafiri wa baharini. Ombi langu ni kwamba, tunaposafiri tujitahidi sana kufuata sheria zilizowekwa na Mamlaka, tuna tatizo la wananchi kutofuata sheria. Kwa mfano, tunasafiri kwa tiketi ya jina la mtu mwengine, tunasafiri bila ya kulipa tiketi, sasa haya mambo nafikiri tuyaangalie sana yasije yakatuharibia.

Lakini jengine Mhe. Spika, nimeshukuru kwamba wizara hii ya Miundombinu inayo mpango mzuri wa kuliimarisha Shirika la Meli, na ni matarajio yangu kwamba matatizo mengi ya usafiri yatapungua baada ya Shirika la Meli nalo kununua meli zake mpya za kileo, lakini pili kuwa na *management* nzuri na muundo mzuri wa shirika lenyewe. Nilipokuwepo mimi ilikuwa tatizo moja la Shirika la Meli kuwa na wafanyakazi wengi kuliko mahitaji yao, lakini pia mfumo wa uajiri wao uko sana kiserikali kuliko Shirika la Meli. Kwa sababu katika Shirika la Meli na meli zote duniani haiwezekani mtu mpaka miaka 60 awe mfanyakazi wa melini, lakini kwa sababu yeye ni sheria awe mtumishi wa serikali hapa hilo ni tatizo. Kwa hivyo nafikiri wazo lao la kuwa na mkataba maalum kwa mabaharia ni jambo jema na nafikiri utapokuja muundo huo Waheshimiwa Wawakilishi tuukubali.

Mhe. Spika, eneo jengine ni la ujenzi wa barabara. Mimi pia naomba niwashukuru sana watu wa miundombinu zaidi kwenye barabara kwamba wameweza sana kuifanya nchi yetu ifikike haraka kwa barabara nzuri. Mhe. Spika, miaka 15 nyuma hatukuwa na barabara Zanzibar zilibakia barabara kama mbili au tatu tu, lakini kutokana na malengo na mikakati mizuri hivi sasa kwa upande wa Unguja karibu barabara zote kuu zimeshajengwa kwa kiwango cha lami. Sasa hivi lengo lao kubwa ni kuzungumzia barabara za *feeder road*, kwa Unguja wamemaliza kabisa barabara kuu za Unguja.

Lakini kwa Kisiwa cha Pemba kama miaka mitano nyuma nayo ilikuwa ni tatizo, sasa hivi bahati nzuri kinafunguka nacho, na ni matarajio yetu kwamba ndani ya miaka miwili mitatu mbele Kisiwa cha Pemba nacho tatizo la barabara litakuwa limekwisha. Kuna barabara tatu za Kaskazini Pemba zinajengwa, barabara za Mkoa wa Kusini Pemba zimejengwa, lakini kuna barabara nyengine tano zinajengwa kupitia *MCC*, nafikiri baada ya hapo itakuwa mambo mazuri. Ombi langu kwa wizara na Mhe. Waziri kwamba, ajitahidi sana kulipatia ufumbuzi tatizo la barabara ya Ole/Kengeja hii nayo itatusaidia sana, ingawa nayo naelewa kwamba tatizo lake kubwa ni fedha kidogo kuliko makisio halisi ya ujenzi wa barabara. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri na watendaji wake wajitahidi sana kuhakikisha kwamba tatizo hili nalo linapatiwa ufumbuzi.

Lakini Mhe. Spika, katika masuala haya ya barabara niombe na mimi kuwaomba Wazanzibari wenzangu. Jana nilimsikia Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali akasema thamani ya barabara, ni kweli ujenzi wa barabara ni gharama kubwa, kilomita moja ya lami inagharimu kati ya shilingi milioni mia nane na bilioni moja. Sasa serikali inapotumia fedha hizi kujenga barabara za lami halafu watu wengine wakachukua mipira ya magari wakachoma moto barabara wanaturejesha nyuma kabisa. Barabara zetu nyingi zaidi za mji wa Unguja zimechomwa moto na zimeharibika sana, watakaoumia ni Wazanzibari wote bila ya kuangalia huyu nani au huyu nani. Mimi naomba tusizionee barabara, barabara hazisemi wala hazizungumzi jambo lolote, tuziache

kwa ajili ya maendeleo yetu kwa sababu hatimaye tukimaliza mambo yetu tutazitaka zile barabara na sote tunakubaliana kwamba, nchi yetu ili iendelee lazima kuwe na uwekezaji tuimarishe utalii. Sasa kama barabara tunaziharibu nani atakuja kuimarisha uwekezaji na utalii.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, wito wangu kwamba barabara tuziheshimu. Jana Mhe. Raza amesema kwamba tusiweke gereji lakini mimi nasema tusichome moto mipira, tusizichore barabara kwa kutumia mafuta na tusilaze magari barabarani haya yote yanaharibu barabara.

Lakini pia nimuombe Mhe. Waziri kwamba katika mpango wake wa *feeder road* waendelee, na jana nilimsikia Mheshimiwa mmoja akasema kwamba kutokana na mpango wa serikali wa kutupatia sisi Waheshimiwa Wawakilishi fedha za maendeleo kuwe na kitengo pale cha kushughulikia Wawakilishi. Mimi nafikiri sasa hivi hakijawa rasmi lakini kipo kuna Mheshimiwa mwenzetu pale wamesema nyinyi tunakupeni Mheshimiwa mwenzenu mkija mtashughulikiwa mambo yenu katika *UUB*. Nafikiri ni jambo ambalo lipo na linaendelea vizuri.

Lakini pia nizungumzie kwamba wananchi wa Jimbo la Chumbuni wamenituma niwaombee barabara yao ya kwa Kichachacha/Bamita ijengwe haraka kwa sababu hawana njia sasa hivi ya kupita baada ya ujenzi wa senyenge ya Chumbuni Studio. Naishukuru serikali hatua iliyochukua mpaka sasa ni matarajio yangu kwamba tutamaliza haraka suala hili.

Mhe. Spika, naomba nimalizie kwa eneo la Uwanja wa Ndege. Mhe. Spika, katika miaka ya 2000 mpaka 2005 hali ya kiwanja chetu cha ndege na hali ya bandari yetu ilikuwa ni tishio, ilikuwa ni tishio kwamba wakati wowote kwanza ndege haziwezi kuingia Zanzibar. Lakini pili meli zilikuwa hazifungi Zanzibar, mizigo yote ya Zanzibar kwa meli ama ilikuwa ikishushwa Mombasa, Kenya ama Dar es Salaam. Na ndege hapa zilikuwa haziji za maana. Kwa hivyo, Serikali ya Awamu ya Sita na hatuna budi kumpongeza sana Mhe. Amani Abeid Karume kwa kusimamia miundombinu na kuhakikisha kwamba mambo haya mawili yote yanawezekana. Ilikuwa kama ndoto wakati ule kuzungumzia bandari tunajenga na uwanja wa ndege tutaufanyia ukarabati.

Mimi nakumbuka kuna mambo kama matano kwa uwanja wa ndege ambayo tulipewa masharti na Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga. Jambo la kwanza tulielezwa kwamba kama *run way* yetu hatukuijenga hakutokuwa na urukaji na utuaji wa ndege baada ya muda, lakini la pili tukaelezwa pia, pamoja na *run way* lazima mjenge na uzio, tatu *taxi way* lazima tujenge mpya na nne *apron* na tano *terminal*.

Sasa Mhe. Spika, bahati nzuri *World Bank* walitukubalia kutupa mkopo kwa ajili ya ujenzi wa *run way* lakini kwa masharti kwamba sisi wenyewe Wazanzibari tutafute fedha za ndani za kujengea uzio, na serikali ikajipiga kifua na ikasema itaweza chini ya Mhe. Amani tukajenga. Tumejenga *run way* nzuri na imemalizika salama na hatua za ujenzi wa uzio zikaanza. Mhe. Spika, pale mimi wizarani Mhe. Hamad Masoud yeye amesema alikaa miezi 20, mimi nilikaa miezi 26 kama Waziri na miezi 12 kama Naibu Waziri, ukuta umeanza nawashukuru naomba waendelee.

Sisi pia wakati ule hali ilikuwa ngumu zaidi na mimi nataka nitamke wazi kwamba mimi naunga mkono sana misaada ya Kichina hata kama mikopo kwa sababu kulikuwa na kipindi hatuna kwa

kukimbilia zaidi ya China. China tukazungumza nao na kwa hili nataka niwashukuru watu watatu kuhusu *terminal*. Kwanza nimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete, nimshukuru Mhe. Amani Abeid Karume Rais Mstaafu wa Zanzibar na nimshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar Dr. Ali Mohammed Shein alikuwa Makamo wa Rais wa Tanzania wakati ule. Pengine kama sio watu watatu hawa leo tungekuwa tunazungumzia jengine kuhusu *terminal*. Mimi na Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi tulishiriki katika mazungumzo na Wachina alipokuja Rais wa China. Kwanza mazungumzo yale yalishirikisha miradi ya Bara peke yake halafu na sisi tukapewa *forum* ya Zanzibar peke yetu na mazungumzo yetu yaliongozwa na Mhe. Amani pale Movenpick Hotel.

Ukweli juhudi za viongozi wetu hawa watatu zilisaidia sana kuona kwamba Zanzibar nao wanaingizwa katika miradi, sisi tulipata miradi miwili; tulipata mradi wa *airport* na tukapata mradi wa *E-Government,* lakini baada ya mazungumzo marefu na juhudi za viongozi wetu. Sasa bado mimi naona kwamba hawa ni rafiki zetu wa kudumu Wachina na ninawashauri kwamba tusiwaseme vibaya kwa sababu inawezekana siku moja na wao wenyewe wakasikia tunawasema vibaya.

Mhe. Spika, jengo limeanza lakini pia nasikia na *taxi way* wameshakubaliana pamoja na *apron*. Mimi naomba Mhe. Waziri na watendaji wake wajitahidi sana kufanya kazi kwa bidii, wizara hii ni ngumu, wizara hii inatumia fedha nyingi, miradi yake sio ya shilingi moja wala mbili, lakini wathamini kwamba wanajenga taifa na hatimaye iko siku wataondoka lakini wananchi na nchi itawatambua nani alifanya mema na nani hakufanya mema. Kwa sababu wizara hii si ya maneno hii ni wizara ya vitendo, pale kuna kujenga ama barabara, ama uwanja wa ndege, ama bandari. Kwa hivyo ukisema tu bila ya kutenda utaonekana, na ambaye atafanya bila ya kusema ataonekana. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri na watendaji wake waendelee kuchapa kazi na sisi Waheshimiwa Wawakilishi tuwaunge mkono vizuri sana.

Mhe. Spika, naomba nimalizie kwa kuzungumzia Mamlaka ya Uwanja wa Ndege. Mhe. Spika, kwa muda mrefu sana kabla mimi sijawa waziri pale tangu niko *back bencher,* maana mimi nimefanya kazi *back bencher* miaka mitano, nimefanya kazi Naibu waziri, nimefanya kazi Waziri, nimefanya kazi Waziri asiye na wizara maalum. Kwa hivyo, mazingira ya Baraza hili karibu yote nimekumbana nayo na ninayaelewa. Kwa muda mrefu tulikuwa tukililia kwamba kwa nini uwanja wa ndege ni idara ya serikali badala ya kuwa mamlaka na mashirika.

Ilikuwa si kazi rahisi kujenga hoja kukubaliwa, na kuna kipindi nilipokuwa idara pale wakati mimi niko Waziri kuna siku moja tunasafiri na Katibu wangu mkuu nafikiri tunakwenda Pemba, lakini tulikuta pale kuna kitu cha shilingi 130,000/- kimeharibika, tukawauliza kwa nini kitu hiki kimeharibika? Wakasema sasa hivi tumeshaandika *voucher* iko hazina huu karibu mwezi, kwamba shilingi 130,000 mpaka ikaombwe Serikali Kuu, Katibu Mkuu akatoa pesa zake mfukoni akawapa wakenda kununua. Usingelimtarajia Meneja atoe shilingi 130,000 kwa sababu mshahara wake pengine shilingi 200,000, lakini sasa kutokana na mamlaka na mimi nataka nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Mamlaka na Mkurugenzi wao Mkuu, ukifika tu pale *airport* unaona pamebadilika kuanzia ndani mpaka nje ya uwanja kwamba kweli kuna mabadiliko.

Sasa niungane na Mhe. Ismail Jussa kwamba fedha wanazozalisha ndizo wanazotumia lakini unapoanzisha kitu kipya lazima utoe fursa, ingeliwezekana serikali ingelitoa ruzuku hasa pale kwa mamlaka kwa miaka fulani wakaipangia watumie chao na serikali iwape waimarishe eneo lile.

Mhe. Spika, mimi naunga mkono bajeti hii kwa sababu muda umekwenda niseme tu naunga mkono hoja na naomba Waheshimiwa wenzangu tuunge mkono hoja hii.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima na kutufikisha Ijumaa ya leo. Naomba nikushukuru na wewe mwenyewe kwa kunipa fursa hii ya kuchangia katika hoja ya Wizara hii ya Miundombinu na Mawasiliano. Tatu naomba pia nimpongeze Mhe. Rashid Seif kwa kupewa dhamana hii ambayo naamini ina changamoto nyingi, lakini kwa kupewa yeye ninavyoamini uwezo wake ni kwamba kwanza imerahisisha jambo moja. Ninavyoamini Mhe. Rashid Seif Suleiman anazo mbinu, sasa Baraza hili na serikali imsaidie tu kumpa miundo ili miundombinu ikamilike. Kwa hivyo, kwa kuweko yeye tayari zile mbinu zimeshatangulia sasa kinachosubiriwa tumsaidie kumpa miundo ili mambo yaweze kwenda.

Mhe. Spika, mimi naomba nichangie kwenye mambo mawili tu, suala la kwanza ambalo lilizungumzwa ni kuhusiana na kuwepo kwa mikataba miwili. Kwanza nitangulie kuungana na wale ambao walikuwa na wasiwasi juu ya suala hili na niwaambie kwamba hata upande wa serikali kwa kweli jambo hili lilileta kidogo fadhaa na lilitupa wasiwasi. Serikali nayo ilipata wasiwasi kwamba suala hili inawezekana kuna sababu nyingi na baada ya serikali kuliona hilo ikachukua hatua. Kwanza kulichunguza ilikuwaje, lakini na pili kuchukua hatua ya kulisawazisha ili likae sawa tuweze kuendelea na ule mradi wenyewe. Lakini kwa kadiri ninavyoamini, kwa kadiri ninavyofahamu ni kwamba hili suala la mikataba miwili silo lililosababisha ule mradi kusimama kipindi hiki ambacho ulikuwa umesimama, ulikuwa ni kwa sababu nyengine lakini tukasema wakati tutakapolisawazisha basi hili ni vyema nalo tulisawazishe kabisa twende mbele.

La kwanza katika suala hili ni kwamba, kweli serikali iliingia mkataba na ile Kampuni ya Kichina inayojenga pale *BCG* kwa US$ 57.5 milioni na hiyo ilikuwa ni mwezi Oktoba, 2009. Lakini wakati huu wa kusaini mkataba na baada ya hapo pia ilikubalika kwamba baadhi ya kazi zifanyiwe mapitio kwa kuongeza baadhi ya vifaa, kwa kuongeza baadhi ya vitu ambavyo vinatakiwa na ni muhimu kuwepo katika *airport* ya kisasa ambayo tunaitarajia kuwa nayo kwa Zanzibar.

Baada ya makubaliano ya kazi za kuongezwa Wizara ya Mawasiliano ikaomba serikalini idhini ya kufanya mapitio ya kazi zenyewe lakini pia na gharama za mradi, kumbukumbu zipo kwamba waliomba idhini hiyo serikalini nadhani tarehe 24 Oktoba na baadae serikali ikawajibu mwezi wa Novemba sikumbuki vizuri tarehe, lakini nadhani ni kama tarehe nne kwamba hiyo idhini imetolewa ya kufanya hayo mapitio. Na hayo mapitio yakaongeza gharama za mradi huu kufikia US$ 70.4 milioni. Sasa kosa ambalo lilifanyika na ambalo kwa kweli ndilo lililoleta fadhaa hii kwa mujibu wa mkataba wenyewe huu wa mwanzo uliosainiwa kama kuna marekebisho ni lazima marekebisho yale yafanywe kwa utaratibu maalum wa kuongeza nyongeza katika mkataba.

Lakini kwa urahisi Mhe. Spika, walioshughulikia suala hili ya kuwahi *dead line* ya kupeleka maombi ya mkopo huu katika hizi benki badala ya kufanya *addendum* wao wakaona labda njia rahisi ni kufanya marekebisho katika ule mkataba wenyewe na hili kwa kweli *technically* lilikuwa ni kosa. Kwa sababu lilipelekea sasa kuwa na hati mbili za mkataba ambao umesainiwa tarehe moja lakini una gharama tofauti. Sasa hilo bila shaka ni tatizo la kisheria na baada ya marekebisho hayo serikali ndio ikachukua hatua ya suala hili kulizungumza, kwa sababu hatuwezi kuendelea kwamba una hati mbili za mkataba zimesainiwa tarehe moja lakini zinazungumza gharama tofauti za mkataba.

Kwa hivyo, serikali ilichukua hatua, ikazungumza, ikapeleka ujumbe China kuzungumza na wahusika kuhusiana na suala hili na baadae tukakaa nao hapa hapa Zanzibar wakaja na haikuwa rahisi kuwafanya hata na wao kufahamu suala hili namna gani ya kulirekebisha, pengine wao walikuwa na wasiwasi. Lakini baada ya juhudi na kwa kweli mimi binafsi nilishiriki katika mazungumzo haya na niseme kwamba kuna *negotiation* ambazo ngumu niliwahi kushiriki ukiachia zile za *ZANTEL* nilikuwa nawaambia wenzangu kwamba zilikuwa *negotiation* hizi za kulisawazisha suala hili, lakini hatimaye Mhe. Spika, suala hili la mkataba angalau tulilisawazisha na tukakubaliana kufanya *ratification* ya yale mambo ambayo yalitokea, na sasa rasmi kisheria tunatambua kwamba tuna mkataba mmoja tu baina ya serikali na ile Kampuni ambayo inajenga katika mradi huu.

Nikiri na nikubaliane na waliosema kwamba hili kwa kweli lilifanyika kosa la kisheria, lakini halikuongeza gharama wala silo lililocheleweshe ujenzi pale *airport*, kuna mambo mengine ambayo nadhani tukiyatafuta ama wenyewe wizara wanaweza wakaja wakaeleza. Mimi nilitaka nilieleze hili na kuwatoa wasiwasi kwamba kwa sasa hivi baada ya kuzungumza na wenzetu tuna mkataba mmoja kisheria na ambao huo ndio tunaousimamia kufanya kazi ile ambayo sasa hivi inaendelea. Hayo masuala ya kwamba mradi labda ni ghali, gharama ni kubwa, hili ni suala la kiuchumi niseme.

Lakini nipende kuwatoa wasiwasi Waheshimiwa kwamba hili suala la kuwa unakopa lazima unapokopa utumie kampuni zao hili si suala la Wachina tu, tunakopa mara nyingi *BADEA* nao pia wana masharti yao, lazima kampuni itoke katika nchi za Kiarabu au za Afrika. Hayo ni katika masharti yao na kama kampuni inayofanya mradi ule haitoki katika nchi hizo haiwezi ku-*qualify* kupewa kazi ile na hiyo ni katika nchi nyingi utaratibu huo upo. Sasa suala la kwamba namna gani katika kufanya hii mikataba tuchukue hadhari, mimi nadhani ule ushauri uliotolewa ulikuwa ni mzuri, kwamba ni vizuri katika hili kwa sababu hata huko China hupewi kampuni hii ndio lazima ijenge. Wewe mwenyewe unatafuta na zipo nyingi na unatizama gharama ambazo ni nafuu, na kwamba unaona huwezi utatafuta njia nyengine lakini mimi niseme kwamba huu upo katika nchi nyingi na ni vizuri huo ushauri kwamba tuchukue hadhari, tutizame wapi tutapata nafuu labda, mimi naona ni ushauri mzuri.

Ingawa pengine wakati mwengine ni kutanabahishana tu kwamba katika chombo hiki ni chombo kikubwa, tunaposema no si lazima tuseme kwa lugha ambayo inayoweza kuleta pengine mtu mwengine au nchi nyengine ikatuona kama tunawatukana au tunawalaani. Wanasema wazungu kwamba, "*no without smile is very strong*".

Unaweza ukataa ukicheka na huko kukataa kwako kukawa madhubutu zaidi mtu akakuheshimu zaidi, pengine wala kukataa ukapiga kelele. Kwa hivyo kwenye hili ninadhani huo ushauri tumeuchukua na hasa katika suala la mikataba, kama nilivyosema tutachukua hadhari kubwa zaidi katika kuisimamia.

Suala la pili Mhe. Spika, ambalo ninaomba nichangia ni kuhusiana na suala ambalo lilizungumzwa sana hapa, kuhusiana na Kampuni ya ZAT kufanya kazi katika uwanja wa ndege. Hili kwanza naomba niwambushe Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza kwamba, kwanza hili ni suala la kisheria. Sheria tuliipitisha hapa kuhusu sheria ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege.

Ile sheria ukisoma kifungu 23 (5) kimeeleza wazi kwamba mikataba yote ambayo iliingiwa na idara au mamlaka nyengine nyengine kwa niaba ya idara kuhusiana na uendeshaji au shughuli yoyote ya uwanja wa ndege, baada ya miezi sita mikataba ita-expire, yaani kwa sheria ile mikataba iliikatisha, na iliikatisha ni kwa sababu kifungu chenyewe hicho hicho kifungu kidogo cha (4) kimesema kwamba uendeshaji wa shughuli pale hautakiwi sasa uwe wa *monopoly* kwa kadri itakavyowezekana.

ZAT ilikuwa na mkataba wa monopoly wa miaka 30. Kwa hivyo ilikuwa ni kufuata sheria wala serikali haikuwa na nia ya kuonea wala serikali haikuwa na nia ya kufanya vyovyote, ni sheria ambayo tuliipitisha Baraza hili hili, tena mwaka jana tu wala sio mbali. Sisi tulikuja na mapendekezo hapa serikali kwamba ile mikataba iendelee kwa muda wa miezi 12 baada ya sheria kuanza kazi, lakini Baraza hili hili likakataa likasema miezi 12 ni mingi, ni miezi 6 tu.

Sasa baada ya miezi 6 na ZAT mkataba wao kisheria haupo. Hili si suala la kwamba labda kuna mtu pengine kaonewa au kuna serikali haithamini juhudi na mambo ambayo ZAT wanafanya. Lakini la pili Mhe. Spika, kuhusiana na suala hili, sheria yenyewe inasema kwamba mamlaka inaweza ikawapa au ikaingia mkataba mwengine kwa masharti mengine na zile kampuni ambazo zilikuwa na mikataba ambapo kwa sheria mikataba yake itakuwa imefutika.

Mhe. Spika, naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe hasa waliozungumza suala hili kwa hamasa, kwamba serikali tulikutana nayo ZAT, tulichukua juhudi ya kukaa nayo ZAT tukaitisha vikao, tukawataka walete taarifa. Madhamuni ya kukaa nao, kwanza ni kujua uwezo wao wa kifedha na uwezo wao wa kiuendeshaji. Kwa sababu kwa kadri tunavyoipenda ZAT, kadri ZAT ilivyokuwa ni kampuni ya kizalendo lakini pale inashughulikia dunia nzima, haishughulikii Zanzibar peke yake.

Kuna vigezo vya kimataifa, kuna vigezo vya kitaifa namna ya kutoa huduma katika uwanja wa ndege kwa huduma ya namna ile. Sisi marekebisho tuliyofanya ya sheria nia yetu ni kuimarisha, kuleta ufanisi katika uendeshaji na utoaji wa huduma wa viwanja vyetu vya ndege.

Kwa hivyo tulikaa nao kuliangalia hilo kwa sababu yalikuwepo baadhi ya mambo tulihisi ni vizuri yarekebishwe ili kuendana na vigezo ambavyo sasa hivi vipo vya kimataifa na vya kitaifa.

Mengi ambayo tuliyagundua kwenye ZAT, kama tutayasema hapa, mimi ninadhani tutakuwa hatuisaidii ZAT wala hatuisaidii serikali. Naomba niwaambie wale Waheshimiwa Wajumbe

ambao walilizungumza hili kwa hamasa kuwa tukiyazungumza hapa, maana yake kwanza yatakuwa ni mambo yao ya ndani ya ZAT. Lakini mimi ninadhani kama kuna mtu anaipenda ZAT basi ni serikali. Kama kuna wengine wanaipenda ZAT basi wawasaidie yale mambo yao ya ndani yakae sawa na mimi labda nitasema machache tu ili isionekane labda tunasema tu.

La kwanza unataka kutoa huduma katika uwanja wa ndege pale, kuna vitu vya msingi lazima uwe navyo na vitu vile vya msingi unahitaji uwekezaji. ZAT yenyewe share capital yake ni milioni mia sita, ina shareholders wanne.

Lakini kampuni ambayo ina serious huwezi kuwa na wawekezaji ambao share zao wenyewe hazijalipiwa. Maana yake share zenyewe ni *non-paid up*. Sasa unapotaka kuekeza kitu cha kwanza unachokikimbilia ni hiyo share capital yako angalau ingelipwa. Sasa *share capital* kama haijalipwa, unapokwenda benki wenyewe, benki wanasema sisi hatukukopeshi.

ZAT imekopeshwa kwa kutumia security ya mtu binafsi ndani ya kampuni. Maana yake ZAT sasa hivi hivi ni kama vile inategemea *shareholder* mmoja. Imekopa badala ya kutumia assets za kampuni, inatumia assets za *individual shareholders* kwa mapenzi yake na imani yake kutaka iendelee, yeye ndio anayesema mimi ninatoa nyumba yangu kuweka *security*.

Kuna shareholder huyu mmoja yeye hata mshahara, maana kuna kampuni ambayo cash flow yake inashinda hata kulipa kwenye mshahara. *Individual shareholder* huyu ndiye anayelipa mshahara zipatikane ndio alipwe pesa zake. Ndio hayo mambo tuliyagundua.

Sasa tulitegemea hawa *shareholders* wengine kama wapo serious basi wauze hizi shares ama waingie ubia ama wachukue hatua nyengine, lakini ndani yenyewe ya ZAT inaonekana kwamba wenyewe hawajaamua hawa kuwa kampuni serious, baada ya shareholders niseme hawajaamua kuwa serious kwa ajili ya kuekeza opportunity waliyopewa kuekeza ni kubwa haiwezi kutokea. Kama kuna mtu anaipenda azungumze na hawa shareholders ili warekebishe mambo yao na fursa bado wamepewa.

Kwa hivyo mwisho baada ya yote hayo kuyagundua na tukaona tatizo liliopo na tukawashauri hatua za kuchukua. Hatua hizo hazijachukuliwa kwa sababu hili suala serikali haiwezi kulazimisha kuwaambia shareholders nyinyi mulipie shares zenu au au muuze shares zenu ili mupate mtaji wa kuweza kufanya kazi, serikali haiwezi kulazimisha.

Lakini serikali inathamini kwamba ina watu waliowaajiri pale ni kampuni ya kizalendo na katika spiriti ya sera ya serikali ya uwezeshaji ni vizuri wakapewa fursa. Ndio maana serikali ikaamua kwamba ZAT iendelee, yenyewe ichukue hatua za kurekebisha mambo yake lakini lazima tutoe fursa na wawekezaji wengine nao waweze kuja kuekeza katika uwanja wa ndege katika huduma hizi ili kuimarisha na kutoa ufanisi katika utoaji wa huduma wa uwanja wa ndege.

Hakuna ZAT iliyoonewa, kama ni kuionea basi ni wenyewe baadhi ya wenye hisa katika ZAT labda hawafahamu biashara namna wangeweza kutumia fursa hiyo, lakini hili si kulaumiwa serikali. Serikali imefuata sheria, utaratibu na imethamini sera yake ya uwezeshaji na ikaamua kuwaachia ZAT waendelee kutoa huduma, lakini kwa masharti mapya kwa mkataba mpya ambao serikali itaingia nao.

Hizi wengine wanaotaka kuitwa kuekeza ni kutoa fursa kwa ajili ya kuimarisha utendaji kwenye uwanja wa ndege na hilo ni jambo pia la kisheria. Kwa hivyo mimi nilitaka sana Waheshimiwa Wajumbe hili tulifahamu na hili tuwasaidie ZAT katika kujiimarisha na tusiisaidie ZAT kwa kuilaumu serikali, kwa serikali imefuata sheria na serikali yenyewe nayo inathamini vile vile mchango huu wa ZAT.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, naomba nitamke kwamba ninaiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia na nirejee nitangulia mwanzo kusema, niwaombe Waheshimiwa Wajumbe tumsaidie Mhe. Waziri kumpa miundo achanganye na mbinu zake ili mambo yaweze kwenda.

Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, awali ya yote na mimi sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehma lakini pia kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi na mimi kusema mawili machache katika mnasaba wa bajeti hii ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano.

Mhe. Spika, mimi mchango wangu wa sehemu kubwa utakuwa ni sehemu ya kutoa ufafanuzi wa baadhi ya sehemu ya masuala yaliyoulizwa Waheshimiwa Wajumbe na michango yao.

Lakini kabla ya hayo Mhe. Spika, naomba nichukue nafasi hii mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Chwaka niseme kwamba tunaunga mkono hoja hii asilimia mia moja kwa moja.

Mhe. Spika, miongoni mwa changa moto ambazo zilizoulizwa ni ilikuwa ni suala barabara katika Jimbo la Chonga. Ninapenda kumuhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba barabara hizo zinafanyiwa kazi na ninaomba akirudi kwenye kitabu chetu cha bajeti aangalie kiambatanisho kwenye ukurasa wa 77 katika barabara nambari 6 barabara husika imetajwa.

Lakini pili ni kwa barabara inayotoka Mazizini hadi Chukwani, suala la matuta ninamuhakikishia Mhe. Mwakilishi na Baraza lako Tukufu kwamba wizara yetu kupitia Idara yetu ya UUB itapitia matuta haya na ikiwezekana kuyaondoa kabisa, kwani kama alivyoeleza Mhe. Mwakilishi kwamba hayaonekani tija iliyokusudiwa kwenye matuta haya.

Suala la tatu Mhe. Spika, ilikuwa ni barabara inayotoka Mbweni, Baraza la Wawakilishi hadi maeneo ya uwanja wa ndege, kuhusu suala la alama. Suala hili tumelipokea na tutalifanyia kazi.

Suala la nne ilikuwa Mhe. Spika, ni suala la around about katika eneo la kwa Mchina. Suala hili tumelipokea na mipango yetu kwamba kutokana na fedha tutakazozipata katika mfuko wa barabara, ukiangalia katika kiambatanisho ukurasa wa 71, barabara nambari nne suala hili limezingatiwa kwa msingi huo kwamba around about tutaijenga katika eneo la kwa Mchina kama maoni na ushauri alioutoa Mhe. Mwakilishi.

Mhe. Spika, suala jengine lilikuwa ni suala la barabara za ndani ambalo limetokana na Mhe. Saleh Nassor Juma. Ninamuhakikishia kwamba akiangalia kiambatanisho katika ukurasa wa 76

kuna barabara nambari 3 ambayo katika mpango wetu wa routine maintenance ambayo ipo katika Jimbo la Wawi, ninamuhakikishia kwamba kazi hiyo tutaifanya kama tulivyokusudia.

UTARATIBU

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri anajibu hoja zetu lakini hatumsikii vizuri. Sasa naomba asimame pale ili tuweze kumsikia ili tuweze kuelewa anachokizungumza.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, kwa idhini yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano na mimi naomba nitoe mchango wangu katika kutoa ufafanuzi wa baadhi ya vifungu na suala la michango iliyoulizwa na Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Spika, naomba nirejee kama madai ya Mhe. Mwakilishi kwamba hanisikii vizuri. Suala la kwanza lilikuwa ni mchango uliotokana na Mhe. Abdalla Juma ambaye amezungumzia masuala ya barabara jimboni kwake.

Majibu yetu ni kwamba ukiangalia kitabu chetu cha bajeti ukurasa wa 77, barabara nambari 6 ime-concern barabara husika kwenye jimbo lake. Lakini barabara hiyo itajengwa kwa mfuko wa barabara na barabara nyengine za jimboni tutazijenga kwa mfumo ule ule wa kushirikiana na Halmashauri na viongozi wa jimbo.

Suala la pili la Mhe. Abdalla Juma ilikuwa ni barabara inayotoka Mazizini hadi Chukwani ambaye alizungumzia suala la matuta. Mhe. Spika, tulichokieleza kwamba matuta hayo tutayaondoa kwa kupitia Idara yetu ya UUB, kwani tija iliyokusudiwa haionekani.

Suala la tatu ilikuwa barabara ya uwanja wa ndege hadi Baraza la Wawakilishi kusema kwamba inahitaji alama. Suala hilo tumelipokea na tutalifanyia kazi kwa fedha zinazotoka kwenye mfuko wa barabara.

Suala la nne lilikuwa ni suala la *round about* katika eneo la kwa Mchina, tumelipokea na tunalifanyia kazi, ukiangalia kiambatanisho ukurasa wa 71 barabara nambari 4 imeonesha concern kwa ajili ya kujenga around about katika eneo hilo la kwa Mchina.

Mhe. Spika, mtu wa pili alikuwa ni Mhe. Saleh Nassor Juma ambaye alizungumzia suala la barabara kwenye jimbo lake la Wawi, na yeye pia ukiangalia ukurasa wa 76 barabara nambari 3 ni miongoni mwa barabara ambazo tutazifanyia ukarabati katika routine maintenance ya mradi wetu kupitia mfuko wa barabara.

Vile vile katika Jimbo la Wawi barabara ya Wawi/Mgogoni imefanyiwa matengenezo wa ujenzi wa culvert tatu na katika mwaka wa fedha 2012/2013, imepangiwa kufanyiwa matengenezo kwa kiwango cha kifusi kupitia mfuko wa barabara. Ukiangalia ukurasa wa 77 barabara nambari 5 inahusika.

Mhe. Spika, suala jengine lilikuwa ni suala la uchimbaji wa kifusi katika maeneo ya Makaani/Vitongoji. Kuhusu uchimbaji wa kifusi kwenye hilo na maeneo mengine, wizara hivi sasa yanafuata maelekezo yanayotokana na Idara ya Mazingira katika uchimbaji wa kifusi. Pia imeanza kuyashughulikia matatizo yaliyojitokeza kabla ya kuanza kutumika kwa utaratibu huu.

Msingi mkubwa ni kwamba tunahakikisha kwamba maelekezo yanayotoka kutoka kwenye Idara ya Mazingira kuona maeneo ambayo yamechimbwa kifusi yanarejeshewa hali yake halisi inafanyiwa kazi.

Mhe. Spika, suala jengine ni suala linalotokana na Mhe. Jaku Hashim ambaye alitaka kujua barabara ya Bwawani hadi Malindi. Barabara hii katika hatua ya awali jana mafundi wetu wa UUB wamemaliza utiaji wa viraka lakini pia ipo katika mpango wetu ukiangalia ukurasa 71 barabara nambari 4 itafanyiwa ukarabati mkubwa wa kuweka eneo lote la karibu mita 270 kulifanyia over ling ya lami.

Suala jengine ilikuwa ni barabara ya Mfumbwi. Mhe. Spika, barabara hii tunachoweza kumuahidi Mhe. Mwakilishi kwamba tutaifanyia grading kwa eneo lote lile linalotoka Mfumbwi hadi Kibigija ili kuweza kuruhusu shughuli za upitaji na matumizi mengine ya barabara kama yalivyo kawaida.

Suala jengine Mhe. Spika, ilikuwa ni suala la Mhe. Suleiman Hemed ambaye ni Mwakilishi wa Jimbo la Konde, aliuliza suala la barabara iliyopita msitu wa Ngezi. Mhe. Spika, barabara iliyopita msitu wa Ngezi ina hatua mbili. Hatua ya kwanza kuna kilomita moja kabla ya kufika kwenye msitu wenyewe ambayo tutaijenga kwa mfuko wa barabara.

Lakini kati kati ya msitu wa Ngezi wenyewe kuna karibu kilomita ambazo tutazijenga baada ya kuzifanyia study na tutajenga kwa mfumo wa kuchanganya mchanga na chokaa, ili kunusuru mazingirra kama vile ambavyo tumeelekezwa baada ya kukaa na taasisi husika. Lakini baada ya msitu huo kuna kilomita ambazo nazo pia zitajengwa kwa kiwango cha kifusi kwa fedha ambazo zinazotoka kwenye mfuko wa barabara.

Suala jengine ilikuwa ni ujenzi wa daraja kwenye barabara ya Mkia wa ng'ombe katika mwaka wa fedha 2012/2013, daraja hilo litajengwa kwa fedha kutoka mfuko wa barabara, ukiangalia ukurasa wa 79 barabara nambari 2.

Mhe. Spika, suala jengine lilikuwa ni suala la Mhe. Hija Hassan Hija ambaye alitaka kujua msimamo wa barabara ya Mgagadu/Kiwani. Katika mwaka uliopita barabara hiyo iliingiziwa jumla ya shilingi milioni mia mbili katika fedha zilizoombwa za milioni mia tatu kutoka Hazina. Ujenzi wa barabara hii utaendelea katika mwaka wa fedha 2012/2013 hadi pale ujenzi utakapomaliza kama ulivyopangiwa.

Mhe. Spika, suala jengine lilikuwa ni suala la barabara ya Ole/Kengeja. Tumesikiliza concerns za Waheshimiwa Wawakilishi na sisi kama Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano tutarudi tena serikalini kwenda kutafakari juu ya maamuzi sahihi juu ya ujenzi wa barabara.

Lakini pia liliulizwa suala la ujenzi wa barabara ya Amani/Mtoni, fedha zilizotumika kwa kazi za ujenzi wa kiwango cha kifusi, subbase yenye urefu wa kilomita tatu na ujenzi wa ma-culverts yenye mahitaji. Aidha lami tani mia tatu na kumi zimenunuliwa. Kwa maana zile ambazo tunazozipata kutoka wenzetu wa SMT zimetumika na zimeisha na maamuzi ya serikali kuona kwamba barabara hii inamalizwa kwa fedha zitakazotoka katika mfuko wa barabara. Ukiangalia katika mpango wetu wa mfuko wa barabara, barabara hii nayo itamalizwa katika mwaka huu wa bajeti 2012/2013.

Mhe. Spika, suala jengine lilikuwa ni suala la fidia ambalo aliliuliza Mhe. Ali Salim Haji. Suala hili la fidia nalo ni miongoni mwa changamoto za serikali katika miradi yetu mikubwa. Ninachotuweza kumuhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba kwa kadri ya hali ya fedha ambazo tutazipata suala la fidia nalo tutaendelea kulilipa kidogo kidogo kwa maeneo yote. Lakini msimamo wa wizara yetu, msimamo wa serikali ni kuhakikisha kwamba tutakapojenga barabara popote hakuna nyumba ya mwananchi yeyote itakayobomolewa bila ya kumlipa fidia. Tutaendelea na utaratibu wetu wa kukata miti na vipando kwa ajili ya kuvipisha miradi ya barabara lakini hatutovunja nyumba mtu yeyote kabla ya kumlipa fidia.

Mhe. Spika, pia Mhe. Asaa naye alitaka kujua barabara za Wete na yeye pia akiangalia katika kiambatanisho husika cha 77. Pia Mhe. Mohamed Said alitaka kujua barabara ilitiwa rojo kwa muda mrefu. Ni kweli barabara hiyo ilifanyiwa matengenezo kwa kushirikiana na Mhe. Mbunge na Mhe. Mwakilishi aliyepita awamu iliyopita. Kwa kiasi kikubwa barabara matengenezo ya barabara hiyo ilikuwa katika hali mbaya.

Wizara kwa kupitia Idara ya UUB ilichangia zana za ujenzi, lami, maji na wataalamu. Lengo la kutiwa rojo kwa barabara hiyo ilikuwa ni kuhami ili isiharibike kwa muda mfupi. Kwa hivyo tunamshauri Mhe. Mwakilishi yeye pamoja na Mhe. Mbunge waendelee kushirikiana na Idara yetu ya UUB na barabara hiyo tutaijenga kwa kupata michango na hisani yao, na mchango wa idara yetu utaendelea kama ulivyoahidiwa hapo awali.

Ombi la kuweka matuta kwa Mchina mwanzo na maeneo mengine aliyoyataja Mhe. Mwakilishi, utaratibu tumeshaeleza kwamba suala la uwekezaji matuta sio kipa umbele kwa wizara yetu. Tunachoweza kumuhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba tutaweka alama stahiki za kuongoza matumizi bora ya barabara.

Aidha Mhe. Mohamed Khalid wa Jimbo la Mtambile alitaka kujua barabara ya Ole/Kengeja, maelezo kama nilivyotoa awali. Pia Mhe. Ismail Jussa Ladhu Mwakilishi wa Jimbo la Mji Mkongwe alitaka kupata ufafanuzi juu ya matumizi ya baadhi ya fedha zilizotumika kwenye ujenzi wa barabara ya Amani/Mtoni.

Ufafanuzi wake ni kama hivi ifuatavyo. Ununuzi wa kifusi ulikuwa ni shilingi mia moja na arobaini na nne kutoka kwenye machimbo ya kampuni ya Salum *Civil Engineering* uliofanyika baada ya Idara ya UUB kupata idhini ya Bodi ya Zabuni ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano.

Idara haikuwa na uwezo wa kuchimba kifusi katika machimbo yake ya Kibele kwa wakati huo kutokana na uchakavu wa zana na uharibikaji wa zana pamoja na vyombo. Aidha lami

iliyonunuliwa ilikopeshwa kampuni ya MECCO, tayari lami hiyo imesharejeshwa siku ya tarehe 28 mwezi pili 2012, lami tulikabidhiwa kwa ushihidi. Lakini pia asilimia 23 ya fedha zilizotumika kwa kazi za ujenzi wa barabara ya Amani/Mtoni zilitumika kwa ajili ya matengenezo ya zana na vyombo ambavyo vilikuwa vipo katika hali mbaya ya uchakavu na kuharibika.

Pia asilimia 4 ya fedha zilizotumika kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo zilitumiwa kwa ajili ya ulipaji wa maposho ya watendaji wetu waliokuwa wakishiriki katika zoezi hilo.

Pili pia Mhe. Spika, Mhe. Jussa alitaka kujua barabara ya Mwembetanga/Mtendeni hadi Darajarani. Wizara kwa kushirikiana na Mhe. Mbunge na Mhe. Mwakilishi wa Mji Mkongwe wataifanyia matengenezo barabara hiyo kwa kiwango cha lami. Makadirio ya gharama ya kazi hiyo ni shilingi milioni 65.

Tayari fedha taslimu shilingi milioni 40 zimechangwa na viongozi hao na zimeingizwa katika mfuko wa kuchochea maendeleo jimboni na Mhe. Mbunge wa Mji Mkongwe kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hiyo. Sambamba na ujenzi wa barabara hiyo wizara itaifanyia matengenezo makubwa barabara ya Mkunazini kwa fedha kutoka mfuko wa barabara katika bajeti hii ya mwaka 2012/2013.

Mhe. Spika, mheshimiwa mwengine aliyeuliza alikuwa ni Mhe. Viwe Khamis aliuliza suala la kuweka matuta barabarani. Utaratibu ni ule ule kuhakikisha kwamba maeneo yote ya barabara yanaekwa alama maalum ya kuongoza matumizi mazuri ya barabara na uwekaji wa matuta sio kipa umbele kwa wizara yetu.

Barabara ya Penjuwani mjini Kiuyu imo katika kazi wa mpango wa kazi za maendeleo za kazi za kawaida chini ya usimamizi wa mfuko wa barabara. Katika bajeti hii ya mwaka 2012/2013 barabara hiyo tutajenga kwa kiwango cha kifusi.

Mhe. Omar Ali Shehe wa Jimbo la Chake-Chake alitaka kujua mashirikiano kati ya Wawakilishi na Idara yetu ya UUB. Ninamuhakikishia kwamba mashirikiano yetu yapo na tunaomba tuendelee kuwepo ili kuwapelekea huduma hizi wananchi wetu kwa urahisi zaidi. Pia alitaka kujua mgawanyo wa barabara kwa mujibu wa sheria.

Kwa mujibu wa sheria ya *Road Decree Act* iliyotungwa 1957, barabara zimegawika katika sehemu kuu zifuatazo. Barabara kuu, barabara ya vijijini, barabara zinazounganisha barabara kuu na barabara za vijijini na barabara za mjini.

Barabara zote hizi zimetajwa kwa majina katika sheria hii na zinazoshughulikiwa na wizara yangu kwa hivi sasa. Barabara ambazo hazikuainishwa katika sheria hii, zinashughulikiwa na Halmashauri za Wilaya husika na wizara yangu hutoa msaada wa kiufundi, vifaa pale kila hali inapostahiki.

Mhe. Spika, pia Mhe. Shawana Bukheit Hassan alikuwa na suala la barabara za ndani. Ninapenda kumuhakikishia kwamba wizara yetu itaendelea kushirikiana na Halmashauri kuhakikisha kuwa barabara hizi za ndani zinaimarishwa ili kutoa huduma kwa wananchi wetu.

Pia Mhe. Mahmoud Mahamed wa Jimbo la Kikwajuni ameshauri utengenezaji wa barabarani pembezoni kuweka capson. Suala hili tumelipokea na tunaanza kulifanyia kazi na ukipita hivi sasa barabara yetu ya Kinazini tayari zoezi hili limeanza.

Ushauri kuhusu uwekaji wa alama za usalama katika eneo la Kisiwandui. Tumelipokea na tutashirikiana na wenzetu wa Baraza la Manispaa kuweka zebra katika eneo linalohusika.

Suala la Mhe. Mohamedraza wa Jimbo la Uzini barabara kugeuzwa maeneo ya gereji na kuoshea magari. Ni kweli tatizo hili lipo katika mji wetu na naomba tu Mhe. Spika, kwamba sisi kama viongozi wa wananchi tuendelee kukemea jambo hili. Kwani ni kweli kwamba gharama za ujenzi wa barabara ni kubwa na matengenezo haya yanayofanyika barabarani yanachochea kuharibika kwa barabara.

Lakini pia suala la uegeshaji wa magari, kufanya parking ya magari katika barabara zetu usiku kucha nalo pia ni kichocheo cha uhabirifu wa barabara. Kwa sababu magari yetu yanavuja oil, oil ambayo ni lubricant ikigusa lami inaendelea kuathiri miundombinu na uimara wa barabara husika.

Lakini pia Mhe. Hamza alitaka kujua na kutoa ushauri wa barabara ya Amani/Mtoni hasa kwenye maeneo ya pembezoni katika daraja la garagara liwekwe mikingo. Ushauri huo tunauchukua na tunaufanyia kazi na tunahakikisha kwamba tutaweka mikingo hiyo. Ujenzi wa madaraja ufanyike ukaguzi wa kina. Suala hili tunalichukua na tunaendelea kufanya kazi kama ulivyoshauri.

Ujenzi wa barabara Shaurimoyo/Mboriborini fedha za maeneo korofi na barabara hiyo zimetengwa katika bajeti ya mwaka huu kupitia mfuko wa barabara. Ninamuhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba kazi hiyo tutaifanya kwa uadilifu mkubwa na kwa ushirikiano wa karibu atakaotupa yeye pamoja na Mbunge wake.

Mhe. Kazina Khamis Kona alitaka kujua utaratibu wa madaraja yote yaliyoelekea Kaskazini tuna mpango gani serikali. Ukiangalia katika mpango wetu wa mradi ule mkubwa wa barabara zinazoingia mjini, madaraja haya takribani matano yamehusishwa. Katika hatua ya awali tunachokifanya sisi ni kuyaimarisha, kujenga vyuma ili kuashiria kujenga ule usalama wa matumizi ya barabara.

Lakini kwa bahati mbaya wananchi wetu wamekuwa wakiharibu miundombinu hii. Niombe tu Mhe. Spika, na nichukue nafasi hii kuwaomba sana wananchi wetu watupe kila aina ya ushirikiano wa kuitunza miundombinu, kwani kuwepo kwake imara kutaokoa maisha ya wananchi ambao hawana hatia na kinyume yake tutaendelea kuwakandamiza wananchi wetu kuingia katika majanga.

Pili alitaka kujua barabara ya Tumbatu kutoka Kichangani hadi Jongowe. Ninamuhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba suala hili kwa kupitia mfuko wa jimbo na ushirikiano wa Halmashauri

husika tunaamini kwamba idara yetu itaendelea kutoa vifaa, wataalamu katika kuikarabati ili kuweza kupitika kwa karibu.

Aidha Mhe. Asha Abdi Haji alitaka kujua kuhusu barabara ya Mwanakwerekwe makaburini hadi Tunguu kujengwa njia mbili. Nalo hili pia limo katika mpango mkuu wa barabara zinazoingia mjini kwamba tutafanya hiyo double way. Lakini suala la ukarabati kutoka Mwanakwerekwe hadi Makunduchi linafanyiwa kazi na hivi sasa ukipita maeneo kutoka Kitogani kuelekea Kusini, suala hilo limefanyiwa kazi kwa sehemu kubwa.

Mhe. Spika, suala jengine lilikuwa ni suala la katika Idara ya Mipango. Barabara ya Ole/Kengeja kama tulivyoeleza, barabara ya Wete/Gando, changamoto inayopelekea barabara hiyo kuchelewa. Ni kweli kuwa kazi imechelewa kukamilika au kasi ya utekelezaji wa mradi huu unakwenda kidogo kidogo.

Lakini miongoni mwa changamoto ambazo zinapelekea mradi huu kuchelewa ni pamoja na kulipa fidia za vipando, kuondoshwa kwa mabomba ya maji, nguzo za umeme ili kumpa eneo la mkandarasi. Lakini pia serikali tumekuwa tukichelewa kumlipa lakini pia wafadhili wa mradi huu nao pia wamekuwa wanachelewa kumlipa. Anapochelewa kulipwa mkandarasi anapelekea kuondosha baadhi ya staffs kwa sababu wanakuwa hawana kazi na yeye anakuwa anawalipa bure.

Kwa hivyo imani yangu kwamba serikali tutaendelea kumlipa kwa wakati lakini pia tutaomba wenzetu wanaotufadhili katika mradi huu kulipa kwa wakati ili kunusuru mradi umalizike kwa muda uliopangwa. Matarajio ya mradi huu utamalizika katika bajeti hii 2012/2013 kama tulivyokusudia.

Barabara ya Wete/Konde itamalizika lini. Majibu ni hayo lakini pia fedha zilizotengwa kwa mwaka huu wa fedha zitatumika kulipa mchango wa SMZ kwenye mradi huu, kwani mkandarasi anadai hivi sasa kiasi takribani shilingi milioni mia tano pamoja na fidia ya bilioni moja milioni mia mbili thamanini na saba, na mchango wa SMZ kwenye mradi huu imebaki ni bilioni tatu, milioni mbili hamsini na moja laki tatu sitini na elfu mia mbili na kumi.

Mhe. Mohamed Said wa Jimbo la Mpendae alitaka kujua Idara ya Mipango imefanya tafiti ngapi. Idara imefanya tafiti nyingi. Miongoni mwao ni kuhusu na matumizi ya udongo na chokaa katika ujenzi wa barabara katika eneo la msitu wa Ngezi. Lakini pia idara inaendelea na utaratibu wa kuibua maeneo ya utafiti katika sekta ya barabara na usafiri wa nchi kavu na baharini katika kugundua changamoto na matokeo yanayotokezea sababu ni nini utafiti unaendelea.

Lakini pia idara inaendelea na utafiti katika mradi wetu mkubwa wa Zanzibar *Transport Master Plan* ili kuweza kushauri kwa namna gani serikali inaweza kutekeleza mradi huu vizuri ambao utaweza kuleta tija kwa wananchi wetu.

Lakini pia suala la utekelezaji wa Zanzibar *Master Plan*, utekelezaji wake mpango mkuu wa usafiri Zanzibar unaendelea kama ulivyopangwa na unatarajiwa kwamba wenzetu wa ADB wataungana mkono katika ufadhili wa mradi huu.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk alitaka kujua malipo ya fidia ya wananchi katika barabara ya Mfenesini/Bumbwini. Malipo ya barabara hiyo yamefanyika kwa Shehia ya Mangapwani, Kiombamvua, Kidazini, Fujoni, Mkadini. Shehia zilizobaki ni Bumbwinimakoba ambao wanadai shilingi milioni kumi na moja laki tatu na mia nane.

Shehia ya Kama wanadai milioni arobaini na tatu, laki nne elfu sabini na nane mia tano na hamsini. Shehia ya Misufini milioni kumi na nane laki, elfu tatu mia nane hamsini na moja.

Bababara ya Amani/Dunga madai ya fidia ni shilingi milioni ishirini na nane laki moja elfu sabini na nne mia moja na saba nukta tano. Barabara ya Kinyasini/Tunguu ni shilingi milioni thalathini mbili.

Aidha alitaka kujua ni kiasi gani kinatumika kwa fidia ya nyumba na vipando. Takribani tumeweza kutumia karibu shilingi bilioni moja nukta tano kwa ajili ya kulipa fidia katika miradi yote.

Fidia ya mazao ya nyumba zinazoathirika baada ya ujenzi zimetengwa kwenye bajeti hii, tumetenga karibu takribani shilingi million mia tatu hamsini kati ya shilingi hiyo bilioni moja nukta tano zinatumika kumlipa mkandarasi.

Mhe. Jussa alitaka kujua mradi wa uzio na kuunganisha na mradi wa maegesho ya njia ya kupitia ndege. Mhe. Spika, kama alivyoeleza Waziri asiyekuwa na Wizara Maalum kwamba concern ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano inatokana na mradi mkubwa ambao tumefadhiliwa na wenzetu wa World Bank. Wakati ule ambao wanatufadhili mradi wa run way walitoa pendekezo kwa serikali kuimarisha ukuta, kwa maana ya ile fensi inayozunguruka uwanja wa ndege.

Kwa sababu mradi wa run way ulikuwa umemalizika na mradi uliokuwa unaendelea hivi sasa ndio sasa ukaona mradi huu wa ukuta umeunganishwa katika mradi wa maegesho na tax kwa maana ya kupata *philosophy* ile ile ya kuimarisha maeneo ya *tax, apron* na kuimarisha ukuta ili zana iliyokusudiwa kwamba ikiimarika *tax, apron, run way* na ukuta nao ukiwa salama, yaani maudhui ya serikali ya kuwa na uwanja salama ambao utajikinga na majanga yatakuwa yamefikiwa.

Lakini mradi wa barabara zinazoingia mjini, kuna baadhi ya barabara zinajengwa. Madhumuni makubwa ya barabara zinazoingia mjini kuna hatua mbili. Kuna baadhi ya barabara ambazo zitavunjwa zote na kujengwa upya, kuna baadhi ya barabara zitatanuliwa lakini pia kuna baadhi ya barabara ambazo zitaongezwa pembezoni kwa ajili ya kupata watumiaji wengine wa miguu, walemavu na ma-pedestrians.

Kwa hivyo maudhui ni kwamba miradi hii inayojengwa kuna barabara hazitovunjwa. Ndio maana huu mkubwa tunaoutegemea wa barabara zitakazoingia mjini hautoathiri kwa maeneo yote. Kwa hivyo kwa barabara ambazo tunaendelea kujenga nyengine zitaendelea kuwepo na barabara nyengine ambazo zipo mjini zitavunjwa ili kuendana sambamba na mpango huo wa mradi wa barabara zinazoingia mjini.

Aidha Mhe. Hamza alitaka kujua shimo lilichimbwa na kampuni ya MECCO limited katika ujenzi wa barabara ya Mfenesini/Bumbwini halijafukiwa. Kwa mujibu wa kampuni hiyo linatakiwa kufanyiwa matengenezo ya shimo ambalo wamechimba kifusi baada ya kumaliza kufanya matengenezo hayo, msimamizi wa mradi atakagua ili kuona kama kazi hii imefanyika vizuri.

Ninachopenda kumuhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba utaratibu wa mkataba unaelekeza wazi kwamba kabla ya kumaliza malipo yake mkandarasi anatakiwa arejeshe hali ya uhalisia wa eneo ambalo amechimba kifusi. Ninamuhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba kama kampuni ya MECCO haitorejesha uwasili wa eneo ambalo wamechimba kifusi, basi serikali ita- *retain* malipo yake ya mwisho hadi hapo atakapofanya ndio atamaliziwa malipo yake. Kwa msingi huo namuhakikishia kwamba atarejesha uwasili wa eneo ambalo amechimba kifusi, ili kuweza kupata malipo yake na ikiwa hakufanya hivyo, basi tutatumia pesa hizi za *retain* kurejesha uwasili wa eneo hilo ambalo tumekubali kwa mujibu wa mkataba tuliokubaliana na mkandarasi huyo.

Aidha, suala la mradi wa uwanja wa ndege Pemba, vipi *ADB*. Wizara kwa kupitia Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ilikubaliana na *ADB* kuwa SMZ ifanye upembuzi yakinifu ya kutayarisha hadidu rejea za upembuzi yakinifu, ambazo zitaendana na matakwa ya benki hiyo. Kazi ya kutayarisha hadidu rejea kwa kuzingatia mahitaji ya *ADB* zimekwishakufanyika, ambapo katika bajeti ya mwaka huu wizara imetenga fedha za utekelezaji wa upembuzi yakinifu huo. Mara baada ya kukamilika upembuzi yakinifu huo utawawezesha *ADB* kwa ajili ya mazingatio na ufadhili kama tulivyokubaliana.

Suala jengine lilikuwa ni suala la Mamlaka ya Usafiri Baharini, Mhe. Abdalla Juma alitaka kujua kama mamlaka je, inawataalamu wa kutosha. Napenda nilithibitishie Baraza lako tukufu kwamba mamlaka inaupungufu mkubwa sana wa wafanyakazi, hasa wataalamu. Kwa hivyo, ni matarajio yetu kwamba katika mwaka huu mamlaka ikiruhusiwa kuanza kutumia mapato yake, pale itakaporuhusiwa kufungua *account* na kuingiziwa fedha, basi imani yetu ni kwamba mamlaka itatumia nafasi hiyo kuwaajiri watu wenye sifa na watakaokidhi mahitaji yaliopo. Hivi sasa tuna *chief inspector* mmoja tu, jambo ambalo halikidhi mahitaji ya mamlaka.

Kwa hivyo, namthibitishia Mhe. Mwakilishi kwamba tuna mapungufu tena mapungufu makubwa ya wataalamu katika mamlaka hii. Uuzaji wa tiketi za ziada, mamlaka imekuwa ikiwaandikia makampuni ya meli kuacha kuuza tiketi za ziada za abiria walioruhusiwa tiketi. Ni imani yetu kwamba suala hili serikali imelipigia kelele sana kuona kwamba linafanyika kwa mujibu wa taratibu na kuheshimu sheria ziliopo. Aidha, suala la uuzaji wa tiketi kiholela, mapungufu yaliopo ni kwamba sheria yetu bado tuna mapungufu ya kanuni. Kwa hivyo, ni matarajio yetu kwamba tukizifanyia kazi kanuni, tutakuwa tuna usimamizi mzuri katika maeneo haya ya uuzaji wa tiketi kiholela na tiketi ambazo zitakuwa zimezidi kiwango husika.

Aidha, suala jengine ni kwamba kwa nini mamlaka inasajili meli mbovu. Mamlaka haijawahi kusajili meli mbovu, meli zote zilizosajiliwa zinafuata taratibu zilizowekwa na ikibainika meli yoyote kuwa itakuwa na matatizo yoyote kwa mujibu ya mamlaka aliyopewa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka katika sheria nambari 5 ya mwaka 2006, sheria ya *ZMA*, ana mamlaka ya kuizuwia na kuendelea kufanya uchunguzi kama atakavyohisi yeye inafaa.

Mhe. Mahmoud Muhamed Mussa, alitaka kujua maslahi ya mkaguzi wa meli. Ni kweli kwamba maslahi ya wafanyakazi wetu bado ni madogo, hayalingani kabisa na majukumu makubwa na mazito waliyoyabeba. Mfano wakaguzi wenzetu wa Tanzania Bara, mkaguzi mwenye sifa *Fist Class Marine* analipwa mshahara mkubwa, ambapo kwa hapa Zanzibar bado hatujaufikia. Ni matarajio yetu kwamba mamlaka hii itajipangia mishahara mizuri kwa mujibu wa kipato chao na mahitaji halisi ya wafanyakazi wetu na wataalamu wetu hawa.

Suala la Mhe. Ismail Jussa Ladhu, alitaka kujua mapato ya mamlaka ya usajili. Mapato ya mamlaka yanaonekana na katika mwaka wa fedha uliomalizika, mamlaka ilivuka lengo lililowekwa kwa kukusanya asilimia 230 ya malengo yaliyokusudiwa ya *ZMA*.

Mapendekezo ya tume ya ajali ya *Spaice Islander*, kwa sehemu kubwa hayajatekelezwa kutokana na ukosefu wa fedha. Mfumo wa mamlaka unahitaji fedha kutengeneza kanuni, mpaka leo hii hazijapatikana, mamlaka haiwezi kufanya kazi kiukamilifu kama haina angalau kanuni 40, kati ya mahitaji ambayo kanuni zinazohitajika. Kwa hivyo, msingi wetu ni kwamba tukipata fedha hizi, tutaweza kutengeneza kanuni ambazo zitaipa nguvu mamlaka katika usimamizi mzuri wa shughuli zetu za kazi za kila siku. Kwa nini hakuna vifaa vya kufanyia kazi, imani yetu kwamba tatizo ni fedha.

Mhe. Hamza Hassan Juma, kuhusu sifa za katibu wa bodi ya mamlaka. Sio kweli kwamba mamlaka haijapata katibu wa bodi mwenye sifa za sheria kama ilivyotakiwa. Hata hivyo, mamlaka kwa hivi sasa inamtumia katibu wa bodi ambaye ana uzoefu mkubwa katika shughuli hizi na amefanyakazi za ukatibu wa bodi kwa muda mrefu hivi sasa, mamlaka ipo katika taratibu za kumpata katibu mwengine atakayeweza kum-*replace* katibu aliyepo. Orodha ya meli zilizosajiliwa hazionyeshi nchi ziliopo, nchi zilikotoka kwa mujibu wa sheria ya *Zanzibar Maritime Authority Act* nambari 5 ya mwaka 2006, meli ikitaka kusajiliwa haiangaliwi nchi ilikotoka, inaangaliwa umiliki wa meli hiyo na uhalali wa umiliki wa meli hiyo, pamoja na usajili uliokuwepo kabla ya kufutwa au huu ni utaratibu wa dunia nzima na si kinyume kama wanavyofanya wenzetu.

Pia Mhe. Ismail Jussa Ladhu alitaka kujua *Filtex* wanatuma pesa kwa njia gani. Wakala wetu wa *open registry* aliyeko Dubai, kampuni ya *Filtex* inatuma pesa kwa njia ya *telegraph transfer* ambao ni utaratibu wa kibenki na unakubalika kwa mujibu wa taratibu za serikali, kwenda katika *account* ambazo kwa sasa ziko chini ya Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Taratibu za usajili wa meli ni kama ifuatavyo.

Kwanza mtu anayeleta maombi anatakiwa kuleta *document* halali za umiliki wa meli hiyo, pamoja na *document* za meli yenyewe, baada ya uhakiki wa *document* hizo, tunampeleka mkaguzi wetu akaikaguwe meli popote ilipo duniani, baada ya kujiridhisha na ukaguzi huo, tunatoa usajili wa muda yaani *entering certificate*. Baada ya kukamilika masharti yetu yote kwa mujibu wa sheria zetu, meli hiyo hupatiwa usajili wa kudumu baada ya kipindi cha *entering certificate* kukamilika.

Aidha, Mhe. Makame Mshimba Mbarouk alitaka kujua mamlaka inajitayarisha kwa kiasi gani katika zana za kuokolea. Mamlaka hivi sasa haina zana yoyote ya kuokolea. Hata hivyo

imetayarisha orodha ya vifaa na kuipeleka katika Ofisi ya Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, hadi hvi sasa tunatarajia majibu yatakayotoka huko yatatupa mwanga wa namna gani tunaweza kupata fedha za kununulia vifaa hivyo.

Pia Mhe. Omar Ali Shehe alitaka kujua mwenye mamlaka nje ya mipaka ya bandari ni nani. Mwenye mamlaka nje ya mipaka ya bandari kwa chombo kinachoondoka kwa mujibu wa sheria ni mamlaka ya *ZMA*. Kuhusu *account* za shilingi tayari imefunguliwa tarehe 28/07/2012 kwa jina la mamlaka usafiri baharini.

Mhe. Spika, suala jengine lilikuwa ni suala linalohusu uwanja wa ndege na hoja ilikuwa ni uwekaji wa taa katika uwanja wa ndege wa Pemba. Mamlaka imezungumza na bodi na kuishauri serikali kuchukua fedha za maendeleo zilizotengwa katika miradi ya maendeleo katika kiwanja cha ndege ili kuzitumia Pemba kwa ajili ya uwekaji wa taa hizo. Jambo hilo linafanyiwa kazi na kama maelezo yalivyoeleza kwamba katika bajeti yetu, katika eneo la miradi ya maendeleo tutachukua fedha zile, ili kuimarisha hatua ya awali ya uwekaji wa taa katika uwanja wa ndege wa Pemba.

Pia Mhe. Abdalla Juma alitaka kujua jina kamili la uwanja wa ndege wa Pemba. Jina kamili la uwanja wa ndege wa Pemba unaitwa *Pemba Airport*. Mazingira ya uwanja wa ndege yanaendelea kuboreshwa kwa kufanyiwa usafi wa kila siku. Njia ya kurukia ndege ya uwanja wa ndege wa Pemba hivi sasa una uwezo wa kuhudumia ndege zenye uwezo wa kubeba abiria hadi abiria 70, yaani ATR 72 ambayo inakidhi haja ya matumizi kwa hivi sasa.

Kuhusu jengo la abiria mamlaka imeshafanya tathmini ya uvujaji na uchakavu wa majengo, pamoja na ukosefu wa huduma muhimu. Hivyo mamlaka inajipanga kushughulikia na kurekebisha mapungufu hayo.

Mhe. Saleh Nassor Juma alitaka kujua suala la *ZAT*. Nadhani maelezo ya Mhe. Mwanasheria Mkuu yamekamilisha. Mhe. Jaku Hashim Ayoub alitaka kujua maegesho ya magari. Sheria nambari 8 ya mwaka 2011 iliyoanzisha mamlaka ya viwanja vya ndege, inaipa uwezo mamlaka kukusanya mapato kupitia vyanzo vyake mbali mbali vya mapato. Miongoni mwa vyanzo hivyo ni pamoja na maegesho ya magari. Vyombo vyote vya moto vinavyoingia uwanjani hutakiwa kutozwa ada kwa maegesho hayo, isipokuwa vyombo vya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar au magari ya mabalozi. Viwango hivyo ni kama ifuatavyo.

Gari ndogo ni shilingi 500, gari kubwa shilingi 1,000, vyombo vidogo vidogo vya vespa na pikipiki shilingi 250. Kwa wafanyakazi wanapewa punguzo maalum akiingia mara moja hatozwi zaidi ya mara hiyo. Aidha, kwa wale watakaovunja sheria kwa kuweka chombo katika maeneo yasiyoruhusiwa watapigwa *fine* ya shilingi 15,000 na ikiwezekana hata magari yao kuyafunga. Mapato yote yanayokusanywa yanaingia katika mfuko wa mamlaka kwa mujibu wa sheria husika.

Vile vile Mhe. Hija Hassan Hija, alitaka kujua suala la jengo. Tayari ufafanuzi ameshautoa Mhe. Mwanasheria Mkuu. Suala la fidia, *apron na tax,* kamati iliyoundwa na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais tayari imeshafanyakazi na zoezi hili linaendelea vizuri, takriban ni zaidi ya shilingi

milioni 900 zimeendelea kulipwa na taarifa tulizokuwanazo, kati ya watu 22 bado watu 4 hawajenda katika mamlaka kuchukua malipo yao, karibu watu 18 tayari wameshafanyiwa malipo. Aidha, mamlaka imepokea ushauri wa kuufanyia kazi kwa kuboresha vikao vya watu kutafuta utaratibu.

Mhe. Asaa Othman Hamad, alitaka kujua mamlaka haikatazi matumizi ya *E ticket*. Mamlaka haikatazi, isipokuwa utaratibu wa watumiaji wa *E ticket* ndio wanaokosea. Mamlaka inachokifanya unapokwenda na simu kama umeuziwa *electronic ticket,* unakwenda kwa wakala wako aliyekuuzia *ticket* unamuonesha ile siku yako, yeye anachukua *reference number*, ana *print ticket*, unapokwenda kwa mtu wetu wa *security* unamuonesha ile *hard copy* ya ile tiketi ambayo umeprintiwa. Lakini unapokwenda na simu kwa mtu wetu wa *security*, hawezi kupata kumbukumbu zinazohitajika. Sote tunajua kwamba utaratibu wa kusafiri ni lazima uwe na vielelezo vinavyoonesha jina lako, unapotoka, ikiwezekana *passport number* na vielelezo vyengine. Sasa unapochukua simu ambapo unakwenda na ile *electronic ticket* kwa yule mkaguzi wa usalama, yeye hana chombo cha ku-*print* ili kuweza kugundua hizo taarifa muhimu zinazomruhusu msafiri kuweza kuendelea na safari yake.

Aidha suala la Chuo cha Anga ni suala ambalo linaratibiwa kwa pamoja na kile chuo cha mabaharia. Tayari kwa upande wa Chuo cha Mabaharia ambao ni *DANAOS* na *Filtex* wameonesha nia ya kutaka kushirikiana na serikali katika kukamilisha, hatua iliyopo ni kwamba tayari kama wizara tumeshaandaa warakawa kwenda serikalini ili kupata ushauri na maamuzi sahihi ya serikali katika uanzishwaji wa vyuo viwili hivyo.

Mhe. Mohamed Haji Khalid, alitaka kujua suala la uwekaji wa taa. Tayari kama tulivyoeleza.

Pia Mhe. Ismail Jussa Ladhu, alitaka kujua mapato ya mamlaka hayo katika kitabu cha bajeti. Mamlaka ni taasisi inayojitegemea katika kukusanya na kutumia mapato yake, hivyo hayamo katika kitabu cha bajeti, kwani bajeti yake hupitishwa na Bodi ya Wakurugenzi wa Mamlaka. Aidha, bajeti iliyopitishwa na Baraza ilikuwa ni ya Idara ya Anga wakati mamlaka iliidhinisha baada ya bajeti.

Mhe. Spika, sote tunakumbuka kwamba mwaka jana mwezi wa *August* ndipo tulipofanya mabadiliko ya Idara ya Anga kwenda katika mamlaka. Twabaan bajeti yetu tulipitisha kabla ya mwezi wa *August*, ilikuwa ni bajeti ya Idara ya Anga. Kwa hivyo, matumizi yale ya Idara ya Anga ndio yaliyohamishiwa katika Mamlaka. Sasa katika matumizi yao mamlaka wamejikuta kwamba wanahitaji ziada ya matumizi, kwa sababu kama tunavyofahamu wametoka katika idara wamekuwa Mamlaka, matumizi yake yatakuwa yameongezeka, kwa hivyo ongezeko lile ndio lililopelekea kuonekana kwamba matumizi yakawa makubwa kulikoni vile ambavyo yalikuwa yameashiriwa au yameruhusiwa na Baraza lako tukufu kupitia Idara ya Anga.

Bajeti ya shilingi bilioni 3, inatokana na vyanzo vyetu tulivyoruhusiwa na serikali kuu ambavyo havikidhi matumizi halisi ya mamlaka. Vyanzo vikuu vya mapato vinatokana na huduma za viwanja vya ndege vinachukuliwa na serikali kama vile *Airport, service charge, safety fee* na *VISA*. Suala la fidia kama tulivyoeleza kwamba katika uwanja wa ndege kuna fidia ya aina tatu. Kuna fidia ya ukuta, kuna fidia ya *terminal* na kuna fidia ya *tax na apron*. Fidia ya ukuta inalipwa pale ambapo mjenzi ukuta wake umefika, analipa kuondoa watu waliopo ili kupisha

ujenzi. Fidia ya *terminal* kuna watu watatu bado wanatudai na hao fedha zipo kinachosubiriwa ni wao wenyewe kwenda kuchukua fedha na katika upande wa fidia ya *apron na tax* ni kama tulivyoeleza kwamba kuna watu 4 kati ya 22 ambao wamesalia hawajenda kuchukua fedha zao.

Aidha, matumizi ya ukumbi wa watu mashuhuri. Mamlaka inafuata ushauri wa serikali wa kuona kuwa eneo hilo mtu anayekwenda kufuata huduma anapaswa kulipa shilingi 20,000 kama maelekezo ya serikali. Mamlaka ina utaratibu wake wa kukusanya mapato kama tulivyoeleza. Pia mamlaka imeweka utaratibu wa kutumia vyoo vya abiria na wafanyakazi na wasindikizaji na hata abiria wanaotuhumiwa kusafirisha madawa ya kulevya, hakuna mtu yeyote ambaye amezuiliwa kutumia huduma ya vyoo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ni kwamba utaratibu uliopo choo ambacho kimezuiwa watu kuingia kwa ajili ya kufanya haja, ni choo kile ambacho kiko katika eneo la *arrival,* na hatua hii imefanywa kwa msingi wa usalama kwa maana mtu hawezi kutoka nje ya uwanja akenda kuingia katika choo cha *arrival,* tuki-*assume* kwamba muda ule ambao yuko chooni, katika choo kile cha *arrival,* kuna na mgeni ambaye ameshuka ndege yuko katika choo kuna uwezekano wa watu hawa kubadilishana vitu au kuna uwezekano wa vyuma kwa wale abiria ambao wanaingia nchini, lakini pia *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, tukipiga makofi sana tutakuwa hatusikii majibu haya. Kwa hivyo, tunaomba utulivu.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Naomba nirudie Mhe. Spika. Choo kilichozuiwa watu kwenda kuingia ni choo ambacho kiko katika *arrive* na utaratibu madhumuni ya kufanya hivyo kukinga usalama. Kwa sababu mtu ameshuka kwenye ndege, ameingia chooni na kuna mtu mwengine anatoka nje ya uwanja ameingia chooni, yule mtu ambaye ameshuka kwenye ndege hajafika eneo la kukaguliwa, kuna uwezekano kama alikuwa na kitu akampa huyo mtu ambaye ameingia na kwa sababu yule mtu aliyeingia hatopita tena katika eneo la kukaguliwa. Kwa hivyo, tunapohimiza suala la usalama ni lazima tukubaliane na taratibu. Utaratibu huu umewekwa kwa lengo la kukuza usalama wa uwanja wetu.

Hivi majuzi Mhe. Spika, kuna mtu ambaye amekamatwa na dawa za kulevya alikuwa ameweka kwenye suruali yake, tuna-*assume* kama mtu yule angekuwa amekwenda chooni akakutana na mtu mwengine angempa hayo madawa, ile azma ya serikali ya kupiga vita madawa ya kulevya isingeweza kufanikiwa. Kwa hivyo, mimi naomba tu utaratibu huu tunaomba uendelee na eneo la watu wanaokwenda kusindikiza wafanyakazi, kuna eneo la choo ambalo limetengwa. Sasa hapa suala la kujiuliza ni kwamba kwa nini unalazimisha wewe ukajisaidie katika choo cha *arrive,* kwa nini usitumie choo ambacho kimetengwa. Maana lazima kuna swali la kujiuliza Mhe. Spika. Choo kipo na kinakidhi kwa nini ulazimishe lazima ukajisaidie katika choo cha *arrive,* ina maana wewe una *intension* nyengine zaidi ya yale matumizi ya kutaka kujisaidia.

Mhe. Spika, Mhe. Omar Ali Shehe alitaka kujua uwanja wa ndege wa Pemba kuhusu uwekaji wa taa. Kama tulivyoeleza kuhusu mipango yetu katika uwekaji wa taa. Pia suala la mgogoro kati ya *Gallary* na Kampuni ya *ZAT*.

Mhe. Spika, Kampuni ya *Galari* ni *agent* wa Kampuni moja ya South Africa ambayo inafanya biashara ya kusafirisha watu. Kampuni hii ya Galari kikawaida ndege ya *Oman Air* inakuja siku ya Ijumaa, inapofika ndege ya *Oman Air* wanakuwepo ndugu zetu wa Pakistani, wengi wao ni waalifu na ni watu ambao wanasafiri kinyume na taratibu. Sasa kilichopo ni kwamba kuna wasafiri wa kutoka Pakistani walikuwa watu watatu na walikuwa wamefika Zanzibar siku ya Ijumaa, Jumamosi wakamfuata Afisa wa Kampuni ya *Galari and Tour* kutaka wasafiri katika ile ndege ya *South Africa* kwa ajili ya kwenda *South Africa* na wakasema hawana *passport* na wao wakaghushi *passport* ya Tanzania. Kwa hivyo, alichokifanya *agent* huyu aliwasiliana na watu wa uhamiaji kwamba kuna watu ambao wanataka kusafiri, lakini hawana hati za kusafiria.

Ushauri aliopewa na watu wa uhamiaji kwamba tunaomba jambo hili tusaidiane sisi, wewe na watu wa *Airport*, uhakikishe kwamba watu hawa wanaingia katika eneo la *Airport*, ili wakishafika katika eneo hilo ndio tukawakamate. Ushauri huo umetoka kwa maandishi kwa Mkurugenzi muhusika wa Kitengo cha Uhamiaji katika eneo la *Airport* na tukakubaliana, akawaruhusu watu hawa wakaingia eneo la *Airport* na wakakamatwa na hatua stahiki za kisheria kwa mujibu wa sheria za uhamiaji zikafuatwa. Miongoni mwa watu hao mmoja alikuwa tayari ameshaingia katika ndege akenda akatolewa na hawa waliokamatwa walikuwa katika waiting lounge.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, tulichomuomba *ZAT* kwamba aendelee kufanyakazi na mtu huyo, kama kosa lilikuwa hili basi ilikuwa ni amri inayotokana na vyombo vyetu vya ulinzi na usalama na sisi kama mamlaka tulishauriana na tukakubaliana, msingi huo wa kutaka kuwakamata watu wahalifu. Kwa hivyo, kama *ZAT* tatizo lilikuwa ni hili la Galari, kwa hili tunamuomba aendelee kufanya nao kazi, kama kulikuwa kuna tatizo jengine hatujalipata, hilo hatuna namna ya kulisema.

Mhe. Spika, pia Mhe. Wanu alitaka kujua suala la uchimbaji. Ni kweli kwamba kuna maeneo ambayo yanachimbwa mchanga, kwenye maeneo ambayo yamezunguka uwanja wa ndege. Tunahakikisha kwamba tutaweka doria na tutawaomba watu wetu wahakikishe kwamba wanayalinda maeneo yale ili kunusuru mazingira, lakini pia kunusuru uwenja wetu.

Mhe. Rufai Said Rufai alitaka kujua suala la Hijja kwa maeneo ya uwanja wa ndege. Suala hili kama tulivyoeleza. Aidha, Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali, alilalamika kwamba kampuni ya *Ethiopia Airline* haijapewa ofisi. Tayari Kampuni ya *Ethiopia Airline* imeshapatiwa ofisi, ipo nje pale ukiingia tu katika eneo lile la *buredechange* mkabala nao kwenye mkahawa wa Ajamin. Tayari kuna eneo ambalo limeshajengwa na tumeshawapatia, kwa hivyo kilichobakia ni wao wenyewe kwenda kujenga ofisi yao. Kuhusu utaratibu unaotumiwa na *ZAA* ni kukodisha *par meter square*.

Aidha, Mhe. Hamza Hassan Juma alitaka kujua fidia ya Ali Mwinchande. Mhe. Spika, bwana Ali Mwinchande tayari tumeshampa fidia ya shilingi milioni 34 tayari yeye mwenyewe ameshavunja nyumba, ameshaondoka na eneo husika tumeshaliziba na ukuta tumeshapita. Pia alitaka kujua suala la *Airport Pemba* chini ya *ADB* kama maelezo tuliyoyatoa.

Mhe. Asha Abdi Haji, alitaka kuanzishwe Shirika la Ndege la Zanzibar. Mpango huu kwa sasa hivi kwenye wizara yetu haupo. Lakini kama ni chachu tunaipeleka serikalini ili serikali ifanye maamuzi kuhusiana na jambo hilo.

Mhe. Mohamed Mbwana alitaka uwanja wa ndege ufanyiwe matengenezo. Suala hili nalo nimeshalijibu.

Mhe. Spika, suala jengine lililoulizwa lilikuwa ni suala la *harbor port*, ambalo tayari nimeshalitolea maelezo ya kina, kwamba azma ya serikali kikwazo kilichopo sasa hivi ni fedha na imani yetu tukipata fedha, basi mpango wa *harbor port* utakamilika.

Suala jengine lililoulizwa lilikuwa ni suala la makampuni na mashirika ya Muungano yanayofanyakazi Zanzibar. Makampuni na mashirika ya Muungano yanayofanyakazi Zanzibar ni pamoja na *TICRA, TCA, TMA, TTC, TTCL* na kadhalika. *TCA* na *TMA* sehemu kubwa wanayochukua ni huduma na hawafanyi biashara. Kwa sababu moja inasaidia usafiri wa anga na moja inasaidia kupata huduma za hali ya hewa.

Lakini suala la *TICRA* ni chombo ambacho kina *regulate* na huduma za mawasiliano, kwa kweli wanatusaidia na taarifa tulizonazo ni kwamba katika mwezi wa Septemba watatusaidia kupata gari lile ambalo litakuwa linatumika kwa ajili ya kufanya *detection* ya maeneo na umahiri wa mawasiliano kwa wananchi wetu. Pia wamekuwa wakisaida miradi mbali mbali ya maendeleo ya kijamii. Kwa mfano Jimbo la Chumbuni walisaidiwa kuchimba kisima na hawa *TICRA*.

Suala jengine lilikuwa ni mradi wa uwekaji wa mkonga Zanzibar. Mradi huu unasimamiwa na kuendeshwa chini ya Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, chini ya Idara ya Vitambulisho ndio wanaosimamia na kuratibu mradi huu.

Aidha, Mhe. Shawana Bukhet Hassan na Mhe. Mahmoud Muhamed Mussa, walitaka kujua suala la nambari yetu ya zamani ya kodi ya Zanzibar. Ni kweli kwamba Zanzibar tulikuwa tuna nambari yetu ambayo ni +259 ambayo baada ya kuungana, nambari ile ikaondoshwa na kupewa nambari ya Jamhuri ya Muungano ambayo ni +255. Mwaka 2003 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilituma ujumbe maalum kwenda kufuatilia suala hilo na wakaambiwa kwamba nambari hiyo imeshafutwa katika utaratibu wa *ICTU*.

Mhe. Spika, suala jengine lilikuwa ni usajili wa simu kwa mujibu wa utaratibu wa sheria husika ya eboka, suala la matumizi ya simu kusajili ni lazima na mtu yeyote ambaye atatumia simu bila ya kusajili akikamatwa anapaswa kutozwa faini ya shilingi 200,000 au kifungo cha miaka 2. Kampuni ambayo itakuwa imempa huduma ya kutoa simu bila ya kusajili, basi itatozwa faini ya shilingi milioni 15,000,000. Changamoto iliopo ni kwamba makampuni ya simu wamefungua kesi mahakamani, kwa sababu wanachokitaka ni kwamba sheria hii ya eboka isiwe *composer* lakini iwe *option*, kwa maana kwamba suala la kusajili liwe ni ridhaa ya mtu isiwe lazima. Kwa hivyo, usimamizi wa *TICRA*, wanachosubiri ni maamuzi ya mahakama, maamuzi ya mahakama yakiamuru kwamba suala hili liendelee kuwa ni lazima, basi utekelezaji wa sheria utafuatwa.

Aidha, Mhe. Mahmoud Muhamede Mussa, alitaka kujua ni chombo gani kinachosimamia kuratibu huduma za mawasiliano Zanzibar. Chombo kinachosimamia ni *director* wa

mawaasiliano kwa hapa Zanzibar, ikiwa inaratibu kwa kushirikiana na vyombo husika kama *TICRA* na vyombo vyengine. Lakini pia chombo hiki kimekuwa kikishughulikia masuala ya Teknohama na masuala mengine ya *electronic* katika mfumo wa uendeshaji wa serikali.

Vile vile alitaka kujua suala la Kampuni ya Zantel. Mhe. Spika, sio kweli kwamba Kampuni ya Zantel imetakiwa kulipa kodi zote Tanzania Bara. Kodi zote zinalipwa Zanzibar kwa kupitia *TRA* na *ZRB* na kwa miaka sita mfululizo Zantel imekuwa mshindi nambari moja kutoka katika sekta binafsi katika kundi la walipa kodi wakubwa, yaani *large posture category*. Matatizo madogo madogo waliyokuwa wakiyapata wadau wetu katika kodi, yameshughulikiwa ipasavyo baina ya Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ya SMZ na Wizara ya Fedha ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Pia suala la fidia kwa minara. Mhe. Spika, minara kuna ya aina mbili, kuna wale ambao wameikodisha Kampuni ya Zantel, lakini pia kuna wale ambao watakuwa wamewauzia Kampuni ya Zantel. Wale ambao watakuwa wamewakodisha wataendelea ku-*bargain* kwa mujibu wa soko lilivyo na wale ambao watakuwa wamewauzia hawatokuwa tena na mamlaka ya kwenda kufanya mabadiliko, kwa sababu masuala ya umiliki tayari watakuwa wameshahaulisha.

Baada ya kusema hayo machache Mhe. Spika, na mimi naomba tena nirejee kwamba mimi binafsi pamoja na wananchi wenzangu wa Jimbo la Chwaka tunaunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja, ahsante Mhe. Spika. *(Makofi).*

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Nakushukuru sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kufanya majumuisho. Kwanza namshukuru Allah kwa kutujaalia uhai, uzima na taufiki ya kufika katika Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, kabla sijaanza kufanya majumuisho na kuwataja wajumbe ambao waliotuchangia, naomba nizungumze mambo mawili kidogo tu. Kwa sababu ya upya wangu sana katika wizara hii, naomba niwahakikishie wawakilishi wote ambao wamepata nafasi ya kuchangia moja kwa moja au kwa maandishi kwamba michango yao nitaichukua kwamba ndio changamoto ya mwanzo ya kuanza katika katika ofisi tukijaaliwa.

Lakini suala la pili Mhe. Spika, ni kwamba wakati tunaendelea na kazi, naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe kwamba nitakuwa na mambo matano ambayo nitayapa kipaumbele katika kazi zangu za wizara.

Jambo la kwanza ni usalama wa wananchi kwa usafiri wa baharini, anga na nchi kavu. Jambo la pili ni kuhakikisha matumizi sahihi ya fedha za serikali na kurekebisha mianya yote ya matumizi mabaya.
Jambo la tatu ni kuongeza ufanisi katika utendaji kazi.
Jambo la nne ni kutoa fursa kwa mamlaka zetu na mashirika kuweza kutekeleza majukumu yao kwa upeo na ufanisi na kuweza kujiendesha.
Jambo la mwisho ni kuleta mabadiliko katika matumizi ya mitandao yaani kutumia IT katika njia ya kupata ufanisi na kuelekea katika *E government.*

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, naomba sasa kwa ruhusa yako nitowe baadhi ya majumuisho ambayo Mhe. Naibu Waziri ameniachia. Baada ya kutoa majumuisho fulani Mhe. Naibu Waziri, yeye alipitia katika idara ya ujenzi na utunzaji barabara, idara ya mipango na sera na utafiti, mamlaka ya viwanja vya ndege na mamlaka ya usafiri baharini.

Mhe. Spika, kama nilivyosema kutokana na upya wangu ilibidi Mhe. Naibu Waziri na namshukuru sana aweze kuniunga mkono katika mambo hayo.

Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe waliopata nafasi ya kuchangia katika bajeti yetu ni wajumbe 23 wa moja kwa moja na wajumbe 8 wamechangia kwa maandishi.

1. Mhe. Spika, naomba nitambuwe mchango wa Mhe. Hassan Hamad Omar, akiwakilisha Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi. Wengine ni:
2. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
3. Mhe. Saleh Nassor Juma
4. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
5. Mhe. Suleiman Hemed Khamis
6. Mhe. Hija Hassan Hija
7. Mhe. Ali Salum Haji
8. Mhe. Asaa Othman Hamad
9. Mhe. Mohamed Said Mohamed
10. Mhe. Mohamed Haji Khalid

11. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
12. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
13. Mhe. Viwe Khamis Abdalla
14. Mhe. Omar Ali Shehe
15. Mhe. Nassor Salim Ali
16. Mhe. Wanu Hafidh Ameir
17. Mhe. Rufai Said Rufai
18. Mhe. Shawana Bukheit Hassan
19. Mhe. Mahmoud Muhamed Mussa
20. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali
21. Mhe. Machano Othman Said- Waziri asiyekuwa na Wizara Maalum
22. Mhe. Mwanasheria Mkuu
23. Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano

Mhe. Spika, wale wajumbe waliochangia kwa maandishi ni;

24. Mhe. Kazija Khamis Kona
25. Mhe. Mohamed Mbwana Hamad
26. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi
27. Mhe. Hamza Hassan Juma
28. Mhe. Asha Abdu Haji
29. Mhe. Abdi Mosi Kombo
30. Mhe. Mlinde Mbarouk Juma
31. Mhe. Mbarouk Wadi Mussa

Mhe. Spika, kwa niaba ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano tunawashukuru wajumbe wote hawa. Napenda nitowe shukrani za pekee kwa Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa ufafanuzi wake aliotoa kutokana na mambo mawili ambayo ni nyeti na yote yako katika uwanja wa ndege wetu. Kwa hivyo, haya ni mambo muhimu na ametutolea ufafanuzi.

Mhe. Spika, kuhusu michango ya kamati naomba niwahakikishie kwamba michango yote ya kamati tumeichukua na tunaifanyia kazi, vikiwemo vichwa vifuatavyo. Kwanza hoja ya marekebisho ya viwango vya mishahara kwa wafanyakazi wa ngazi ya chini, kupatiwa wafanyakazi wa idara ya utumishi hadidu rejea, mikataba ya ujenzi wa barabara na suala la ujenzi wa mitaro, uharibifu wa mazingira kwa uchimbaji wa kifusi na makampuni ya ujenzi wa barabara, mashirikiano na waheshimiwa wawakilishi katika ujenzi wa barabara, uwekaji wa barabara pembezoni mwa barabara, mashirikiano baina ya idara ya usafiri na leseni na jeshi la polisi, utoaji wa leseni za vyombo vya moto, utaratibu wa ukaguzi wa magari barabarani, uharibifu wa mazingira katika eneo la uwanja wa ndege ikiwemo uchimbaji wa mchanga, ujenzi wa bandari ya Mpigaduri, upatikanaji wa meli mpya kuzingatia utoaji huduma zaidi kwa wananchi na uwekaji wa nyaya za mkonga wa taifa pembezoni mwa barabara.

Maudhui yote haya yalizungumzwa na kamati na tunawahakikishia kwamba wizara itafanya kila bidii ili kuhakikisha kwamba haya yanafuatiliwa kwa kina.

Mhe. Spika, baada ya kamati tunakuja katika michango ambayo ilitolewa kwa kupitia wawakilishi kuhusiana na Shirika la Meli na Uwakala. Mhe. Abdalla Juma Abdalla wa Jimbo la Chonga aligaka kujua kigezo kilichotumika mpaka kufikia mapato ya bilioni 4.36, wakati kipindi cha Julai / Machi Shirika lilikusanya bilioni 2.56.

Mhe. Spika, nyongeza ya mapato yanatokana na mambo yafuatayo. Kuongezeka kwa meli za nje kama nilivyotaja huko nyuma, ili ni Shirika la Meli na Uwakala. Kwa hivyo, hiki kitengo cha uwakala ndio kinashughulika na meli za nje. Kwa hivyo anasema, kuongezeka kwa meli za nje bandarini pamoja na kuongezeka kwa mizigo na makontena kurudi kwa MV Maendeleo kwenye biashara ambayo ilisita kwa mwaka wa fedha uliopita, pia kuongezeka kwa ada ya mizigo midogo midogo inayosafirishwa na meli zetu na tozo za utozaji wa mizigo bandarini kwa meli za kigeni katika mwaka wa fedha 2012/2013, haya ndio mambo yaliyochangia kuongeza mapato.

Mhe. Viwe Khamis yeye alitaka kujua mapato ya MV Maendeleo kwa mwaka 2011/2012, vile vile meli hiyo ilikwenda chelezoni mara ngapi. Jibu, Meli ya MV Maendeleo kwa mwaka 2010/2011 ilikusanya jumla ya shilingi bilioni 1,391,031,815 katika mwaka wa fedha 2011/2012. Meli ya MV Maendeleo ilifanyakazi kwa miezi mitatu tu Julai Septemba na kuweza kukusanya jumla ya shilingi milioni 352,460,000.

Mhe. Spika, MV Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2010/2011 ilikwenda *draidog* mara moja tu, kwa shilingi milioni 191,402,215. vile vile ilikwenda tena *draidog* mwaka 2011/2012 na iligharimu shilingi milioni 283,784,932.

Mhe. Ali Salim na Mhe. Mohamed Said walishauri meli ya MV Maendeleo iuzwe, ushauri huu ulitolewa vile vile na Mhe. Mohamed Mbwana Hamad na badala yake inunuliwe meli mpya itakayokidhi usafiri wa visiwa vyetu na mwambao wa Afrika ya Mashariki. Jibu, meli ya MV Maendeleo hivi sasa tayari imeshatengenezwa na kukaguliwa, meli hii tayari imefuata vigezo vyote vya ukaguzi baina ya *ZMA* na *SUMATRA*, hivi sasa meli hiyo iko tayari kuanza safari. Mhe. Spika, kuhusu suala la kuuzwa kwa meli hii, taratibu zitafanywa mara itakapopatikana meli mbadala.

Mhe. Shawana Bukhet Hassan alitaka kujua Shirika la Meli limejitayarisha vipi huko Dar es Salaam hasa baada ya kuja kwa meli mpya. Jibu, Shirika la Meli kwa muda mrefu sasa linazo ofisi na nyumba za kukaa wafanyakazi pamoja na usafiri kwa huko Dar es Salaam. Shirika limejipanga vizuri kupokea meli mpya katika ofisi zake zote ziliopo Zanzibar, Dar es Salaam na Pemba.

Mwisho Mhe. Spika, katika Shirika la Meli Mhe. Mohammed Said Mohammed na Mhe. Hamza Hassan Juma, walitaka kujua uwakala wa meli za kigeni unaofanywa na Shirika la Meli na Uwakala ubinafsishwe, ili kuruhusu watu binafsi kufanyakazi hiyo.

Jibu kwa hivi sasa serikali haina mpango wa kubinafsisha Kitengo cha Uwakala kutoka Shirika la Meli. Hivyo, serikali itafikiria jambo hili hapo itakapokuwa na bandari kubwa zaidi, ambayo itaweza kufunga meli zaidi ya moja na kuweza kutengenisha meli za abiria, meli za ndani na zile za kigeni. *(Makofi)*

Mhe. Spika, maswali yaliyoulizwa kuhusiana na Idara ya Utumishi. kwa hivyo, haya kama nilivyojibu yaliulizwa na kamati, hivyo suala hili tayari limeshajibiwa na kwamba kamati ilitaka kujua mishahara ya watumishi.

Vile vile kulikuwa na suala jengine la ustaafishaji wa wafanyakazi. Wizara katika kipindi cha mwezi wa Disemba, 2011 na hili liliulizwa na Mhe. Hija Hassan Hija, yaani 2011 na Februari, 2012 ilistaafisha wafanyakazi 16 kwa upande wa Unguja na wafanyakazi 37 kwa upande wa Pemba, ambapo jumla ya wafanyakazi 53 waliotengenezewa mafao yao, ilibainika wafanyakazi 12 walitengenezewa mafao yao kimakosa.

Mhe. Spika, watendaji wakuu wa wizara waligundua kosa hilo na kulifuatilia kwa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kwa ajili ya kutaka kujua ukweli wa suala hilo. Wizara ilipowasiliana na watendaji wa Ofisi ya *CAG*, tuligundua kuwa kosa hilo lilifanyika, kubaini wafanyakazi watatu kati ya hao 12 waliokuwa wameshapokea malipo hayo na hatua za haraka za kuwataka warudishe fedha hizo zilichukuliwa.

Watendaji wa Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali waliandika barua kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kumjuilisha juu ya suala hilo, ambaye naye alichukua hatua za kuiandikia wizara yetu. Kwa hivyo, wizara ilichukua hatua ya kuwasimamisha wafanyakazi wanne, mmoja wa Makao Makuu na wengine watatu wa Ofisi Kuu Pemba.

Kamati Maalum ya Kuchunguza suala hilo iliundwa na tume tayari imeshawalisha taarifa yake wizarani, ambapo taarifa hiyo imeshajadiliwa na Kamati ya Uongozi wa Wizara na Katibu Mkuu wa Wizara yumo katika hatua za mwisho kumuandikia Katibu Tume ya Utumishi ya Serikali kumjuilisha suala hilo, kwa ajili ya kuchukua hatua zinazofaa kwa mujibu ilivyoelekezwa na Sheria ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2011.

Mhe. Spika, kuhusu mabadiliko au bajeti ilivyoonesha katika vifungu, wizara imetoa chapisho jengine. Kwa hivyo, tunawaomba Waheshimiwa Wajumbe wapitie lile chapisho jipya la wizara ndilo lenye kukubalika na yale yaliomo katika daftari kama ilivyotajwa na wizara nyengine ni kwamba kulikuwa na makosa mengi. Hivyo, wizara tayari imeshagawa kwa Waheshimiwa Wajumbe toleo jengine la vifungu.

Mhe. Spika, Shirika la Bandari lilipata maswali yafuatayo. Kwanza Mhe. Abdalla Juma Abdalla alitaka kujua vigezo gani shirika kwa mwaka linakadiria kukusanya shilingi 16.5 bilioni. Viegezo vinavyotumika kwanza hali halisi ya mwaka wa fedha uliopita. Pili inaangalia mtazamo wa kibiashara, ambapo takwimu zinaonesha kuwa kunaongezeko kubwa la ukubwa wa meli pamoja na idadi kubwa ya makonteni, ambayo ndio vigezo vikuu vinavyotumika katika shirika.

Mhe. Saleh Nassor Juma alitaka kujua kutowaka kwa taa ya Mnara wa Matumbini. Mhe. Spika, jibu ni kweli Mnara wa Matumbuni hauwaki, hata hivyo shirika limeshafungiana mkataba na Kampuni ya Dubai ya *Save Sea Services* kwa kufunga taa mpya za *solar* katika minara yote mikubwa ya Unguja na Pemba ukiwemo wa Matumbini, kazi hii inatarajiwa kuanza baada ya mwezi mmoja unaokuja.

Aidha Tani Boya ya Bandari ya Mkoani ambalo lilikuwa na matatizo ya kiufundi limesharekebishwa tokea tarehe 31/05/2012 na linafanyakazi kama kawaida.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub alitaka kujua matatizo ya *Signal Tower*, Usafiri wa *Harbour Master* na Ofisi za Bandari ndani. Jibu kuhusu Mnara wa Beit-el-Ajab *Signal Tower* matatizo yaliopo, tayari yameshachukuliwa hatua kwa kununuliwa viti vipya na pia kifaa kipya cha mawasiliano kinafanyakazi kama ilivyokusudiwa.

Shirika linakiri kweli kuwa kuna matatizo ya usafiri, lakini *Harbour Master* anapatiwa usafiri kila anapohitajika na shirika hilo liko katika hatua za mwisho za kununua gari zake kwa maafisa wake.

Ni kweli shirika linakabiliwa na changamoto za afisi, ambapo wanatumia Ofisi za *COGIFER*. Hata hivyo, linakamilisha taratibu za kumpata mkandarasi kwa ajili ya kufanya matengenezo makubwa jengo ambalo lilikusudiwa kutumika kama *Duty Free*. Ofisi zote za bandarini zinatumia jengo hilo na kutoa nafasi kwa majengo ya *COGIFER* kubomolewa, hivyo kuongeza eneo la kuwekea makontena bandarini.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa, Mhe. Mohammed Said Mohammed, Mhe. Ismail Jussa Ladhu na Mhe. Hamza Hassan Juma walizungumzia kuhusu *crane* zilizonunuliwa na Shirika la Meli.

Jibu *crane* mpya *Grove* zilizonunuliwa na wizara kupitia Shirika la Bandari linawathibitishia Waheshimiwa Wajumbe kwamba shirika limenunua *crane* mbili na moja ina uwezo wa kunyanyua tani 1 mpaka 75 na ya pili inanyanyua tani 1 mpaka 18. Hivyo, uzito wa *crane* hizo unaweza kunyanyua na unategemea urefu wa mkonga wake pamoja *radius* inayokunjuka. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ni kweli kwamba *crane* hizo kadri zinapokunyua mkonga wake na kuongeza *radius* uliopo mzigo uwezo wake hupungua. Hata hivyo, shirika limewasiliana na watengenezaji kuhusu tatizo hilo na wameahidi kutoa mafunzo zaidi kwa wafanyakazi. *(Makofi)*

Mhe. Hija Hassan Hija, Mhe. Hamza Hassan Juma na Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa hoja ya maslahi ya wafanyakazi bandarini, walizungumza kuhusu maslahi ya wafanyakazi, ambapo inadaiwa kwamba wafanyakazi wana maslahi duni na wakubwa wamejipangia mishahara kwa kisingizio cha nyadhifa zao.

Mhe. Spika, marekebisho ya mishahara yaliyofanyika yamezingatia vigezo vya elimu, wadhifa na uzoefu, pamoja na marekebisho hayo uongozi wa shirika unaendelea na hatua ya kufanya mapitio ya maslahi ya wafanyakazi hasa wa ngazi ya chini.

Aidha maslahi kadhaa ambayo Mhe. Waziri aliyepita aliahidi yamefanyiwa kazi kama vile bonasi kwa wafanyakazi imeshalipwa posho la Siku Kuu limerekebishwa na posho la Ubani limerekebishwa kufuatia kwa Kanuni za Shirika.

Mhe. Assaa Othman Hamad hoja ujenzi wa bandari mpya ya Mpigaduri na Mkunguu, utanuzi wa Bandari ya Wete na Wesha. Jibu Mhe. Spika, kuhusu ujenzi wa bandari mpya ya Mpigaduri na kutaka kujua serikali imefikia wapi juu ya mradi huo. Suala hili linaendelea kuratibiwa na wizara yangu, ambapo tatizo kubwa la upatikanaji wa fedha nyingi zinazohitajika kwa mradi huo.

Kuhusu Bandari ya Mkunguu, hivi serikali inashughulikia ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri na baada ya kumaliza kwake itafikiria Bandari ya Mkunguu. Aidha suala la urefushaji wa Bandari ya Wete pamoja na Bandari ya Wesha hilo tunalifahamu na wizara italishughulikia suala la kudidimia kwa Bandari ya Wete mapema iwezekanavyo, ili iweze kurudi katika hali yake. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kuhusu vyombo vya kuingiza meli bandarini *Tag Boat* na *Pilot Boat*, wizara inakiri kuwa vyombo hivyo vimeanza kuchakaa na uwezo wake ni mdogo kulingana na ukubwa wa meli zinazofika bandarini hivi sasa, masuala haya ni miongoni mwa changamoto ambazo zinafanyiwakazi na wizara.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu gharama za matengenezo za Mv. Jitihada na mashine ya kuunganisha vyuma. Meli ya Mv. Jitihada imegharimu jumla ya shilingi bilioni 2.6 hadi kukamilika matengenezo yake, mashine iliyonunuliwa na shirika hivi karibuni kwa ajili ya kuunganisha chuma ni aina ya *Duall Purpose Machine*.

Mashine hiyo inao uwezo wa kuunganisha chuma cha kawaida, pia mashine hiyo inayo uwezo wa kuunganisha chuma cha *Aluminium* baada ya kufungwa kifaa maalum. Mashine hiyo bado iko ghalani na bado haijaanza kutumika kikamilifu kutokana na kuwa mashine hiyo ni ya kisasa inayotumia *Digital* na wafanyakazi wetu wanaendelea kujifunza. *(Makofi)*

Mhe. Spika, shirika linafuata kikamilifu taratibu za Manunuzi kulingana na Sheria ya Serikali Nam.9 ya mwaka 2005.

Mhe. Mohmmed Haji Khalid gharama zilizotumika kwa matengenezo ya Gati ya Mkoani. Mhe. Spika, gharama zilizotumika kwa matengenezo ya Gati ya Mkoani ni shilingi milioni 195,000,000/=. Katika matengenezo hayo zege juu ya Gati ilikatwa na kuwekewa zege ambayo ilinyanyuka na kuweka mteremko wa maji.

Mhe. Omar Ali Shehe malipo ya kodi kwa Shirika la Bandari na Wazamiaji wa Shirika. Jibu Shirika la Bandari kwa mwaka wa fedha 2012 halijalipa kodi, hatua hii imetokana na kumbukumbu za madeni baina ya serikali kwa shirika yanayotokana na kodi na madai ya shirika kwa serikali yanayotokana na mikopo ya fedha taslimu na huduma mbali mbali zilizotolewa na shirika kwa serikali pamoja na taasisi zake na zile ambazo serikali ilikuwa inamiliki. Kwa hivyo, mazungumzo bado yanaendelea katika kuyapatia ufumbuzi masuala haya ya serikali.

Vile vile imeundwa tume maalum kwa ajili ya kuangalia uendeshaji mzima wa shirika yakiwemo masuala ya fedha, utawala na utumishi pamoja na uendeshaji, ambapo kukamilika kwa kazi ya tume hiyo kutatoa ufumbuzi wa masuala hayo.

Mhe. Spika, shirika linao wazamiaji wake watatu kwa kazi za shirika, inapotokea haja ya kuwatumia wazamiaji binafsi shirika linawalipa gharama ya kazi yao. *(Makofi)*

Mhe. Wanu Hafidh Ameir alitaka kujua jengo la Abiria la Bandari ya Malindi litajengwa lini. Wizara inaendelea na utaratibu wa mradi kwa kushirikiana na wawekezaji binafsi.

Mhe. Shawana Bukheit Hassan kujifukia kwa Gati ya Malindi. Shirika limekamilisha taratibu za kumpata mshauri wa kufanya uchunguzi wa kina cha maji na tunategemea kusaini mkataba katika kipindi cha wiki mbili zijazo.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa aliuliza matatizo ya meli ya Mv. Jitihada. Kwa kweli meli hiyo sio mbovu isipokuwa imepata hitilafu za kiufundi katika *pump* ndogo na hivi sasa linashughulikiwa tatizo hilo. Kuhusu kuikodisha meli hiyo kwa mtu binafsi shirika kwa hivi sasa haina mpango huo. Wizara inakiri kuwa kulitokea matatizo baina ya Vyama vya Ushirika vilivyopo Bandarini, shirika kwa kushirikiana na Vyama vya Ushirika inashughulikia tatizo hilo.

Mhe. Spika, kabla sijatoa hoja naomba niwashukuru tena Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza hili Tukufu, kwa kutusikiliza na kutufuatilia kwa makini na yale majina matukufu yale naomba sana wanipe muda, maana yake hapa kuna majina ya Maswahaba hapa.

Kwanza naanza na jina la Mtume Ismail, ujue kuwa jina lako alianza Mtume, halafu kuna majina ya Maswahaba Saidina Omar na Hamza. Vile vile kuna mmoja analo jina zuri sana kwa sababu watu wanakwenda sana kule kujikoshwa Bwana Hija. Kwa hivyo, nawaomba kwa sababu mimi ni mpya sana na nimeahidi kufanyakazi, basi tupeni muda ili tuweze kufanyakazi hiyo na nawashukuru sana. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nichukue nafasi kumshukuru Mhe. Waziri kwa majumuisho na mpaka mtu unapoona anatumia majina ya Viongozi Wakuu basi tena huyo, yaani anaomba Baraka za viongozi hao zisaidie pamoja na nguvu ya Mwenyezi Mungu isaidie kwa ajili ya kumaliza jambo hili kwa vizuri. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Kicheko/Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika , kwa kuwa Baraza limejadili na kukubali Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano. Sasa naomba Baraza

lako Tukufu likae kama Kamati ya Matumizi, ili kuvipitisha vifungu vya matumizi ya wizara yangu. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, naafiki.

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU 26 – WIZARA YA MIUNDOMBINU NA MAWASILIANO

Kifungu 0301 –	Afisi Kuu Pemba	42,500,000/=
Kifungu 0701 –		

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nimeona nisimame hapa kwa sababu maalum naamini utanielewa Mhe. Mwenyekiti.

Katika mchango wangu nilizungumzia suala la mamlaka ambazo ziko chini ya wizara hii na ambazo mapato yake hayaonekani, yamo katika hotuba ya Mhe. Waziri lakini katika hichi kitabu hayamo.

Kwa mfano, hapa utakuta kuna Ofisi Kuu Pemba tumeikwepa Idara ya Mipango Sera na Utafiti ina 00 na ndio maana nimepiga hapa Mhe. Mwenyekiti na tumeingia kwenye Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara.

Mimi nimesikiliza kwa makini sana majibu ya Mhe. Naibu Waziri pamoja na Mhe. Waziri. Mhe. Spika, niseme wazi majibu yao sio juu ya hoja hii tu, isipokuwa juu ya hoja zote hayaridhishi Mhe. Mwenyekiti. Hii inathibitisha Mhe. Mwenyekiti uoza uliomo katika wizara hii. *(Makofi)*

Nenda katika hoja Mhe. Mwenyekiti, nilisema kwamba mapato ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, mapato ya Mamlaka ya Usafiri Baharini, mapato ya Shirika la Bandari hatuyaoni katika kitabu hichi. Hoja iliyojibiwa ni kwamba haya ni mashirika yanayojitegemea, lakini haya si mashirika ya kampuni ya binafsi na wala si *ZAT*, isipokuwa haya ni Mashirika ya Serikali na mapato ni ya serikali. *(Makofi)*

Sasa tumezoea na ndio maana mara nyingi tunapiga kelele kwamba hakuna *consistence* katika serikali kuhusu masuala mazima ya vitabu vya bajeti, kwa sababu mengi pia ni mashirika au ni taasisi zinazojitegemea, lakini ukifungua humu ndani unazikuta zimeombewa ruzuku hata kama ndicho kile kile kinachokusanywa lakini kinaombewa katika mapato na halafu kinatajwa katika matumizi, humu hukuti Mhe. Mwenyekiti.

Jana nilitoa mfano wakati nilipokuwa nikichangia katika kitabu hichi juu ya Mamlaka kwa mfano ya Uwanja ya Ndege na matumizi yake. Kwa hivyo, nasema hoja ya kwamba haya ni mashirika yanayojitegemea, hivyo mapato yake ambapo mimi naamini ni mapato ya wananchi wa Zanzibar kama ni walipa kodi wa nchi hii yalipaswa yaonekane hapa katika mapato halafu yaje yaingie katika fungu la wizara kama ruzuku, ili tuwapelekee wale hata kama ndiyo yale wanayokusanya, lakini utaratibu huu umekiukwa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nasema kwamba tufupishe hadith kwa sababu hatutaki kuchukua muda wako na leo ni siku ya Ijumaa. Mhe. Mwenyekiti, nasema na jana nilisema, lakini nalisema hapa kwa sababu litahusu kote na mimi naomba hasa Waheshimiwa Wajumbe wenzangu kwamba bajeti ya wizara hii tuipumzishe mpaka watendaji wote watakapokwenda kupumzika. Kwa hivyo, Mhe. Rais atuletee watendaji wapya kuanzia Katibu Mkuu mpaka chini na wala hatuwezi kuendelea kuwatoa kafara mawizi huku ndani Mhe. Mwenyekiti kwa utendaji mbovu. *(Makofi)*

Mhe. Waziri nimemsikiliza uzuri sana na alisema kwamba tumuonee huruma kwa sababu yeye ni mpya. Lakini Mhe. Mwenyekiti, wakati alipokuwa akisoma Katibu wako alisoma uzuri sana kwamba vifungu vya fungu hili vinavyooneshwa hapa chini mapato yake yanasimamiwa na Katibu Mkuu Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano na sio na Mhe. Waziri, isipokuwa Mhe Waziri anakuja kutuomba tu, hivyo hawa si wapya.

Kwa maana hiyo, Mhe. Mwenyekiti Katibu Mkuu na timu zao za kila wizara watatufelishia kila mawaziri na tutamalizika humu ndani Baraza la Wawakilishi Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Kwa hivyo, mimi nasema Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu hatuyaoni mapato haya katika fungu hili wala fungu la Wizara ya Fedha la popote pengine na wala hatuoni utaratibu unaoeleweka wa matumizi ya mafungu haya. Mhe. Mwenyekiti, naomba kabisa kwamba bajeti hii tuirejeshe na tumwambie Mhe. Rais atutafutie timu mpya itakayoweza kusimamia shilingi bilioni 5 zinazoombwa hapa zitumike kwa tija ambayo wananchi wa nchi hii wanaitaka. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba maelezo ya hilo kwa Kiongozi wa Shughuli za Serikali katika Baraza hili Mhe. Mwenyekiti, kama si hivyo bajeti hii mimi hata kama peke yangu nitatoka hapa. Lakini mimi binafsi siwezi nikawasaliti wananchi wa Zanzibar nikapitisha shilingi bilioni 5 kwa wizi tuliouona katika wizara hii na wala sikubali hata siku moja Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, nimeipata *concern* ya Mhe. Mjumbe. Lakini mashirika akumbuke kwamba yanalipa *Corporate Tax* na yanachangia kwenye serikali. Kwa hivyo, fedha zao zitatokeza kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali na wala hayatatokeza kwenye mapato haya, isipokuwa idara ndio inayotokeza katika mapato haya.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima naomba kutafautiana na Mhe. Waziri. Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imeundwa mwaka jana, lakini buku hili lao linawasura serikali naomba tuangalie ukurasa wa 44 kuna Mamlaka ya Usafiri Baharini na wala hii haikuundwa mwaka jana Mhe. Mwenyekiti na inalo fungu lake hapa na ushahidi huu hapa Mhe. Mwenyekiti naomba uangalie hapo.

Sasa ulikuwa uhalali upi wa kisheria hiyo tunayoambiwa leo kwamba mashirika kwa utaratibu wa kifedha hayapaswi kutajwa hapa na fedha hizi shilingi milioni 163,000,000/= zikatajwa mwaka jana na iwe mwaka huu ghafla sheria imebadilika na hazitajwi tena Mhe. Mwenyekiti na wala hatuna hoja Mhe. Mwenyekiti.

Kwa hivyo, hapa kama nilivyosema kwamba kuna uoza mkubwa na katika hili Mhe. Mwenyekiti naomba tusitizame nyani usoni, sisi kama Wawakilishi hatupendi kila siku kuja kuwasulubu mawaziri hapa kwa makosa ambayo si yao. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba tena kwamba bajeti hii irudi na tumuombe Mhe. Rais atupe timu mpya ambayo tutakuwa na yakini na tutaridhika nyoyo zetu, kwamba wanakwenda kuzisimamia shilingi bilioni 511,000,000,000/= ya mapato yake katika wizara hii Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, ikiwa hivyo sivyo basi mimi nitaomba nitoke nje nikapumzike tukijaaliwa. *(Makofi)*

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani turudi kwenye sheria kwa nini labda mashirika yanapoombewa ruzuku yanaletwa kwenye vifungu. Nadhani katika kila shirika ambalo lina sheria katika mapato ya mashirika kile kifungu kinachozungumza mapato ya shirika huwa kinasema "*Funds Appropriated by the House of Representatives*" kwa ajili ya shirika, yaani ni moja ya ile *source* ya *fund* yenyewe.

Kwa hivyo, ndio maana lazima uombe hapa, kwa sababu Baraza ndilo lenye idhini kisheria ya kuweza kusema kwamba rukuzu hii inakwenda kwenye kifungu hichi cha shirika. Lakini unaposema kama ni shirika basi shirika yale mapato yake inakuwa sio sehemu ya Bajeti ya Serikali, isipokuwa ni bajeti ya shirika lenyewe, lakini serikali inachotoa kuwapa shirika basi ile ni lazima ionekane katika Bajeti ya Serikali, kwa sababu sheria yenyewe ya lile shirika tukisoma nadhani kuna vifungu mule na tutafute sheria ya shirika lolote lile utakuta kuna kifungu kinachosema hivyo.

Kwa hiyo, hilo ni wajibu wa kisheria kwamba lazima bajeti inapoombewa ruzuku lazima iwemo. Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la mapato shirika inao mchango wake wa shirika ama kwa utaratibu wa siku hizi uliowekwa wa kiserikali kwamba kama inalipia Kodi ya Mapato then na faida yake inalipia kodi kama kawaida.

Sasa kama kulikuwa na kosa kwamba yalioneshwa basi inawezekana ikawa ni kosa. lakini bado tunarudi katika Kanuni kwamba sheria utaratibu wake unatakiwa uwe hivyo, kuwa *appropriation* ioneshwe kwenye Bajeti ya Serikali, ili ipate idhini ya Baraza. Lakini mapato hayo si sehemu ya mapato ya serikali isipokuwa ni sehemu ya mapato ya shirika na mapato ya serikali ni kile kitakachokuja katika serikali kama ni mchango.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la watendaji pengine ni wezi. Kwa kweli suala la wizi ni au kukosa uadilifu ni suala la *facts*, ambalo linalohitaji kuthibitishwa. Kwa hivyo, mimi ninachosema ni kwamba kama kuna tuhuma hizo *Appoint Go Authority* inao uwezo wa kusema kuwa ninamuondoa leo ama ninamuondoa kesho.

Kwa maana hiyo, mimi nadhani itakuwa si sahihi kusema kwamba huyu mtu wakati bado hajatiwa hatiani na Mahakama ikasema kwamba lazima aondolewe, tukasema Rais lazima amuondoe kesho. Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema hiyo *concern* kama anaona kuna *inefficiency*, bado ibaki kwa serikali na kupitisha kwa bajeti hii sidhani kama inamuondolea mamlaka Rais ya kusema kwamba ninafanya mabadiliko.

Kwa hiyo, anaweza kufanya mabadiliko kesho au kesho kutwa ama siku yoyote, lakini sidhani kama itakuwa sahihi kusema kwamba *condition* ya kupitisha bajeti lazima mtu fulani lazima

aondolewe, kwa sababu na huyo unayesema aondolewe naye pia ana haki zake lazima uzingatie ni mipaka gani, kuna tatizo gani, utaratibu gani ndipo hatua ziweze kuchukuliwa kama ni hatua.

Lakini sidhani kama kutumia nyenzo ya bajeti kusema kwamba lazima mtu fulani aondolewe, sidhani kama hilo ni sahihi, isipokuwa njia sahihi ni kupitisha bajeti. Mhe. Mwenyekiti, *concern* ameshaisema Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwa kinywa kipana na serikali imesikia. Lakini tuiache serikali ifanyekazi yake na Baraza pia lifanyekazi yake. Nadhani hiyo ndio *checks and balance* na nadhani tutalijengea heshma Baraza hili kama tutaifata hiyo ili kuleta nchi yetu kwa ujumla iweze kuendelea.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, suala la Mamlaka hizi nafikiri Katiba yetu inafafanua vizuri kabisa. Moja ya kazi ya Mamlaka hii ambayo katika kifungu cha 5(a) imetajwa kwamba ni Mamlaka ya kusimamia utendaji wa shughuli za umma. Hapa moja katika jukumu letu na ndio maana tumeletewa sisi kuidhinisha mapato na matumizi. Ni kwa sababu sisi kwa niaba ya wananchi waliotuchagua ndio tunaosimamia fedha zao. Kama haturidhiki na matumizi ya fedha hizi au usimamizi wa mapato ni jukumu leo hapa sisi kuchukua hatua, wala hili halitokuwa ni jambo la kwanza kwa Baraza hili duniani la kutunga sheria ambapo pia linashughulikia shughuli za umma kuchukua hatua kama hizi Mhe. Mwenyekiti.
Hatuna hata haja ya kwenda mbali, hata hapo Dodoma tu tunashuhudia suala la mtu anapokuwa na serikali yenyewe ikaamua baada ya kuwa Baraza limetoa maamuzi yake kumpeleka Mahakamani hilo ni suala jengine. Lakini hilo haliondoshi mamlaka yetu na sisi kama ikiwa haturidhiki kutoa maelekezo hayo kwa serikali. Mimi naamini kwamba hilo ni jukumu letu kabisa Kikatiba Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu ilikuwa kuhusu mapato. Mimi nasema nimemfahamu sana Mhe. Mwanasheria Mkuu, lakini mimi najiuliza hii iliyojitokeza mwaka jana na serikali ni hii hii na watendaji ni hawa hawa, nadhani kama sikukosei niko tayari hata Mwanasheria Mkuu huyu tumepitisha hapa na tumeletewa fungu la mapato. Sasa mimi najiuliza hivi jukumu la chombo hichi kwa mapato yale yanayoingia pale ambayo ni fedha za walipa kodi, zinaingia wapi kusimamia fedha zile. Kama chombo hiki ni shirika hakina mamlaka ya kusimamia na kujua mapato yale ni kiasi gani na yanatoka kiasi gani.

Mhe. Mwenyekiti, kama ni hivyo nini mantiki ya kitabu hiki kuja kutuomba. Tatizo nililokuwa nikilisema jana hapa hili buku halisemi lakini kitabu hichi cha Mhe. Waziri kataja humu ndani. Labda nitoe mfano ili nifahamike vizuri zaidi. Mhe. Mwenyekiti, naomba nitizame ukurasa wa 41 wa hotuba yake. Anaizungumzia Mamlaka ya Uwanja wa Ndege, Mamlaka imepanga kukusanya jumla ya Tsh 3,060,072,000 na kutumia jumla ya Tsh 3,060,072,000. Mwaka jana vile vile akatwambia mpaka jinsi ilivyokuwa imeidhinishwa hapa na zilizoongezeka.

Mhe. Mwenyekiti, kama shirika linajitegemea tunajitegemea nini sisi hapa, ndio ogomvi wetu uliokuwepo hapo. Kwamba humu tunatajiwa, lakini hivi miye kama siridhiki na shirika lile, nalisimamia wapi kifungu kile Mhe. Mwenyekiti. Halionekani katika mapato, halionekani katika matumizi. Mhe. Mwenyekiti, bado nasema hili kama ni suala la *policy* la serikali kuja kutupa maelekezo hapa, tunaamua vipi juu ya mashirika haya, tuamue. Lakini mimi kunipa majibu tu kwamba kwa sababu ni Shirika halipaswi ku – *appear* nasema hii si Kampuni Mheshimiwa hata kama Shirika tumeliundia sheria zake na Mhe. Mwanasheria Mkuu kazitaja hapa. Lakini mimi

bado nasema tulipaswa buku hili lioneshe mapato yake hata kama yanaendelea kwa ruzuku, yale yanayohitaji kwenye matumizi katika ruzuku kama yanavyofanywe kwenye taasisi nyengine zinazojitegemea. Kwa sababu vifungu kama hivi kwa taasisi zinazojitegemea vipo takriban kwa taasisi zote. Kwa nini katika taasisi kama hizi zisionekani Mhe. Mwenyekiti. Mimi bado sijapata maelezo ya kuniridhisha hoja yangu.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Raisi Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nieleze kwamba nimefahamu vizuri sana *concern* ya Mhe. Ismail Jussa. Lakini vile vile nataka niseme Mhe. Jussa naye akubali maelezo ya Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa sababu huo ni utaratibu ambao upo kisheria na ndio tuliokubaliana. Kama kumbukumbu zangu ni sahihi mwaka jana tulipokuwa tunapitisha bajeti hii Mamlaka ilikuwa bado haijaundwa, ndio maana ikaripotiwa pale. Wenzetu waliporipoti katika bajeti yao walipaswa tu kusema kwamba mwaka jana ilikuwa ni Idara ndio kwa maana wakaripoti taarifa.

Lakini vile nataka nimsaidie tu Mhe. Jussa, Mwakilishi wangu wajimbo la Mji Mkongwe kwamba si vibaya kwa baraza nalo kupata taarifa juu ya mapato ya mashirika si vibaya. Kama tunakubaliana hivyo basi tukubali kwamba katika muda ujao, katika bajeti zijazo kwa kutoa taarifa kwa kupata taarifa sio kwamba tunaidhinisha mapato yao, tunatoa taarifa kwamba mashirika haya mapato yao ni hiki na hiki na matumizi yao ni hiki na hiki na wameomba ruzuku kiasi fulani. Ile ruzuku waliyoomba kama alivyosema Mwanasheria Mkuu ndio tunapaswa kuieleza katika Bajeti yetu.

Ninachotaka kumuomba Mhe. Jussa na namuomba sana jambo letu la msingi sisi kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ni kupitisha bajeti na kuisimamia utekelezaji wa bajeti. Suala la uteuzi tumuachie mwenyewe Mhe. Rais. Ninaimani kubwa sana Mhe. Rais, ametusikia amesikia kilio cha wananchi. Mimi nina imani kubwa sana Mhe. Rais ataangalia uongozi au utendaji uliyomo ndani ya Wizara hii.

Sisi jukumu letu la msingi kama viongozi wa Baraza ni kupitisha bajeti. Sisi tupitishe bajeti hii, tuisimamie bajeti hii kupitia Kamati zetu matumizi yake. Vyenginevyo tutakuwa lile jukumu letu la msingi hatulitekelezi. Namuomba sana Mhe. Jussa *concern* yake naifahamu sana namuomba sana.

Mwenzangu Waziri amesema hapa kwamba kupitia jina la Mtume (SAW) na mimi namuomba sana kupitia jina la Mwakilishi wangu wa Mji Mkongwe Jussa Ismail Ladhu namuomba sana aturuhusu tufanye jukumu letu la msingi kama ni Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Leo ni siku kubwa, siku ya Ijumaa, aturuhusu tuipitishe.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, jana kuna mtu alimwita Mhe. Omar Alhajj Mtarajiwa na yeye akamrekebisha akamwambia keshakwenda, yeye Alhajj tayari. Mimi nikamuuliza wa Makka au wa Malindi akanambia wa zote mbili.

Mhe. Mwenyekiti, nimemsikiliza hoja zake ninachosema mimi kama ingelikuwa Mhe. Mwenyekiti duniani tunakwenda kwa sababu ya mfumo kama ulivyoukuta uyaendeleze tu basi kusingekuwa na mabadiliko katika dunia hii tangu zama za Adam mpaka leo. Sasa kama utaratibu utakuwa umewekwa huko mimi *personal* siuwafiki.

Kama nilivyosema kama ni suala la *policy* ya serikali kuna haja ya kuiangalia tena hii. Kama ninavyosema ni lazima chombo hichi Mheshimiwa ni Mashirika ya wananchi. Kwa hivyo ninavyosema Mheshimiwa matokeo ya haya yanayoelezwa ndio yale niliyoyasema jana kwamba kuna watu wakishakukabidhiwa haya wanadhani ni *personal chief* damu zao. Ile kufanya wanavyotaka kwa sababu hii inayozungumzwa bodi itaburuzwa inavyotaka kwa sababu anajua kwamba yeye hahitaji hapa.

Mhe. Mwenyekiti, nimemsikia lakini ninachosema kwamba humu yote yametajwa na yameombewa fedha na yameombewa idhini ya mapato na matumizi. Lakini kwa sababu hiyo na kwa vile leo ni siku ya Ijumaa na tuna mengi ya kuhoji katika matumizi. Mimi nakubali hao Mheshimiwa tuendelee lakini *take note* kwamba yale mapato ambayo yametajwa katika hotuba hii ya Mhe. Waziri naya *take note* tutakuja kutaka maelezo baadaye kuja katika Kamati zetu ikiwa mwakani tukirudi hapa juu ya matumizi na *brake down* ya fedha zile za Shirika. Bado ni haki yetu kujua.

Mhe. Mwenyekiti, Baraza lako ni tofauti na Bunge halina Kamati tatu za *over site* commette PAC ni moja tu. Kwa wenzetu Bungeni kuna PAC, kuna POAC, ambayo kazi yake ni kuyasimamia Mashirika ya Umma ambayo Mwenyekiti wake ni Mhe. Vito Kagwe. Halafu kuna na LAK ambayo kazi yake ni kusimamia serikali za Mitaa. Hapa kwetu yote hayo yamechanganywa hapo chini ya PAC.

Mhe. Omar ananiomba mambo mengi namkubalia anajua kwamba mimi si mkaidi kwa hivyo ninachosema nakubali kwa hapa kwa mapato, tuendelee tutakumbana kivumbi katika matumizi. Mhe. Mwenyekiti, tuendelee ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe bahari nzuri na mimi nimekuwemo ndani ya chombo hichi kwa muda mkubwa na kuna baadhi ya mambo nayakumbuka. Kamati hii ya POAC ilikuwepo lakini baada ya mashirika mengi kuwa yameanguka hayapo tukaona kuwa itakuwa ni Kamati ambayo kuwa haina kazi. Kwa hiyo kwenye kanuni tukaiondoa na shughuli za mashirika machache yaliyobaki tukasema basi iangaliwe na PAC. Hiyo ndiyo historia ya jambo hili, lakini Kamati ya PAC kama anavyosema Mhe. Jussa ilikuwepo. Hilo moja.

La pili Mhe. Waziri na Mwanasheria Mkuu kazungumzia kuhusu kuripoti juu ya mapato. Kwanza nataka niseme Waheshimiwa Wajumbe wanayo haki kabisa ya kusimamia shughuli za serikali ndani ya serikali na mashirika, hakuna pahali tunapozuiwa kwenye mashirika tusisimamie hapana. Tunayo haki hiyo na huo ni utaratibu ambao naukumbuka kwa muda mrefu, kwamba mapato ya mashirika huwa hayaonyeshwi kwenye vitabu hivi.

Isipokuwa nataka niseme kwamba kama itakuwa hatukufunja sheria nadhani sio tatizo kutoa taarifa juu ya mapato ya mashirika na mamlaka mbali mbali. Kwa hivyo tuiachie serikali iangalie kama tutakuwa tumekwenda kinyume na sheria basi tunaweza tukatafuta utaratibu wa kurekebisha hiyo sheria ili mapato hayo pia waheshimiwa wajumbe wajue, wayasemee pale inapoonekana kuna mtereko wa kutopata vya kutosha kwa kuyaona mapato hayo na tofauti iliyopo ya kipindi kilichopita na kilichoendelea basi wajumbe wanawaweza wakasema na wakatoa mashauri juu ya masuala hayo.

Kwa hiyo nadhani tuiwachie serikali ili iangalie sheria kuhusu utaratibu wa kuripoti mapato hayo ili tusije tukawa chombo hichi tunafanya kitu kinachogongana na sheria. Lakini kimsingi inaonekana ni jambo la umuhimu kwamba mapato hayo yawe yanaonekana. Tunakushukuru sana Mhe. Jussa.

Tunaendelea.

Kifungu 0701 Idara ya Ujenzi na Utunzaji Barabara	6,000,000
Kifungu 0801 Idara ya Usafiri na Leseni	346,000,000
Jumla ya Fungu	**394,500,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadili yoyote)

FUNGU 26 – WIZARA YA MIUNDOMBINU NA MAWASILIANO

Kifungu 0301 Afisi Kuu Pemba

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii na hapa nitaeleza tena lile tatizo tulilonalo katika Katika Mawizara yetu kwa namna ambavyo Afisi zetu Kuu Pemba hakuna mafungu yanayohusiana na Idara.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niseme kwamba hili ni tatizo kwa sababu takriban linapelekea kukiukwa kwa taratibu za matumizi ya fedha za umma. Kama nilivyosema jana kwa Wizara ya Kilimo na Wizara hii ya Miundombinu tatizo ni lile lile. Nadhani hapa namuomba vile vile Mhe. Waziri wa Fedha anisaidie kwamba hili linapelekea kukiukwa kwa taratibu za matumizi. Tunafika pahala mdhibiti tatizo liko Pemba lakini tunapokwenda Pemba tunaambiwa jibu mtalipata Unguja, kwa sababu matumizi ya manunuzi yote yamefanywa Unguja. Mategemeo yangu kwamba litafanyiwa marekebisho.

Lakini hapa hapa kwa sababu hiyo hiyo Mhe. Mwenyekiti, niliulizia mpango wa serikali juu ya gati ya Wesha kwa sababu hili silijui nilipatie wapi. Nilitegemea kwamba fungu hili litakuwepo hapa, sera ya mipango Pemba kifungu kidogo kitakuwepo ili nifike pahala suala hili niliulizie kule. Naomba hapa nijibiwe mpango wa serikali hasa wa kuiendeleza Bandari ile ya Wesha. Serikali imetumia fedha nyingi lakini bandari haitumiki sasa hivi, mwezi kwa kupata mashuwa moja inakuwa ni kinyume ya matumizi ya fedha zilizopotea. Naomba serikali inipe msimamo nini hasa mpango wa serikali kuiendeleza Bandari ya Wesha.

Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Miundombinu: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru *concern* ya mjumbe tumeisikia na tuliipatia majibu kwa uchache tulipokuwa tukijibu. Lakini tuliichanganya pamoja na gati ya Wete majibu yake. Katika kipindi hichi cha bajeti hii itashughulikiwa gati ya Wete kwanza halafu baadaye ndio wataona fedha kiasi gani walizonazo ndio waishughulikie ya Wesha kutokana na ukwasi wa Shirika la Bandari. Lakini gati ya Wete itapewa umuhimu zaidi kwa sababu tayari ina abiria wengi ambao wanashuka pale. Gati ya Wesha inachukua zaidi

mizigo kuliko abiria, kwa hivyo *priority* iko kwenye ile ya abiria kwanza. Lakini tumeisikia *concern* yake na tualifatilia kwa kina utekelezaji wake uweze kupatikana.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, jibu la waziri linanisikitisha kidogo kusema kwamba Bandari ya Wete ni muhimu zaidi kulikoni Bandari ya Wesha. Mimi naamini na Bandari ya Wesha ni muhimu zaidi kulikoni Bandari ya Wete. Kwa msingi huo kwa nini basi serikali ikatumia fedha nyingi kuijenga bandari ile.

Maana yake inapofika pahala serikali ikawekeza fedha nyingi halafu ukaja ukasema kwamba bandari si muhimu zaidi kulikoni kitu chengine lile suala la *value for money* linakuwa halipo. Mimi naomba Mhe. Waziri anambie kwamba na Bandari ya Wesha nayo ni muhimu vilele kulikoni Bandari ya Wete.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, naona kaninukuu vibaya, nilisema kwa bajeti ya mwaka huu *priority* ni bandari ya Wete kwa sababu inahudumia abiria lakini sikutofautisha umuhimu wa Bandari ya Wesha lakini kwa bajeti ya mwaka huu. Kwa sababu Bandari ya Wesha ni Bandari ya mizigo basi itafuata baadeye kwa sababu nilisema katika kifungu change cha mwanzo wakati nikitoa majumuisho kwamba katika *priority* yangu kubwa ya mwanzo wakati ni usalama wa watu katika usafiri wa baharini. Siwezi kwenda kinyume na kauli ambayo nimeitoa pale.

Naomba Mhe. Mwakilishi akubali hiyo hoja kwa sababu hatuidharau. Miye ni mtu wa Chakechake na nikenda katika jimbo langu napitia hapo Weshe pamoja na kwamba ipo katika jimbo lake lakini nimepakana nayo. Wavuvi wa jimbo langu wanatumia, naijua umuhimu wake, wafanyabiashara wengi wanaitumia kuleta mizigo yao, naijua umuhimu wake lakini tumesema *priority* ni usalama wa watu kwanza halafu tena ndio nyengine.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, mwenyewe kajua lakini kwanza nilitaka nimkumbushekwamba wafuvi wa ndagoni na maeneo yote ndio wanayoitumia lakini mwenyewe kalikumbuka nashukuru. Katika hili nikitaka tu aniahidi lini au kipindi gani angalau kwa kweli na mimi angalau niwe na cha kujibu tu kwa wananchi wa jimbo langu. Ni lini Shirika au wizara watalingiza katika mpango huo.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, mimi binafsi nitachukua jukumu hili kuhakikisha kwamba bandari wanaipa kipaumbele mara tu baada ya matengenezo ya Bandari ya Wete. Kwa hivyo ikiwa ndani ya Bajeti hii kutatokezea lolote, kwa sababu hili ni shirika mapato yeke hasa ya matengenezo hayalazimiki kufuata bajeti hii kwa sababu hili ni Shirika. Ikiwa haikuwezekana cha mwanzo kitakachofanyikana katika bajeti ijacho ni bandari ya Wesha.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, hilo ndio balaa ambalo Mhe. Ismail Jussa kalizungumza kwamba wao hufanya vile wanavyotaka pasi na sisi Wawakilishi kuona nini kinachoendelea katika matumizi ya fedha za wananchi. Kwamba wanaweza wakafanya vile wanavyotaka wao bila ya kuangalia utaratibu hasa tuliokubaliana. Kwa hiyo hilo ndio tatizo moja. Kwa hiyo baada ya ahadi hiyo ya Mhe. Waziri na kwa kuwa yeye mwenyewe wapiga kura wake ni watumiaji wakubwa bandari ile nakubali tuendelee, ahsante.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru nadhani wale waliokuja na ule msemo tuachiwe tumue unatusaidia wengi hata na wewe umeuona umuhimu wa kupumua kwamba ukishakufanya kazi nzito unahitaji kupumua kidogo.

Mhe.Mwenyekiti, katika mchango wangu nilizungumza suala moja kama unakumbuka ulikuwa juu ya kiti wakati ule, kwamba nikidondoa kifungu kimoja kimoja sitovimaliza. Nikatoa orodha ya vifungu ambavyo ilikuwa takriban kila wizara nilikuwa nahitaji maelezo. Majibu ya jumla aliyonipa Mhe. Waziri ni kwamba nisitizame kile cha zamani nitizame hichi kipya kimesharekebishwa.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nimuhakikishie Mhe. Waziri kwamba nimekitizama hichi na nikalinganisha na hichi. Mimi ninavyoamini marekebisho hayo wanayoyafanya waheshimiwa Mawaziri dakika za mwisho kwa sababu watendaji wao wameshashtuka kwamba Baraza hili sasa linafatilia vifungu kimoja kimoja, ndio maana kila tukiingia tunapewa makaratasi haya mapya kila siku.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, nataka nimuhakikishie kwamba nimeshatizama na kwa idara ya Afisi hii Kuu ya Pemba naomba bado nipewe maelezo katika vifungu ambavyo nilivihoji jana. Bado nataka maelezo kwamba kwanini tuidhinishe fungu kubwa la safari kwa Afisi Kuu Pemba peke yake ni sitini na sita milioni laki nne liko ukurasa wa pili Mhe. Mwenyekiti pale. Mimi nilidhani katika marekebisho haya angalau lingepunguzwa. Lakini katika hichi kitabu cha original jumla ya safari Pemba ilikuwa ni 59 milioni, wao wamekwenda kuongeza, wameona hawajasafiri vya kutosha bado, kukaa hewani huko kunapendeza kweli kweli kwa wengine Mhe. Mwenyekiti. kwa hivyo wamekwenda kuongeza imekuwa ni sitini na sita milioni laki nne.

Vile vile niliitaka pia Mhe. Mwenyekiti, nipewe maelezo vile vile katika fungu hili la viburudishaji, ambapo mwaka jana ilikuwa ni shilingi milioni sita laki tatu, mwaka huu imeombewa milioni kumi na moja laki tisa. Takriban mara mbili yake. Nilikuwa naomba maelezo yake kwa Afisi Kuu ya Pemba na mengine nitaingia Idara zake zikifika. Naomba maelezo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli *concern* aliyoonesha Mhe. Mjumbe kuhusiana na kifungu kinachozungumzia suala la safari hasa safari za ndani kwamba zimeongezeka hadi milioni 49. Sababu ya msingi ya kuongezeka kwa kima hicho ni kutokana na posho ya tiketi pamoja na Idara. Kwa maana kwamba Idara sasa hivi zote tatu zinalipiwa kupitia Afisi Kuu Pemba. Idara ya Mipango, Idara ya Uendeshaji pamoja na Idara ya Usafiri na Leseni zote timekuwa *included* katika fungu hili moja la safari.

Suala la pili la milioni 11 zimetoka milioni 6 mpaka milioni 11 katika suala la viburudishaji na Usafiri. *Concern* kubwa ni hiyo hiyo kwamba Idara zimeongezeka kutoka Idara moja iliyokuwa ikisimamiwa na Afisi Mdhamini Pemba kwa maana ya kwamba wale *Incharge* wa zile *department* kwa upande wa Pemba na wao wote wanatumia fungu hili.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, unajua Mheshimiwa rafiki yangu Waziri wa Nchi, Afisi ya Raisi, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kapewa kazi kubwa sana ya kuzitafuta fedha ya kununua meli mpya katika mwaka huu wa fedha, tunamsaidia azipate.

Mhe. Mwenyekiti, niseme wazi mimi siridhiki na maelezo yaliyotolewa. Nina sababu zangu kwanza nimsaidie rafiki yangu Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano na jirani yangu hapa, leo tu kahama kwa muda.

Mhe. Mwenyekiti, fungu ukilitizama la safari katika marekebisho yaliyofanywa katika haya mahesabu mapya tuliyopewa haikuongezwa katika Safari za Ndani, wameshajiongezea vya kutosha kutoka milioni 28 mpaka milioni 49. Lakini safari za nje ndio ilikuwa milioni 10 ikafanywa 16.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani Naibu Waziri angenisaidia zaidi angeliniambia kwamba kumeongezeka kitu gani Pemba cha kufanya bajeti hiyo ya safari za ndani nadhani ndio ingelikuwa maelezo ya kunitosheleza. Bajeti ambayo kwa miaka mitatu mfululizo wakitizama treni pale, imekuwa milioni 24, milioni 28, halafu ghafla mwaka huu ichupe mpaka ifike milioni 49. Kumeongezeka activities gani zizopelekea safari za ndani, maana safari ninazozifahamu mimi ni baina ya Unguja na Pemba. Zingesaidiwa hizi takriban mara mbili yake, safari za ndani ziongezeke.

Lakini na safari za nje vile vile Mhe. Mwenyekiti kama nilivyouliza. Hivi karibuni hapa Mhe. Saleh ilibidi mpaka kumuofa tiket Mhe. Naibu Waziri, kwa jinsi ilivyokuwa mambo magumu. Fedha hizi badala yake aliikataa tiket kwa sababu pesa wanazo. Sasa nashangaa mimi kwamba bajeti hii iongezeke kiasi hichi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi jana nilisema kitu kimoja na hili nawatahadharisha tena na tena na tena Mawaziri, watendaji Mhe. Mwenyekiti watawamaliza. Jana nilisema yale mafungu ya ruzuku yaliyokuwa yanakwenda kwa sababu mara hii inaonekama mataasisi yanajitegemea. Katika kuwaongezea *ceiling* Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais Fedha walikuwa hawajui wazifanye nini, kwa hivyo pachika tu Afisi Kuu Pemba pachika hichi, mipango sera pachika hichi na tutayaona huko mbele tunakokwenda huko mbele, ukinipa fursa utayaona mengi .

Kwa hivyo mimi nasama bado mimi hajanirishisha, angelisaidia kunaongezeka shughuli gani zinazopelekea muongezeko wa safari za ndani za kufikia milioni arubaini na tisa laki tano kwa Afisi Kuu Pemba peke yake, mbali ya safari za nje kwamba kuna milioni kumi na sita, niambiwe safari za nje hizi kwa Pemba zinakwendewa wapi na Maafisa waliokuwepo Pemba. Lakini mle kuna na viburudishaji navyo pia hajanaipa maelezo bado, nilisema kwamba hili fungu limeongezeka mara mbili, fungu la viburudishaji Pemba kutoka milioni 6 mpaka milioni kumi na moja laki tisa takriban mara mbili. Hebu nielezwe kuna shughuli gani.

Mhe. Mwenyekiti, shughuli ndio zinazopelekea kuhalalisha kuongezeka kwa matumizi. Siku moja mlitwambia kwamba tatizo msishtuke na mafungu kuongezeka, lakini muhoji kuna shughuli gani. Sasa nilikuwa nataka hizo *activities* kwa kufuata wasiwa wako nisaidiwe kumeongezeka *activities* gani. Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, *concern* ya Mhe. Ismail Jussa Ladhu, mwakilishi wangu wa Mji Mkongwe naiyona. Mhe. Jussa mimi nataka nimshukuru tokea tumeanza bajeti na baada ya kumaliza bajeti ya Taifa ile amekuwa akihoji pamoja na waheshimiwa wengine baadhi ya vifungu na kuniomba na kunishauri nivipitie kama Waziri mwenye dhamana ya fedha.

Mhe. Mwenyekiti, tokea siku ya kwanza kama utakumbuka nimeahidi kuvipitia baadhi ya vifungo hivyo na kuona kwamba kama kuna pesa ya ziada kulingana na maelezo ambayo nitakayoyapata basi niweze kuihamisha na niipeleke katika maeneo mengine ambayo inastahiki kutumika fedha ile.

Nataka nimuhakikishie Mhe. Jussa na Waheshimiwa Wajumbe nina vifungu 19 naviangalia na naviangalia kwa Wizara zote na kwa Idara zote. Nataka vile vile nimpongeze sana Mhe. Rais, baada ya kunipa kazi ya kutafuta fedha kwa ajili ya meli, nguvu ya kuviangalia vifungu hivyo imezidi. Nataka nimuhakikishie Mhe. Jussa na Waheshimiwa Wawakilishi vifungu hivi wala asipate wasi wasi kuvipigia buti, serikali imeshafanya maamuzi kuviangalia na nikifika siku ya bajeti yangu nitawambia ni kiasi gani cha fedha nitakihaulisha kutoka kwenye kifungu hicho.

Nitaka niwambie watizame vifungu vyengine, hivi vifungu Safari za ndani, safari za nje, vitafunio, semina, vikao, wavipunguzie budi. Serikali imeaamua na nitakuja kuliomba Baraza hili hili siku ya bajeti yangu kuniruhusu nihaulishe kiwango cha fedha ambacho nitakachokipata kwa ajili ya shughuli nyengine.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Ismail Jussa Ladhu, kabla hujaeleza kitu nataka niseme jambo moja tu, pengine Mheshimiwa Barazani usije maana nina Kamati Teule nyingi.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Mawaziri wa serikali makini wanakuwa kamka Mhe. Omar Yussuf Mzee, kwamba panapoonekana panadosari hawatetei tu. Ingelikuwa katika hili tunasikilizana Mheshimiwa nafikiri ingelikuwa hatupati tatizo na mawaziri wote hapa.

Mara nyingi tumesema kwamba mafungu haya kila ukurasa wake unaanzia yanasimamiwa na Katibu Mkuu. Waziri lakini ndio kizungumkuti wa *process* hii. Anaekuja hapa kuomba na baadaye kuja kujibu baada ya mwaka ni waziri. Ndio maana tukawambia sisi ni wenzao kwa niaba ya wananchi tunawasaidia kuyaonesha hayo anayoeleza Mhe. Omar Yussuf. Sitaki kupoteza muda wako Mhe. Mwenyekiti, nataka nimshukuru Mhe. Omar Yussuf kwa msingi huo aliyosema nakubali tuendelee, lakini lile moja tu alilonionba.

Mhe. Mwenyekiti, lile la buti naomba aendelee kutuvumilia buti tutaendelea kupiga Mhe. Mwenyekiti. Kwa sababu sisi *record* yetu Mhe. Mwenyekiti, katika Hansard ni hii. Tukimuachia yeye tu halafu tutakuja kuwa hatuna pahala pakuja kumuhoji. Kwa hivyo hili la kupiga buti labda ikiwa kila baada ya buti moja vifungu hivi, atanyanyuka yeyote katika serikali akatoa majibu kama yale, nafikiri itapunguza hii kusimama mara kwa mara. Lakini kuyahoji tutayahoji kwa sababu tunataka ikae katika *record* ya serikali kwamba sisi wasimamizi wa fedha za walipa kodi, haturidhiki na matumizi haya.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti, nakubali kwa moyo mkunjufu na namuamini Mhe. Omar Yussuf naomba tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri wa Fedha, kubali buti zipigwe ili wakuoneshe maeneo mengine ya kupata pesa unununlie meli.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, mimi kama nilivyomuhakikishia Mhe. Ismail Jussa Ladhu, katika vifungu hivi buti wazipunguze, kwa sababu tayari nimeshazifanyia kazi. Vifungu vyengine waendelee kupiga buti na wakitaka buti mpya nitawapa mimi.

Mhe. Mwenyekiti: Na kweli jana wakati wa michango alisema mmoja mpaka buti itachanika. (Vicheko).

Kifungu 0301 Afisi Kuu Pemba 1,356,800,000

(Baraza linarejea)
(Baraza lilirudia)

Mhe. Spika: Waheshimiwa wajumbe ninafikiri muda uliobaki ni mdogo na leo ni Ijumaa kazi iliyobaki ninafiikiri sio ndogo sana, kwa hivyo ninafikiri tungesitisha shughuli zetu hapa na tuje tumalize baadae lakini nikiwaomba sana waheshimiwa wajumbe kwamba kazi hii tunayokuja kuifanya baadae inahusu kuwepo wajumbe wengi, kwa sababu tunafanya maamuzi. Kwa hivyo time tutayokubaliana pengine nane na nusu sina hakika, tuhakikishe kwamba tunafika kwa wingi ili tumalize hii kazi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa kuwa shughuli iliyo mbele yetu inahitaji muda wa kutosha ili tuweze kuifanya kwa ufanisi na kwa kuwa leo ni Ijumaa na muda wetu wa siku ya Ijumaa kwa mujibu wa kanuni zetu ni mpaka saa sita na hasa ukizingatia kwamba huu ni mwezi mtukufu wa Ramadhani. Kwa hivyo Mhe. Spika, naomba tuweke kanuni kando ya muda ili tuakhirishe Baraza kwa sasa tuwahi kusali Ijumaa na baadae saa nane kamili barabara tukutane hapa kwa ajili ya kuendelea na shughuli mpaka pale tutapoweza kumaliza shughuli iliyo mbele yetu.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

(Saa 6.00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 8.00 mchana)

(Saa 8:00 mchana Baraza lilirudia)

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 – Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano

(Majadiliano yanaendelea)

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU 26 - WIZARA YA MIUNDOMBINU NA MAWASILIANO

Kifungu 0401

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia suala la mamlaka na nilisema kuwa kuna barua ambayo alipewa ambaye ni mwenye Meli ya M.V. Serengeti lakini bahati mbaya niseme Makamo hakuweza kunijibu ameghafilika nakubaliana naye. Kwa hivyo naona sasa anipe jibu kutokana na barua hii aliyopunguziwa abiria kwa mizigo kwa Meli ya M.V. Serengeti na wakati meli hii imesharudi kwenye chelezo na imekaguliwa rasmi na kitengo chake. Naomba Mheshimiwa wangu anipe jibu kwa sababu barua hii inatakiwa ipelekwe *inclination* na hiyo anayo mhusika Mkurugenzi sasa naomba anisaidia maarifa ili niweze kupitisha sitaki kumzuilia fungu lakini kidogo nipate taarifa rasmi na yeye mtu mzima, mwenye busara naomba kidogo anisaidie.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Mhe. Mjumbe alionesha *concern* hiyo wakati akiwa anachangia. Na ni kweli kwamba pengine wakati tunamjibu hakutufahamu vizuri, lakini tulichokizungumza ni kwamba baria hiyo ni kweli imetoka mamlaka kwenda kwa mmiliki Mkurugenzi wa Kampuni ya *RAC* ambayo maudhui makubwa ilikuwa ni kumtaka mmiliki wa meli hiyo kwenda kufanya *inclination experiment*. Maudhui haya yanatokana na mamlaka ambayo tumempa Mkurugenzi, Mkurugenzi wa *ZMA* chini ya sheria Nambari 5 ya mwaka 2006 amepewa mamlaka ya kukagua, kusimamisha ama kuzuia chombo chochote atakapojenga shaka kwamba chombo hiki kina matatizo basi anayo mamlaka hayo ya kuzuia.

Kwa hivyo, ninachotaka kumwambia Mhe. Mwakilishi kwamba, uzuiaji ule uliomzuia mmiliki wa meli kwa kumataka kwamba meli ile iendelee katika *exclamation experiment* haimaanishi kwamba ule ukaguzi wa kwanza kuwa haukufanyika. Ukaguzi wa kwanza umefanyika lakini kwa mamlaka aliyokuwanayo Mkurugenzi anayo kila sababu ya kutaka kujiridhisha ili kuona kwamba usalama wa chombo hiki bado uko vizuri ili kuruhusu kutumia huduma hizi za kubeba abiria. Sasa matarajio yangu kwamba, katika kipindi hiki ambacho meli hii imetakiwa kwenda katika ukaguzi tena ameruhusiwa kupunguza idadi ili kutambua kwamba tukipunguza idadi bado ataweza kufanya shughuli zake na siku ile ambayo amepangiwa kwenda kufanya huo uchunguzi atakwenda. Kwa hivyo, nimuombe tu Mhe. Mjumbe aturuhusu tuendelee sababu yetu ya msingi ni hiyo tunachotaka kuzingatia hapa zaidi ni usalama wa vyombo vyetu pamoja na raia wetu wanaotumia usafiri katika vyombo husika.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, ninavyojua mimi meli inapokuwa katika chelezo kabla ya kushushwa kuja huku kufanya kazi anakuwa mtaalamu ambaye amebobea ana *certificate* zake zote, anakwenda kule kukagua na akatoa maelekezo ya kuwa aa huku hakuna tatizo lolote na kuweza kuja hapa kuendelea na shughuli zake. Lakini sasa nataka kumwambia Naibu Waziri hili suala mimi kidogo limenishitusha kwa sababu inavyoonesha yeye huyu Mkurugenzi hawaamini wataalamu wake kwa mantiki hio. Mimi ninachosema tupunguze kazi, aturuhusu aidha tutumie kifungu cha 120 ukurasa wa 92 au airuhusu kamati yake yenye ikajiridhishe kwa sababu lazima kutakuwa na kitu, sioni sababu kubwa hapa Mhe. Naibu Waziri kunijibu ya kitaalamu mimi sijafahamu utaalamu huo. Kwa sababu hiki kitu *inclination* unatoa baadae na hiki kitu kimekwenda kabla na hiki kitu anacho, kwa nini akaruhusu kutoa *certificate* baada ya kukagua hii *inclination* yenyewe.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu aliyotoa Mhe. Naibu Waziri kwa kirefu napenda nimwambie Mhe. Mwakilishi kwamba meli haikuzuwiwa imepunguziwa idadi ya abiria ili waweze kufanya hiyo *inclination test* kama meli ile ina uwezo wa kubeba abiria zaidi ya hao au laa. Hii ni kutokana na mwenendo wake wa meli katika kipindi hiki cha karibuni, kwa hivyo si suala la kuwa ilifanyiwa au haikufanyiwa, kama ilivyosomwa sheria hapa wakati wowote Mkurugenzi kwa mamlaka yake atavyoona kwamba chombo kutokana na mwenendo yake inavyoripotiwa basi anayo haki ya kuamrisha ifanyiwe chochote kile.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, nilifikiria Mhe. Waziri atanijibu zaidi kwenye utaalamu. Mhe. Mwenyekiti, ilipotoka kwao hii meli ilikuwa ina abiria elfu moja, hayo ma-*book let* hao, *inclination* yenyewe, *experiment* na nini, imetoka kwao inachukua abiria 1,000; imekuja hapa mamla hiyo hiyo imeona ipunguze ikawapunguzia mia nane, baada ya hapo ina maana kwamba ina *expire inclination* kama ina *expire date* hii nikubaliane nayo, laa kama haina *expire date* basi ningeomba kabisa twende na wakati. Kwa sababu mimi nahisi hapa kuna mchezo na ndio maana nikaingia wasiwasi. Kwa sababu kuna meli hata haijafika hapa imeshajitangaza ina uwezo wa kuchukua abiria 1,500 wakati meli ile ni pantoni lingeweza kuwekwa pale Mkwajuni na Tumbatu basi ndio saizi yenyewe meli hiyo.

Halafu isitoshe hiyo meli huko kwao ishaonesha kuwa ina uwezo wa kuchukua abiria 740, *low season* ina uwezo wa kuchukua watu mia nne, lakini leo kwenye gazeti ni abiria 1,500 sasa mimi wasiwasi wangu ni huu, tusiwaonee hawa kwa misingi ya kuwajengea watu wengine tukawafanyia biashara. Ni kweli nakubaliana nalo lakini hebu twende na wakati na mimi niliwaambia hebu muiteni tukae naye mumsikilize, mumpe sababu.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Mwakilishi atufahamu hasa ni kwa sababu alikuwa Mwenyekiti wangu sijui leo kwa nini picha zikawa zinatisha sana. Ni kwamba vyombo hivi vinavyotembea baharini vinafanyiwa ile *routing check* mbali, lakini kuna na *checking* ya dharura inaweza ikafanywa wakati wowote. Sasa anachozungumza Mjumbe ni ile *routing check* ambayo wakati inapokwenda katika *dry-dock* na nini, hii ni ya dharura.

Mimi nahisi kwamba, kama chombo chenyewe ni kisafi, kizuri, kuna wasiwasi wa nini wa kufanyiwa hiyo *experiment*. Kwa hivyo naomba Mhe. Mjumbe ajiridhishe kwa sababu vyombo vyengine baada ya kuonekana vimefutwa kabisa, na yeye anavijua lakini hii haikufutwa wala haikukatazwa kwenda isipokuwa imepunguziwa idadi ya abiria kutokana na namna inavyoyumba ile meli. Sasa ili kuridhisha matakwa ya kitaalamu basi ifanyiwe hiyo *experiment* iki *prove* itaendelea kufanya kazi. *(Makofi)*

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti sawa, Wajumbe nawaombeni msipige makofi kwa sababu mengine inakuwa hatusikii, pahala pa kuruhusu mtatufanya tukwame kuruhusu. Mhe. Mwenyekiti, nimemsikia Mhe. Waziri sasa nataka nimuulize lini itafanywa hiyo.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa hiki ni chombo cha binafsi yeye madhali keshapewa taarifa hiyo ilikuwa aende kwenye mamlaka na wapange namna gani ya kufanya, lakini kwa kuzungumza lini yeye hatapangiwa kwa sababu yeye ndiye mwenye dhamana ya kuona kwamba kile chombo chake kinafanyiwa ule ukaguzi kwa sababu ni cha binafsi. Kwa hivyo, wakati wowote atakapokwenda kuonana na mamlaka wataifanya hiyo *experiment* na ikiridhisha atapewa ruhusa ya kusafiri.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, mimi sitaki kuwa mbishi hata kidogo na hasa alivyonitaja Mwenyekiti wake lakini Mwenyekiti lazima akasirike na yeye akiona manyago.

Mhe. Mwenyekiti sawa, lakini sasa kwa taarifa mimi ningeomba kuwa hebu nipeni sheria moja nataka nipate, sasa itabidi twende kwenye sheria kama alivyonielekeza Mwanasheria Mkuu. Huu utaratibu barua kama hii anasema hivi, naomba kuisoma Mhe. Mwenyekiti, anasema hivi, “kupunguziwa abiria kwa mizigo ya meli M.V. Serengeti, kwa heshima naomba uhusike na mada iliyopo hapo juu. Mamlaka ya Usafiri Baharini inakutaka kuanzia tarehe ya barua hii upunguze abiria kutoka 850 hadi 350 na mizigo kutoka tani 100 hadi 50 hadi hapo meli hiyo itakapofanyiwa *inclination experiment* ili ijulikane uwezo wake halisi ili kuchukuliwa abiria na mizigo. Naomba mashirikiano yako katika kudumisha usalama wa abiria wetu”.

Sasa mimi wasiwasi wangu ni hapa pamoja tu padogo, kuwa lengo na madhumuni ilikuwa nani amtaarifu mwenzake kumuita njoo tupange, ilikuwa huyu baada ya kupewa barua ndio afuatilie au wizara imuite kwa kufanya ukaguzi huo. Ndio hapo tu akinijibu hapo sina tatizo.

Mhe. Mwenyekiti: Waziri tusaidie naona mambo yote yako wazi wazi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano kwa ufafanuzi mzuri na nimpongeze sana. Kwa sababu katika kipindi kifupi ameonesha uwezo mkubwa sana wa kufanya shughuli hiyo.

Vile vile nimshukuru Mhe. Makame Mshimba, Mhe. Mwenyekiti, sote tunaelewa janga lililotukuta kutokana na usafiri wa baharini hasa meli hizi chakavu, ni uamuzi wa serikali uliopitishwa na Baraza la Mapinduzi kwamba meli hizi chakavu zote zifanyiwe uchunguzi upya ili kuhakikisha usalama kwa wananchi wetu. Haya yote yameelekezwa na Baraza lako hili tukufu

Mhe. Mwenyekiti. Sasa tunapochukua hatua za kuhakikisha usalama wa watu wetu wakati huo huo tena anatokea Mjumbe anavunja moyo jitihada hizo kidogo mambo haya yanahuzunisha na yanaweza kusababisha majanga makubwa.

Mhe. Mwenyekiti, mambo yale ni ya kitaalamu sisi hata tukienda sote pale hatuwezi kugundua chochote na yapo kwa utaratibu wa kisheria. Ni vizuri Mhe. Mwakilishi akatuamini na akaviamini vyombo vyetu vilivyowekwa kwa mujibu wa sheria vifanye kazi yao. Kwa sababu akienda yeye Mhe. Mjumbe kufanya uchunguzi likitokea la kutokea na yeye atakuwemo, atakubali kubeba dhamana hiyo? Mheshimiwa haya mambo lazima tuyafanye kwa utaratibu mzuri ili tuendelee kufanya shughuli zetu. Namuheshimu sana Mhe. Mshimba lakini ajue kwamba tunavyoingia kati mambo haya yanaweza kutukuta mambo ambayo ni kinyume kabisa na taratibu zetu. Kwa hivyo, naomba Mhe. Mwenyekiti, tuheshimu mamlaka yetu ya sheria, sheria tunazitunga wenyewe tufanye kazi yetu ili tukamilishe wajibu wetu. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nishataka kuridhika, lakini sasa ndio siridhiki kabisa. Kwa sababu moja nilikuwa tayari nishakubaliana naye na nilikuwa jawabu langu dogo tu, kwamba ni nani mmoja wapo anayepaswa kumuita mwenzake ilikuwa limekwisha lile suala. Angenambia Mhe. Waziri aa mimi nina uwezo wa kukuita wewe au yule aliyepelekewa barua hii ana uwezo wa kwenda yeye, lakini asizungushe huko kwa sababu kama ni kweli tuna nia hiyo kama serikali basi mimi nafikiri Mheshimiwa huko asiende kwenye lugha hiyo.

Kwa sababu lugha ni hapa padogo tu, ushanifahamu Mhe. Mwenyekiti, lugha yangu ni ndogo tu lakini hawataki kunifahamu tena Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais ni mtu ninayemuamini sana mimi, akinambia kunako serikali nitamwambia anipe barua iko wapi iliyoonesha hiyo atakuwa hana. Sasa mimi sitaki niende huko ninachosema mimi jibu dogo tu, ili niridhike nani atakayeweza kumuita mwenzake basi, ilikwisha. Waziri amuite yule aliyepewa barua au aliyepewa barua afuatilie Mhe. Mwenyekiti, mbona tunajizonga.

Mhe. Mwenyekiti: Mimi nadhani hayo mengine tungeacha, kama mwenye meli ana haja masuala yake yamalizike muache aende na ndio alivyosema hapa. Waziri anasema wakati wowote aende kule aombe wazungumze kwa sababu suala hapa inafanyiwa *test* ili tuepukane na hizo nakama zinazotokea mara kwa mara. Nadhani tuendelee.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nachangia niliomba kupata maelekezo na msaada juu ya suala la barabara ya Kisiwandui, lakini Mhe. Waziri alipokuwa akizungumza hapa Mhe. Naibu Waziri alikuwa amejibu lakini yale majibu aliyonijibu hayakunitosha. Skuli ya Kisiwandui tumeshashuhudia watoto wawili tayari wamefariki kwa ajili ya barabara ile na wenye daladala wanavyokwenda mbio, sasa pale tunaomba matuta, kama matuta hayawezekani kuna hatua gani za dharura zitachukuliwa ili kunusuru vifo vya watoto katika eneo lile. Nilikuwa naomba majibu sahihi katika hili.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Mhe. Mjumbe alionesha hiyo *concern* ya eneo hilo kwamba aliomba matuta. Katika majibu yangu nilichomjibu ni kwamba Wizara yetu ya Miundombinu na Mawasiliano suala la uwekaji wa

matuta sio kipaumbele, lakini kwa kuzingatia suala la usalama nilimwambia sisi tutashirikiana na wenzetu wa Manispaa kuweka alama za *zebra* ambazo tunaamini madereva wetu wataziheshimu ili kujikinga na ajali hizo ambazo zinapelekea kupoteza maisha kwa vijana wetu wanaosoma skuli hiyo.

Sasa ninalotaka kumhakikishia Mhe. Mjumbe ni kwamba, muda wowote kuanzia Jumatatu sisi wenyewe binafsi tutakwenda na wenzetu wa Manispaa kwenda kuweka alama hizo za *zebra* katika eneo husika ili kuwakinga vijana wetu na ajali zinazoweza kuepukika.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na matuta yatakayokuja kuwekwa pale kuanzia Jumatatu tunaomba na vyombo vya ulinzi vile vya usalama kama *traffic* wawepo kila wakati ambapo watoto watakuwa wanaondoka katika maeneo yale. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, wakati jana nilipokuwa nikichangia kuhusu Mamlaka ya Usafiri uwanja wa ndege pale nilizungumzia kuhusu *ZAT*. Mhe. Mwenyekiti, katika michango yangu nilisema ni lazima tuweke mbele maslahi ya nchi kuliko maslahi ya watu binafsi. Katika mchango wangu nilisema kwamba hii Kampuni ya *ZAT* imeajiri vijana wetu wengi, sasa wakati Mhe. Mwanasheria Mkuu ananijibu hapa alisema kwamba *ZAT* kuna baadhi ya mapungufu ambapo kuna masharti hawakutimiza na kuna mapungufu mengine inabidi wayarekebishe.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, naanza kupata khofu kwamba matokeo ya uchunguzi aliyoutoa Mhe. Mwanasheria Mkuu unanipa mashaka, kwa sababu sijui nani kachunguza, inaonekana pale kuna *conflict of interest*, huyo mchunguzaji nina wasiwasi kwamba ana *interest* pale na lengo lake kubwa ni kuwafanya hawa *ZAT* waondoke na badala yake waje watu ambao yeye *interest* yake italindwa. Katika hili Mhe. Mwenyekiti, mimi naishauri serikali kwamba *ZAT* ni Wazanzibari, *ZAT* wana haki sawa na Wazanzibari wote waliopo katika nchi hii, na kama ni uchunguzi basi ningeomba serikali iniambie kwamba nani kachunguza, alikuwa *impartial* kweli huyo au ana *lay down their all personal interests?*

Ninachoomba Mhe. Mwenyekiti, ni vyema Baraza lako hili katika kumtendea haki huyu *ZAT* likaunda japo Kamati ya kuweza kuchunguza ili kuweza kutoa haki. Mimi kwa mujibu wa taarifa nilizonazo ni kwamba wale kila *specification* wanazopewa *ZAT* na serikali wamezitimiza, leo serikali inatwambia hivyo tumuelewe yupi ni mkweli. Ni vyema ikaundwa tume kwenda kuchunguza mwenye haki akapewa, lakini majibu ya Mhe. Mwanasheria Mkuu hayakuniridhisha kwa sababu yame-*lay down personal interest***,** kwa hivyo wale watu wame *create conflict of interest* kusudi *ZAT* aonekane ni mbovu pale waweke mtu wanayemtaka wao.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nimemsikiliza kwa makini Mhe. Saleh Nassor Juma na nashukuru leo kasema pole pole nimeweza kusikia. Nilipokuwa najibu kwanza nilisema kwamba kitu cha mwanzo kilichofanyika pale ni kutimiza matakwa ya kisheria ambayo ilipitishwa na Baraza hili. Sheria ile kifungu cha 23 kifungu kidogo cha 4 na 5 kimeeleza wazi marekebisho ya utendaji na utoaji huduma katika uwanja wa ndege. Moja kimesema kwamba, si ruhusa kutoa mkataba wa ukiritimba isipokuwa kwa masharti maalum, lakini mamlaka inaweza ikaingia mikataba mipya na wale ambao walikuwepo pale. Lakini pia kimeeleza kwamba, Baada

ya miezi sita mikataba yote iliyokuwepo pale basi itakuwa imefutika na mamlaka itaingia mikataba mipya na wale ambao wanatoa huduma pale. Hilo ni jambo limo ndani ya sheria sio la kwangu, sio la uchunguzi wala sio la serikali peke yake ni Baraza hili ndilo lililopitisha sheria hiyo. Wajibu wa serikali kuisimamia na serikali imefanya hivyo katika kuisimamia.

Lakini la pili nikasema, serikali kwa kujua umuhimu wa *ZAT* na katika sera ile ile ya serikali ya uwezeshaji ilijua *ZAT* ni Kampuni ya Wazalendo, lakini bahati mbaya *ZAT* haishughulikii wazalendo watupu inaishughulikia dunia inayokuja Zanzibar kwa kupitia uwanja wa ndege. Kwa hivyo, lazima baadhi ya mambo yarekebishwe ili kutoa huduma kwa mujibu wa vigezo vitakavyokidhi vile viwango vya kimataifa vya kutoa huduma, na baada ya hapo ndio serikali ikaagiza basi timu ya serikali kaeni na *ZAT* mtizame mambo gani yarekebishwe mueleze, lakini mtizame pia na katika kuyarekebisha hayo uwezo wao utakuwaje.

Timu hiyo ambayo ilichunguza kwanza haukuwa uchunguzi yalikuwa ni mazungumzo ambayo yalikuwa ya wazi, ya bayana *ZAT* walipelekewa barua, wakaitwa kwenye vikao, wengine wakaja wengine hawakuja Mwenyekiti wao tunamshukuru Mhe. Mohamedraza Hassanali alionesha mapenzi yake na imani ya kutaka *ZAT* iendelee akawa anakuja. Na suala hili akalishughulikia lakini alikaa. Upande wa timu ya serikali alikuwa ni Katibu Mkuu Kiongozi, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na mimi mwenyewe Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Tukataka taarifa zao tukachunguza taarifa, uwezo wao wa kifedha, wa kiutendaji na masharti mengine waliyopewa, ni wenyewe ambapo tunasema kwamba *ZAT* labda niseme imekuwa kama vile Mhe. Mohamedraza, kama si uwezo wake yeye na kutaka iendelee kesho inaweza ikafa Kampuni haiendeshwi hivyo, kampuni inaendeshwa kwa misingi ambayo inafaa.

Sasa mimi nasema kama kuna mtu anaipenda *ZAT* iendelee na iendelee kutoa huduma kwa kiwango kile cha kimataifa kwa sababu *ZAT* ni kampuni ya wazalendo jamani inashughulikia dunia na pale inaposhughulikia ndio kioo cha Zanzibar, ndio uso wa Zanzibar. Lazima viwango vya kutoa huduma vilingane na viwango vya *airport* nyengine duniani au katika Mkoa huu. Kwa hivyo hayo ndio waliyotakiwa, na hakuna mtu ambaye kama mimi nina *personal interest* Mhe. Saleh Nassor aseme asimame aseme, kama Katibu Mkuu Kiongozi ana *personal interest* au ana *conflict of interest* asimame aseme atoe ushahidi mbele ya Baraza hili, na kama Katibu Mkuu Wizara ya Fedha ana *personal interest* asimame aseme kwa uwazi, lakini hili limefanyika kwa uwazi na serikali kama si kwa imani ya *ZAT* ingesema basi isimamishe atafutwe mtu mwengine, lakini serikali kwa kuthamini hilo ikasema jamani *ZAT* iendelee iimarishe hili na hili, lakini lazima tukuze ufanisi katika utoaji wa huduma. Hilo ndilo lililotokea na hakuna *personal interest* ni *interest* ya nchi na mimi nasema serikali kwa kweli imekuwa na huruma na mapenzi makubwa na *ZAT* ndio maana ikaruhusu iendelee.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, kama kuna mtu ambaye namheshimu sana na ninamuogopa pamoja na kwamba nimemzidi kiumri ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Namuheshimu sana na hata hivyo neno la ziada la kumuheshimu ni kumstahi. Sasa katika hili Mhe. Mwenyekiti, kwanza Mhe. Mwanasheria samahani sana sijataja mtu nimeeleza wasiwasi wangu kwamba inaonekana kama kuna *a set of conflict of interest* pale, na wasi wasi unaweza ukawa wa kila mtu, kila mtu anaweza akapata wasiwasi, mimi naweza nikapata wasiwasi. Jaji anaweza kupata wasiwasi hata mshtakiwa anaweza akapata wasiwasi.

Sasa mimi Mhe. Mwenyekiti, naendelea na wasi wasi wangu katika hili kwamba *there is a conflict of interest* pale baina ya baadhi ya viongozi na kampuni nyengine jambo ambalo Mhe. Mwenyekiti, Wazanzibari tunaathirika sana watu wana-*lay down personal interest* huku kundi la Wazanzibari tukiendelea kuathirika. Huyu kaajiri vijana karibu 200 hawa *ZAT* sasa tukiwakatia ajira vijana 200 wale watazubaa kutupigia maunga huku wakituibia viatu vyetu misikitini jambo ambalo ni tatizo.

Mimi naomba kwamba wasiwasi naendelea kuwa nao na hata hii sheria hapa ninayo nayo inanipa wasiwasi kidogo Mhe. Mwenyekiti, naomba uniruhusu dakika mbili niinukuu ile ya Kiswahili na hii ya Kiingereza.

Sheria katika kifungu cha 23 (5) inasema:

> "Isipokuwa kwa mikataba itakayoishia mapema mikataba yote itakayoingiwa na idara",

Hiyo IDARA naomba iwekwe kwa *capital letter* Mhe Mwenyekiti.

> "Mikataba yote itakayoingiwa na IDARA kabla ya kutungwa sheria hii itaendelea kwa kipindi cha miezi 12 kuanzia tarehe ambayo sheria hiyo itaanza".

Tulifanya marekebisho hapa ikawa miezi sita, naomba niishie hapa kwanza nije kwenye hii ya Kiingereza ambayo inasema kwamba,

Kifungu cha 5 cha sheria kinasema:

> *"Save for those contract terminated on the earlier days all contracts anchor by the department or by other government institutions".*

Huku ilikuwa ni idara lakini huku kataja *government institutions*, hii hatukuipitisha sisi hapa tuliyoipitisha ni hii ya Kiswahili pamoja na mabadiliko yake, iliyokwenda kusainiwa na hii tuliyoipitisha tofauti. Kwa hivyo ndio nikasema mimi napata wasiwasi Mhe. Mwenyekiti, na sipati wasiwasi kwa ajili yangu binafsi, napata wasiwasi kwa wale vijana 200 ambao tumewaajiri pale.

Isijeikawa kama anataka kutucheza shere hapa akawa anataka kuleta watu akaendelea kuajiri Wakenya, Wajuluo kama inavyofanyika huko kwenye sekta ya utalii mashamba. Hilo ndilo tatizo langu Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, watu wanasema dawa ya wasi wasi ni imani. Ukiona mtu ana wasi wasi kakosa imani. Sasa sijui Mhe. Saleh kakosa imani na nani na serikali au na mtu.

Mimi ninadhani angemtaja tu nani ana wasi wasi naye ili tukapata kushughulikia ndio Baraza hili kazi yake kushughulikia mambo kwa uwazi na sio kuficha ficha. Sasa mimi nadhani angeweka wazi.

Lakini yote nimejaribu kumueleza, mimi ninasema mengine nitangulia nilipokuwa ninachangia kwamba mengine hatutaki tuyazungumze hapa kwa sababu tutakuwa tunawasema watu mambo wao ya ndani ambayo mengine ni unfair kwa sababu hawana haki ya kujieleza mbele ya chombo hiki, mbele ya hadhara tunayosema wananchi wote wanatusikia.

Mimi sipendi tuyachambue mambo ya ZAT ya ndani. Kama anataka tufanye hivyo tutafanya lakini mimi ninasema hayatosaidia ZAT, hayatomsaidia Mhe.Saleh wala hayatosaidia hao wenye hisa ambao Mhe. Saleh anadhani anawatetea wale waajiriwa.

Sisi serikali tunapenda tumuhakikishie na Mhe. Mwenyekiti, na Waheshimiwa Wajumbe na Mhe. Saleh kwamba kwa kweli serikali katika kufanya uamuzi huu imezingazingatia sana moja hilo kwamba ZAT imeajiri watu wengi na tukaulizana watu wale wale utawapeleka wapi.

Lakini suala la kwamba ZAT inahudumia dunia, hilo ni lazima tulizingatie. Tumelalamikiwa, tumeletewa barua mbali mbali. Mimi binafsi yangu nimekwenda mpaka Italy katika kuzungumzia huduma za uwanja wa ndege namna gani ya kuziboresha. Hayo ni moja katika mambo ambayo tumeyazingatia katika kuwaambia ZAT rekebisheni.

Mimi ninasema suala la ZAT ni wana hisa wenyewe, wakitaka kuwa wakweli, wakitaka kuwa wadhati kufanyakazi kwa imani baina yao wakaaminiana na bila ya wenyewe kukomoana. Mimi ninaamini ZAT inaweza ikafanya vizuri na naomba hilo Mhe. Saleh awasaidie hilo kueleza biashara wafanye namna gani.

Hili la sheria Mhe. Saleh mswada huu ulipokuja ulikwenda kwenye kamati na kamati ikaja na mapendekezo ya kurekebisha. Miongoni mwa marekebisho ambayo kamati ilipendekeza kwenye ukurasa wa 5 wa taarifa ya kamati, ilisema kwamba miongoni mwa mapendekezo ni kifungu cha item ya 27 ya mapendekezo yake. Ni kurekebisha kifungu cha 23 (5) mstari wa pili kutoka juu, baada ya neno idara, liliopo baina ya neno iliyoingiwa, yaongezwe maneno, au na taasisi nyengine yoyote ya serikali kwa niaba ya idara.

Sasa hayo huyakuti kwenye mswada lakini hayo yamo kwenye mapendekezo ya kamati ambayo Mhe. Waziri aliyakubali na ndio maana yakaingizwa katika sheria. Sasa hapa hapana tofauti. Huo ndio utaratibu wetu.

Sasa hilo ndilo jambo ambalo lilifanyika. Kwa hivyo hakuna kilichoongezwa wala hakuna kilichopunguzwa. Sheria imeingizwa maneno ambayo yalipendekezwa na kamati. Sasa kama anaona labda nimuazime hii aweze na yeye kujiridhisha pia nitampa Mhe. Mwenyekiti, kwa muongozo wako.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, mimi katika masuala ya sheria ni ngumbaro, nina maana kwamba sina taaluma yoyote kama mambo haya ya sheria. Lakini Mhe. Mwenyekiti, kiongozi ni naibu wa Mwenyezi Mungu duniani. Nadharia mbali mbali zinaonesha hivyo na hata maandishi matakatifu yanaonesha kwamba kiongozi ni naibu wa Mwenyezi Mungu katika uso wa ulimwengu, anatakiwa atende haki.

Uadilifu wake unapimwa na kuna siku ataulizwa kwa Mwenyezi Mungu, nadharia zinaonesha hivyo na maandishi matakatifu yanaonesha hivyo.

Maneno ya serikali nimeyasikia kupitia kwa Mwanasheria Mkuu lakini maneno ya ZAT hawana msemaji hapa. Kwa hivyo hayasikiki. Ili haki itendeke katika hili kwa sababu kwa mujibu wa taarifa nilizonazo wamepewa specification ili waweze ku-exist pale wamezikamilisha.

ZAT wameweza ku-meet hayo mambo ya kimataifa pale wameyakamilisha. Sasa tatizo kwamba wao hapa hawasikiki anasikika serikali tu. Ninatoa rai Mhe. Mwenyekiti, ili Baraza lako wewe ndio unaotuongoza na watu wapo nyuma yako wanakuangalia iundwe Kamati Teule iende ikafuatilie suala hil, ili tutakapofika mbele ya Mwenyezi Mungu tuweze kujibu. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe nilikuwa ninalalamika hapa asubuhi nikamwambia Mhe. Waziri Waziri wa Fedha kwenye vifungu vya Baraza asije, maana Kamati Teule nyingi. Nilisema hivyo na kwa kweli zinachukua sehemu kubwa ya matumizi ya afisi yetu.

Mimi ninafikiri Mhe. Mwanasheria Mkuu maelezo aliyoyatoa yapo wazi na hiyo haki ambayo viongozi sisi ni naibu wa Mwenyezi Mungu duniani inatakiwa tuende kwa mujibu wa sheria tulizojiwekea na ndio hizo alizozisema Mhe. Mwanasheria.

Ninadhani maelezo yapo wazi na yanatosheleza. Tuendelee.

Mhe. Hamza na Mtando wamefahamu kwamba hoja sasa zimekwisha tuendelee.

Kifungu 0401 Idara ya Mipango na Sera shs.250,000,000/=
Kifungu 0701

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia suala la ujenzi wa barabara nilizungumzia kadhia ya waathirika nikawataja kwa idadi 171, Shehia nikazitaka kwa idadi, Shehia karibuni nne; Shehia ya Kidimni, Dungabweni, Koani na Ubago.

Tathmini nikataja wazi wanadai milioni kumi na nne laki moja sitini na saba elfu mia tatu na tisini saba na senti hamsini tangu tarehe 9 mwezi wa nane 2006, ni miaka sita iliyopita awamu nzima ya Serikali ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, katika ufafanuzi pia nikajaribu hivi sasa haraka haraka ukurasa wa 2 pana watu orodha ya watu 9; watu 9 hawa wa Shehia ya Dungabweni Jimbo la Chwaka. Hesabu ya haraka wanaodai watu 9 hawa Mhe. Mwenyekiti, ni shilingi laki mbili, mia sita na tisini na sita elfu na senti ishiniri na tano.

Watu hawa Mhe. Mwenyekiti, wamekatiwa mifenesi, miembe ambayo walikuwa wanategemea wakodishe ili waishi na familia zao. Hii hesabu kila nikiangalia Mhe. Mwenyekiti, kwenye kichwa changu inanipa mashaka. Hesabu ndogo na miaka mingi.

Lakini pia nikashauri nikasema kuwa kuna vifungu vinaonekana wizara imejipangia hata wananchi wetu wakisikia watahuzunika. Watu wamejipangia viburudishaji nikataja mpaka na

kifungu 0901 wametoka shilingi milioni nne mpaka milioni kumi na sita laki moja na tisini elfu. *Almost* pana *different* ya milioni kumi na mbili kutoka mwaka jana na mwaka huu, lakini wananchi hawa miaka sita wanadai shilingi milioni kumi na nne Mhe. Mwenyekiti.

Pia nikanukuu kifungu cha 0401 Idara ya Mipango na Sera, Safari za Ndani wametoka shilingi milioni kumi na moja mpaka shilingi milioni arobaini. Almost pana different ya shilingi karibu ishirini na tisa, watu wanasafiri wanyonge wa nchi hii wanakufa njaa ni miaka sita.

Mhe. Mwenyekiti, alipokuja Mhe. Naibu Waziri majibu aliyonijibu yale yale ambayo haturidhiki nayo ni majibu ya kisiasa. Serikali itajitahidi, eeh! ndio majibu yetu serikali ipo mbioni ni miaka sita Mhe. Mwenyekiti.

Mimi ninataka anieleze kwa sababu ndani ya bajeti siioni atajitahidi vipi, aniambie kwamba kwa sababu wananchi hawa wanaotoka katika Jimbo la Chwaka atatoa mfukoni kwake sawa Mhe. Mwenyekiti. Naomba kukaa.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundumbinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, ninashukuru kunipa nafasi hii na ninapenda tu nimuhakikishie Mhe. Ali Salum Haji kwamba tatizo alilolisema la fidia ni tatizo kubwa kwenye wizara yetu.

Kama atakuwa amenisikiliza vizuri wakati na mimi ninatoa mchango wangu tulisema takriban shilingi bilioni tatu tunadai hivi sasa au zinazidi katika tatizo la fidia. Nilichomuhakikishia Mhe. Mwakilishi na Baraza lako tukufu kwamba kadri ya hali itakavyokuwa tutapunguza madeni haya.

Sasa ninataka kumwambia Mhe. Mwakilishi ni imani yetu kwamba madeni haya kwa kusema tupate pesa zote kwa wakati mmoja tuyapunguze tutashindwa kufanya hivyo. Lakini ninamuomba Mhe. Mwakilishi ajenge imani kwa kutambua kwamba imani huzaa imani.

Azma hii ya serikali tunayo ya kutaka kupunguza madeni haya. Ndio maana tukaweka msimamo serikali kwamba tusivunje nyumba kabla ya kulipa fidia. Hilo tumelimudu kwa hatua ya kwanza. Hatua ya pili tunakwenda katika yale maeneo ambayo tunadaiwa kwa muda mrefu tuone serikali inajipanga vipi kutafuta fedha kwa ajili ya kupunguza hizo changamoto ya wananchi ambao wanaotudai.

Sasa Mhe. Mwakilishi akichukua *reference* ya milioni kumi na nne, yeye anachukua *reference* moja lakini ukichukua *reference* ya wizara tuna deni kubwa. Ninachotaka kumuhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba *concern* ya serikali kutafuta namna kuona kwamba madeni haya yanapunguzwa kadri hali ilivyo kidogo kidogo.

Mimi ninamuhakikishia kwamba mradi wetu huu wa barabara yetu ya Amani/Dunga tutachukua hata ikiwa katika malipo ya mwisho tutakayomlipa mkandarasi basi utaona serikali tunatumia jitihada gani ili kuweza kupunguza kadhia hii ya wananchi wetu.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, sina haja ya kulumbana na Mhe. Naibu Waziri na hususan watu wanavyotujua historia zetu mimi na yeye.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, hizi jitihada anazozizungumza Mhe. Naibu Waziri azioneshe mpaka. Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kwamba wizara wana maeneo mengi lakini pia tuangalie na muda. Mimi ninachokifahamu baada ya utafiti wangu kuna watu wanalipwa kwa upendeleo. Kuna watu wanadai miaka sita lakini kuna watu wa miaka mitatu au miwili tayari wameshalipwa. Bahati hizo mbaya hizo kumbukumbu mimi sikujanazo lakini akizitaka nitampelekea afisini kwake.

Sasa hii ndio hofu kwamba hawa wananchi bado wanateseka. Mhe. Mwenyekiti, ninataka nimueeleze labda anachokitaka yeye wamalizike wote. Miongoni mwa watu hawa basi watu watatu wameshakufa. Sasa anasubiri wameshakufa wote akilipe marehemu.

Mhe. Mwenyekiti, sisi nsi Waislamu tunapata shida kubwa na hofu. Mimi nilikuwa ninamtania hapa mheshimiwa ninasema jamani haya majanga ya miundombinu siku nyengine ni dua za watu, nilikuwa na hofu hiyo Mhe. Mwenyekiti.

Kwa sababu mwananchi mnyonge kumkatia miti yake kama mifenesi minne ambayo alikuwa anaitegemea izae halafu apate pesa akiishi na watu wake na unamuachilia mpaka anafika kufa, hali ile haioni ni miaka sita.

Mhe. Mwenyekiti, bado ananiambia jitihada. Mimi anieleze tu kwamba jitihada hizo zitaishia lini. Hata kama miaka mitano aniambie baada ya miaka mitano jitihada hizo tutamaliza, nitakaa na kuwalipa pesa wananchi wa Dunga.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundumbinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, nimemuelewa Mhe. Mwakilishi concern yake na uzito wake wa jambo hili.

Ninachomuhakikishia kwamba katika bajeti hii tutalipunguza eneo hilo la barabara hiyo ya Amani/Dunga kwa kutambua uzito wa jambo lenyewe lilivyo. Lakini nilichomwambia Mhe. Mwakilishi kwamba ukitaka majukumu ambayo niliyokuwa nayo ya madeni ya fidia ni makubwa. Lakini uzito wa jambo hili tutalichukua.

Ninachomuhakikishia katika bajeti hii kwa namna yoyote ile kutafuta fedha kuweza kupunguza hilo deni ambalo analolisema. Kwa hivyo ninamuomba tu Mhe. Mwakilishi aendelee kujenga imani juu ya wizara yetu.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Naibu Waziri nimemsikia yeye kasema imani huzaa imani na mimi ninasema ahadi ni deni muungwana ni kitendo. Tuendelee.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Ninashukuru Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kuniona, maana inaonekana huko mbele mumekaa watu warefu kidogo huku nyuma kuona ni taabu. Nimeshanyanyuka sana.

Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu niliompelekea Waziri niliulizia suala zima la ujenzi wa uwanja ambao ulibomolewa na watu wa barabara kukawa kuna makubaliano baina ya watu wa barabara na timu ya Potoa FC ndani ya Jimbo langu la Mkwajuni.

Mwaka jana hapa nilitaka kuzuia kifungu nikaambiwa nikaachie nikaahidiwa kwenda kufanyiwa utanuzi wa uwanja ule baada tu ya kumalizika bajeti ya mwaka jana ile, lakini mpaka hii leo ninavyokwambia Mhe. Mwenyekiti, nimekuja kuulizwa juzi ule uwanja upo upande gani. Nikawaeleza lakini hapajafanyika kitu.

Sasa nilikuwa ninataka kujua tu Mhe. Waziri baada ya bajeti hii vile vile nitapewa ahadi kama ile au nitafanywa nini.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe Mwenyekiti, ni kweli Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Mkwajuni juu ya *concern* hii ambayo ameieleza.

Tulimuahidi kwamba tutakwenda kumtengenezea uwanja wake wa Potoa FC kwa wakati huo ikiitwa timu ya Banyamulenge. Ahadi yetu ni kwamba baada ya bajeti tutakwenda.

Lakini kwa bahati mbaya sana tulijikuta kwamba kazi zimetutinga zimekuwa nyingi, kuna matatizo ya vifaa vyetu vingi vichakavu na kuharibika na ni kweli kwa siku za karibuni walitendaji wetu walimtafuta Mhe. Mwakilishi kwa ajili ya kwenda kuifanya kazi hiyo.

Yeye Mhe. Mwakilishi akatoa ushirikiano kwa kuwaelekeza na watendaji wetu wakenda katika maeneo husika, lakini bahati mbaya makubaliano yetu ya awali yalikuwa ni kuongeza eneo la uwanja. Lakini watendaji wetu walipokwenda juzi wakapewa eneo jipya, kwa maana kwamba ujengwe uwanja mwengine mpya.

Sasa hilo pia halikuwa tatizo. Tatizo lililojitokeza kwamba eneo hilo walioneshwa watendaji wetu lina matatizo. Matatizo yenyewe kwamba mawe yaliopo pale ni mawe yanayoitwa ya kuota lakini zana ambayo waliyokuwa wamekwenda nayo ilikuwa ni zana ndogo.

Sasa *bulldozer* letu kwa bahati mbaya wakati tunafanya kazi katika Jimbo la Uzini lilikuwa limeungua. Kwa hivyo ninachotaka kumuhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba bulldozer lile lipo katika harakati za kutengenezwa na litakapokamilika tu ninamuahidi kwa kauli moja kwamba tutakwenda kufanya kazi ya kujenga uwanja huo wa Banyamulenge ili kutimiza ahadi yetu lakini pia kumtimizia ahadi za Mhe. Mwakilishi alizoahidi vijana wake hao kwamba yeye atawasimamia, na ninaomba vijana hao waamini kuwa Mhe. Mwakilishi amewasimamia ametufikishia kauli yetu kama sisi waungwana tutakwenda kutekeleza kwa vitendo kuujenga uwanja huu.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, ninashukuru kwanza kwa Mhe. Naibu Waziri kukiri. Sasa mimi kwanza ningemtaka Mhe. Naibu Waziri awaombe radhi vijana hawa kwa sababu amewadanganya.

Mwaka jana baada ya bajeti tu ninakuja lakini mpaka imekwisha, anatoa ahadi mpya na mimi nilikuwa ninamsikiliza tu pale ahadi mpya nahisi tutakuwa tunadanganywa tena. Kwa kusema kwamba amekwenda kupewa eneo jipya la kujenga uwanja mpya si kweli, kwa sababu ule uwanja ulimegwa nusu, wao watu wa barabara ndio walionunua hilo eneo la pili kwa ajili ya kuutanua huo uwanja. Kufidia kule wameshafidia kwa hawa watu wenye vipando vyao.

Wao walikuwa bado kwenda kuusafisha ili vijana wale waweze kutumia. Kwa hivyo si kwamba ni eneo jipya labda wanajenga uwanja mpya si kweli. Ni eneo lile ambalo walikubaliana lakini wao hawajaenda kulitekeleza mpaka hii leo. Leo ninaanza kupewa ahadi basi bora mimi Mhe. Mwenyekiti, nimuomba Mhe. Naibu Waziri atoe tarehe maalum ya kwenda kufanya ile kazi tushirikiane mimi na yeye tuhakikishe kazi inakwenda kufanyika.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa sana ninapenda kumuhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba azma yetu hii itatimia. Mimi kikwazo chetu hapa ni tatizo moja tu kwamba kifaa chetu kikubwa cha kufanyia hiyo kazi kimeharibika,

Namuomba Mhe. Mwakilishi atoe ahadi hiyo ya tarehe mwenyewe anayoitaka, bulldozer litakapotengenea mimi nitakwenda kumuonesha kwamba limeshapona twende tukafanye kazi Mkwajuni.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi ninafikiri Mhe. Naibu Waziri atakuwa hajanifahamu. Mhe. Naibu Waziri amekuwa ananidanganya kwa sababu kwa makubaliano tuliyokubaliana mwaka uliopita na mwaka huu ninanaza kupokea ahadi nyengine. Hivyo hili *bulldozer* limeharibika mwaka mzima, mbona maeneo mengine linakwenda kufanyakazi.

Au hawa watu wa Potoa FC wamekosa nini. Mimi naomba Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Naibu Waziri anisaidie aniambie hasa ni lini kazi ile itakwenda kufanywa. Mimi sina tatizo nitaridhia hivi sasa hili fungu liende zake lakini anihakikishie Mhe. Waziri maana Mhe. Naibu Waziri anaonekana ameshanidanganya sana, sasa ninamuomba huyo Mhe. Waziri mwenyewe mpya.

Hebu asimame hasa aniambie ni lini watakwenda kunifanyia hiyo kazi yangu, mimi nimridhirie lakini Mhe. Naibu Waziri ishakuwa simuamini anadanganya sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Kwanza Mhe. Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mhe. Mtando kwa kuamini kwamba ninaweza kutekeleza hiyo kazi. Kwa hivyo na mimi ninamwambia kwamba kwa niaba ya wizara na Idara ya UUB tutaitekeleza kazi hiyo mara tu bulldozer letu litakapokuwa katika hali ya kuridhisha.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu hii ni ahadi ya Waziri mpya, mimi ninaridhia tuendelee.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, wakati nikichangia nilikuwa nikichangia barabara ya Amani au maarufu barabara ya Benjamin Mkapa.

Barabara ile tangu mwaka jana imekuwa ina kigugumizi kwa serikali na katika kikao cha Bunge tayari SMT ilikuwa imeshatoa pesa zote kwa Serikali ya Zanzibar. Sasa inaonesha wazi ni aibu kubwa ambayo sisi hatuwezi kuhudumia barabara zetu wakati pesa tayari zipo.

Na vile vile wakati wa bajeti ya mwaka jana hapa Mhe. Hamza alijenga hoja kuwa kwa nini watu wanapewa watu wa nje, tukaaambiwa kifusi kinachotiwa pale kuharakisha mvua isishe ili

barabara ile ijengwe kabla ya mwezi wa tatu itakuwa imemalizika. Lakini mpaka leo barabara ile imekuwa ni mtihani mkubwa haipitiki, umati uliokuwepo kule ni mwingi, hebu naomba maelezo ya kutosha niweze kujua barabara hii ni lini itakwisha.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba Mhe. Benjamin William Mkapa wakati akiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alitoa ahadi ya kuisaidia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika ujenzi wa barabara hiyo ya Amani/Mtoni yenye urefu wa kilomita nne.

Fedha kweli zimetolewa ingawa fedha zile zilichelewa kupatikana kwake na kuanza matumizi kama ilivyokuwa imekusudiwa. Lakini ni kweli kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imepokea fedha hizo na ikatupatia Idara yetu ya UUB.

Matumizi ya fedha hizo tayari Mhe. Mwenyekiti, nimeyaeleza kwenye majibu yetu ya leo, kwamba fedha hizo zimetumika kwa ajili ya kifusi, kutengenezea zana, kulipa maposho watendaji. Changamoto iliyobaki tukasema kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeshafanya maamuzi ya kumaliza barabara hiyo kwa fedha ambazo zitatoka katika mfuko wa barabara kwenye bajeti ya mwaka huu 2012/2013.

Kwa hivyo ninataka kumuhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba katika bajeti hii fedha zile ambazo zilizokuwa zina mapungufu kutoka fedha zile ambazo zimechangiwa na Serikali ya Muungano wa Tanzania zitakamilisha ujenzi wa barabara hii ya Amani/Mtoni.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, sitaki kubishana hata kidogo na ndugu yangu Gavu na inaonesha wazi hatupo serious na kazi za wananchi ambao wametuchagua.

Tunatakiwa tuwe serious na majukumu ambayo tumepewa ya usimamizi lakini bado tunaonesha hatupo serious, tangu mwaka jana mwezi wa tatu, tumeingia mwaka huu wa bajeti hakuna hata wale vibarua waliokuwepo pale hawajalipwa. Naomba Mhe. Naibu Waziri akubaliane na mimi hata wale vibarua waliokuwepo pale hawajalipwa naomba hili anieleze kidogo ili niridhike niweze kumuachia.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, suala alilolisema Mhe. Mwakilishi kuhusiana na barabara hii maelezo yote tumeyatoa. Lakini suala la kwamba kuna vibarua ambao hawajalipwa, hili ni gei masikioni mwangu.

Namuomba Mhe. Mwakilishi atupatie orodha hiyo na sisi kama uongozi wa wizara, tutawaita watendaji wetu na kuwauliza kulikoni, kama kuna watendaji walioshiriki katika kazi hiyo hawajalipwa. Kwa sababu taarifa tuliyokuwa nayo sisi miongoni mwa matumizi yaliyotumika katika fedha zile ni pamoja na kuwalipa posho watendaji ambao waliokuwa wakishiriki katika zoezi la ujenzi wa barabara ile.

Kwa hivyo kama kuna watu ambao hawajalipwa namuomba sana Mhe. Mwakilishi atupatie orodha tutawaita watendaji wetu kuona kwa sababu gani hawakutimiza ahadi yao kama taarifa ambavyo wametupatia.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, ninasema hao watu wapo na leo wamekuja kwangu lakini wakataka kuja hapa kuandamana kwenye bajeti hii inayoendelea, lakini nikawazuia ili mimi mwakilishi wa wananchi nije hapa nizungumze na serikali, na serikali imenisikia na mimi nitawapa watu hao, nitampa orodha yake au nitakwenda nao wote ili aweze kuwaona na hatimaye waweze kusawazishwa matatizo yao.

Mhe. Mwenyekiti, naomba tuendelee.

Kifungu 0701 Idara ya Ujenzi na Utunzaji Barabara shs.1, 458,500,000/=
Kifungu 0801 Idara ya Usafiri na Leseni shs.591, 700,000/=
Kifungu 0901

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa ninachangia hotuba hii ya Mhe. Waziri nilitoa malalamiko juu ya watendaji wake wa idara hii walivyohusika na kughushi viwango vya mishahara na hatimaye viinua mgongo kutoka milioni thamanini hadi milioni mia moja na sitini na moja, ikiwa ni ongezeko la milioni thamanini na moja.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri amekiri kwamba hilo limetokezea lakini kwa kuchukua hatua ya kuwasimamisha kazi watendaji watatu. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri kwanza anielimishe watendaji hawa watatu wamesimamishwa hapa Unguja au Pemba.

Lakini pili hawa waliosimamishwa kazi ndio wenye jukumu la kuandaa viinua mgongo. Naomba kujibiwa hayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi sina budi kumshukuru sana Mhe. Hija Hassan juu ya kuonesha *concern* yake hii kutokana na kadhia hii ya upotevu wa fedha za serikali na nimshukuru tena kwa namna ambavyo analiuliza ili kutaka kujua undani wa suala lenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, wafanyakazi hawa waliosimamishwa kwa Unguja na Pemba. Tulichokifanya wizarani ni kwamba taratibu ziliohusika kwa mujibu wa sheria na kamati ya nidhamu tumeshawaandikia wenzetu wa Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa hatua zaidi ikiwemo pamoja na Tume ya Utumishi Serikalini, ili kuchukua hatua za ziada kwa wahusika hao.

Kwa hivyo, namuhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba wahusika hao kwa Unguja na Pemba, wote wamechukuliwa hatua hiyo ya kusimamishwa.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, sisi hapa Barazani tunaidhinisha fedha na msimamizi wa fedha hizi ni Katibu Mkuu wa wizara husika na ndiye ambaye Baraza hili linampa fedha kwa ajili ya kusimamia. Sheria ya fedha na sheria ya manunuzi pia inamtambua yeye kuwa ndiye dhamana wa fedha za serikali kwenye wizara yake, na kuna adhabu ambayo hutolewa kwa Afisa kushindwa kusimamia majukumu yake, ikiwa ni pamoja na fedha. Sasa Mhe. Naibu Waziri ananiambia kwamba wamechukua hatua ya kuwasimamisha kazi. Lakini Wazanzibari wangehitaji kujua fedha yao ni lini itarudi, milioni 81 ambayo watu hawa

walisababisha fedha ile ipotee ni fedha ya serikali. Bila shaka naamini kwamba limetokezea juzi, lakini ni miaka mingapi huko nyumba yaliwahi kutokezea.

Mhe. Mwenyekiti, tuyawache hayo ya nyuma, lakini hili la juzi namuomba Mhe. Waziri aniambie, pamoja na kuwasimamisha kazi hawa watu ambao yeye anawajua, lakini mimi siwajui, lakini fedha ya serikali ambayo imepotea kwa uzembe ni lini itarudishwa na pia aniambie kwa nini tuwaamini tena kuwapa fedha idara hii ambayo watendaji wake sio waaminifu ndani ya serikali hii.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, niendelee tena kumshukuru Mhe. Hija Hassan kwa *concern* yake katika eneo hili. Mhe. Mwenyekiti, hii kadhia yenyewe ilivyotokezea naomba nichukuwe nafasi ndogo, kueleza hili tatizo lenyewe hasa lilivyotokezea.

Mhe. Mwenyekiti, kulikuwa kuna wafanyakazi wetu ambao muda wao wa kustaafu ulikuwa umefika. Kwa kawaida Afisa wetu wa Utumishi ambaye ndiye anayehusika katika uandalizi wa hayo mafao ya wahusika. Sasa orodha ya watu ambao walikuwa wanapaswa kulipwa walikuwa ni wengi, takriban ni zaidi ya watu 13 na huo udanganyifu ukawa umefanyika. Sasa wenzetu wa wizara husika kwa kupitia wizara ya kazi wakaliona hili tatizo, wakatujulisha na walipotujulisha fedha zikazuiwa, ikawa kuna watu watatu ambao waliwahi kulipwa na waliosalia wakawa hawajaliwa kwa kutambua tu kwamba kulikuwa kuna makosa ya uwekaji kumbukumbu sahihi. Kwa hivyo, kilichoendelea ni kwamba hawa watatu wametakiwa kurejesha fedha hizi serikali ambao wamelipwa kinyume na taratibu, lakini wale kumi hawajalipwa kinyume na utaratibu, na utaratibu wa kuwalipa malipo sahihi unaendelea serikalini.

Kwa hivyo, napenda nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba *concern* ya serikali ni kuona kwamba wale ambao watakuwa hawajaliwa, lakini wana haki ya kulipwa na wamemaliza muda wao wa utumishi serikalini, watalipwa lakini kwa mfumo ambao uko sahihi na uwazi wala hauna ubabaifu na wale watatu ambao watakuwa wamelipwa kwa njia ya ubabaifu, basi serikali itawachukulia hatua ya kuwataka kurejesha fedha hizo, kwa sababu kuchukua fedha hizi ni kinyume na sheria na taratibu za serikali za kutumia fedha kinyume na utaratibu.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, mimi namfahamu sana Mhe. Naibu Waziri, na nampongeza kwa kunijibu vizuri. Lakini Mhe. Mwenyekiti, fedha hii anakabidhiwa Katibu Mkuu ndiye mdhamini wa fedha, na mbali ya ripoti hii ya ofisi kuu ya utumishi Unguja ambayo ninayo mkono wa kushoto hapa, kuna ripoti kubwa zaidi ya wizara hii hii Pemba kwa mkono wangu wa kulia, hii sijaizungumza. Pia hii hii inahusu hii hii Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano.

Swali langu ni kwamba kwa nini tuwaamini watu ambao hawaaminiki kukopa fedha.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, ninachokiomba sana kwa Baraza lako hili tukufu ni kujenga imani. Maelezo yametolewa hapa asubuhi na Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ya kuomba tu kwamba tuendelee na kupitisha bajeti. Kama kuna mapungufu mengine ya kiutendaji sehemu na mamlaka husika zitakuwa zinasikia, sisi wajibu wetu ni kuja kusema haya ambayo yako katika jukumu letu na

panapo makosa sisi kama wahusika tutaendelea kuwaagiza walio chini yetu kama watendaji na kama kuna maamuzi mengine ambayo sisi hatuna mamlaka, basi ngazi husika zitakuwa zinasikia. Lakini naomba Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mwakilishi ajenge imani, kutokana na tatizo hili lilivyokwenda serikali na wizara yetu tumechukua hatua, ikiwemo kuwasimamisha kazi, kufuata taratibu kwa mujibu wa sheria ya utumishi ili kuona kwamba haki inatendeka. Mhe. Mwenyekiti, aliyetenda makosa haya bado ana nafasi ya kujitetea mbele ya vyombo husika na ndicho hicho ambacho tumekifanya.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, haja yangu ilikuwa ni kauli hii ya Mhe. Naibu Waziri. Mimi kama mwakilishi najua kwamba mawaziri wote haya mambo wala hawayajui, haja yangu ilikuwa ni kwamba atowe kauli ili Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ambaye ni Rais, ajuwe kwamba hao anaowaamini ndio hawa na mwakilishi wake Rais yupo anasikia. Kwa hivyo, nimwambie kwamba hili limetokea kwenye Wizara ya Miundombinu na Mawasilino. Lakini Jumatatu nitampa la wizara yake ambalo linahusika kama hili.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, ikiwa sisi kazi yetu ni kuchuma pesa watu wakawa wanakula tu. Mhe. Mwenyekiti, tuendelee Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo anasikia na naamini mimi atafanyakazi kwa niaba ya Wazanzibari, ahsante tuendelee.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, nilisimama sana katika Idara ya Ujenzi na Utunzaji Barabara lakini sikubahatika, lakini kama kawaida yangu unanijua Mhe. Mwenyekiti, mimi ni mtu wa kuheshimu utaratibu, kwa hivyo sana sikunyanyuka kukukera. Lakini uzuri wa Idara hii ya Uendeshaji na Utumishi hapa ndio pahala ninapoweza kuhoji lolote Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, nilihoji mambo mengi, yale ya vifungu namkubalia Mhe. Omar alivyoniambia asubuhi kwamba nimwachie nisubiri wizara yake atakuja kunieleza. Lakini namwambia atizame mafungu mengi yale namuomba aitafute Hansard yangu, kwa sababu nilitaja kwa orodha vile vifungu, kwa hivyo naliwacha Mhe. Mwenyekiti.

Suala ninalotaka kupatiwa maelezo Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba Idara ya Uendeshaji na Utumishi inaomba fedha hizi ambazo jumla yake ni bilioni 1,279,000,000 kutoka fungu la mwaka jana Mhe. Mwenyekiti, 632,000,000 milioni. Hii ni mara mbili ya bajeti ya mwaka jana, wakati hii sio idara inayofanya shughuli, hii ni idara ya usimamizi na utawala ofisini. Lakini ndio yale tunayosema kwamba fedha kasma imeongezwa, we kabandike pale, wako wale aliyosema Mhe. Hija Hassan, ambao nadhani Mhe. Rais anatusikia kwamba tumechoka kulea watendaji waliokuwa hawaheshimu maadili ya kazi yao, waliokuwa kazi yao ni kutafuna fedha za walipa kodi.

Hoja yangu Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba kwa nini tuidhinishe fedha hizi ikiwa idara hii iko chini ya usimamizi wa Katibu Mkuu na Mkurugenzi muhusika inashindwa kusimamia ipasavyo matumizi ya fedha ambazo tuliziidhinisha kipindi kilichopita.

Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu ya msingi aliigusia kidogo Mhe. Mohamed Said, lakini mimi nitakwenda upande mwengine. Hoja ambayo niliigusa ni ya barabara ya Amani na Mtoni, lakini

mimi niko katika matumizi ya fedha bilioni 1.6 ambazo zilitoka katika Serikali ya Muungano wa Tanzania kuhusiana na ujenzi wa barabara ile.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuthibitisha kwamba hakuna ukweli katika matumizi, hata maelezo ya Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akijibu hoja yangu, nilimsikiliza kwa makini sana, nilikiinamia hiki kipaza sauti. Kama alivyoniambia hapa siku moja Dk. Mwinyihaji kwamba nikiinamie, basi nilikiinamia sana leo ili nimsikie kwa makini. Alichofanya ni kuthibitisha yale matumizi ambayo jana mimi niliyaeleza hapa Mhe. Mwenyekiti. Labda kubwa alichokanusha ni kuhusu kifusi, ambapo bado mimi nathibitisha. Kama alivyosema Mhe. Mwenyekiti, sitaki twende katika kamati teule tu, kwa sababu tutaunda nyingi humu ndani kwa uoza uliokuwemo serikalini.

Mhe. Mwenyekiti, bado nathibitisha hoja yangu kwamba kifusi kilichukuliwa kutoka Kibele na badala yake zikatumika pesa katika mfuko huu. Sasa Mhe. Mwenyekiti, nasema hili linanipa wasi wasi kwa nini tuiidhinishie idara hii ambayo inashindwa kusimamia kazi zake. Mhe. Mwenyekiti, ukitizama kitabu cha bajeti hiki katika barabara hii ya Amani na Mtoni. Naomba nisome kifungu kimoja tu katika ukurasa wa 28.

Mhe. Mwenyekiti, huu ni mradi ambao unaendelea na unalengo la kujenga sehemu ya pili ya barabara ya Amani Mtoni, yenye urefu wa kilomita 4 naomba ni rudie Mhe. Mwenyekiti, kilomita 4. Hatua ya uwekaji kifusi kutoka tabaka la mwanzo na tabaka la pili kwa sehemu kubwa na ujenzi wa ma-*culvert* umefanyika.

Kwa mwaka huu wa fedha 2012/13 wizara inakusudia kuuendeleza mradi huu na hakuna fedha zinazoombwa kutoka mfuko wa serikali kupitia Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, kwa vile ujenzi wake utagharimiwa kwa kupitia mfuko wa barabara. Huu mfuko wa barabara Mhe. Mwenyekiti, bado ni fedha za serikali.

Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu ni kwamba hapa palikuwa na bilioni 1.6. Ili hii hoja yangu ifahamike na Mhe. Mwenyekiti, uifahamu. Naomba nifanye kumbukumbu ya kitabu cha mwaka jana cha hotuba ya waziri, kuna kifungu kimoja tu katika mradi wa ujenzi wa barabara ya Amani Mtoni. Iko katika ukurasa wa 19 kwenye kitabu cha mwaka jana kifungu cha 45, kinasema;

“Mhe. Spika, huu ni mradi unaoendelea wenye lengo la kujenga sehemu ya pili ya barabara ya Amani Mtoni kilomita 4, hatua iliyofikiwa ni kwa ujenzi unaendelea kwa usafishaji na kuweka kifusi ambapo jumla ya kilomita 3 zimekamilika”.

Mhe. Mwenyekiti, nilisema jana kwamba mradi huu hasa ukitizama sio kilomita 4 ni kilomita 3.8. Kwa hivyo, kwenye hotuba ile ya mwaka jana kilomita 3 ilikuwa tayari, bado 0.8 kilomita. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, tunataka kudanganywa kwamba haya ndio matumizi yote tunayohangaishana. Hata Mhe. Naibu Waziri, kakiri mwenyewe hapa katika maelezo yake hapa kwamba lami ambayo ilinunuliwa. Mimi nashangaa MECO ni kampuni binafsi, vipi wizara inunuwe lami kwa fedha hizi halafu ikopeshe MECO. Katuambia hapa kwamba wameshalipa. Mimi ushahidi wangu nilionao ni kwamba mpaka mwezi Machi ilikuwa hata barua kutoka wizarani kudai MECO lami yake ilikuwa hakuna, lakini sitaki kwenda huko.

Hoja yangu Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba kwa hoja hizi, kwa nini idara hii. Pia jana nilizungumza jengine la fidia ambalo nalo lina matatizo yake katika eneo la kiwanja cha ndege. Kwa nini niruhusu na wenzangu turuhusu kuipa mara mbili ya bajeti yake iliyoombwa mwaka jana, wakati usimamizi wa matumizi ya fedha hizi ni mbovu kama nini. Mhe. Mwenyekiti, nataka kutoa hoja, mheshimiwa alisema kama kuna hoja mpya tumsaidie. Hapa mimi nataka kutoa hoja kwamba fungu la Idara ya Uendeshaji na Utumishi, nakubali kuna *inflection*, kuna matumizi lakini kwa sababu hawawi wakweli kutumia hoja *habitual*.

Mimi natoa hoja Mhe. Mwenyekiti, kwamba fungu hili tulipunguze kutoka bilioni 1.2 tuwape za mwaka jana 632,000,000 na nyongeza tuwape ya milioni 300,000,000 Mhe. Mwenyekiti, lakini fedha zilizobakia hapa zipunguzwe katika Idara ya Uendeshaji na Utumishi zikahudumie Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo katika kutafuta meli na mambo mengine.

Mhe. Mwenyekiti, idara hii imeshindwa kazi siwezi kuruhusu kuiidhinishia mara mbili ya fedha zake za mwaka jana, wakati hakuonekani kitu chochote ambacho kinafanyika. Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, naomba nichukuwe nafasi hii kumpongeza kwa dhati kabisa Mhe. Ismail Jussa Ladhu, juu ya *concern* ambayo ameionesha katika idara hii. Ni kweli kwamba ukiangalia idara yetu hii ya utumishi utaona kwamba kuna ongezeko kubwa la gharama, lakini kuna ongezeko ambalo lina msingi ikiwemo suala la ongezeko la mishahara, maposho yale ya idara zote tatu yamewekwa pahala pamoja, huduma za viongozi wakuu wa wizara zimewekwa pahala pamoja, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu wake.

Lakini pia nakubaliana na rai yake ya kusema kwamba kama Baraza litapitia na likiona kwamba kuna kifungu ambacho hakistahiki kukatwa, mimi nimeridhia wafanye hivyo. Lakini msingi mkubwa wa bajeti hii ni kutaka kwamba serikali kwa kupitia wizara yetu husika tuweze kufanyakazi. Kwa hivyo, maamuzi tunayoyafanya tuangalie pande zote mbili, tunachokiamua hapa na athari zake, mimi sikatai. Lakini naomba sana Mhe. Mwenyekiti, tuangalie kama kuna maeneo ambayo tunahisi kwamba hayakukaa vizuri, basi tutumie nafasi hii kufanya marekebisho. Lakini kwa kusema kwamba tukate pande la bajeti katika idara hii, basi tutafanya pahala hata hao viongozi ambao tunasema hawafanyikazi naowa watashindwa na hata hicho kilio cha wananchi kutaka kuona ufanisi wa serikali nao pia utashindwa kupatikana.

Kwa hivyo, nilikuwa naomba sana Mhe. Mwenyekiti, tuangalie yale maeneo ambayo tunahisi kwamba fedha za walipa kodi na fedha za wanyonge wa nchi hii zitakuwa hazitumiki vizuri, nakubaliana twabaan mia kwa mia kwamba tufanye mipango mizuri ambayo italeta tija. Lakini mipango yetu hiyo tusije tukafika pahala tukaiathiri idara na wizara ikashindwa kufanyakazi zake.

Swali la pili Mhe. Mwenyekiti, lilikuwa linahusu suala la mradi wa barabara ya Amani Mtoni, au Mkapa road. Barabara hii ni kweli kwamba mwaka jana tuliahidi na tukafanyakazi, mapungufu yake yameonekana yametokea wapi, tumejenga hoja serikalini na serikali imetuelewa na ndio maana yakaja maamuzi kwa kuona kwamba matumizi ya fedha ambazo tulikuwa tumeziomba, tumezitumia zimeishia wapi na serikali ikawa imeridhika ndio ikafanya maamuzi ya kuiomba

taasisi husika ya mfuko wa barabara kuweza kumalizia fedha zilizoombwa ili kukamilisha zoezi hilo.

Kwa hivyo, nilikuwa naomba sana Mhe. Mwakilishi akubaliane na rai yetu, waturuhusu tupitishe bajeti, ili tuwaruhusu wenzetu wa mfuko wa barabara wapitishiwe bajeti yao ili tupate fedha hizo tukakamilishe mradi huu. Sasa ikiwa tutapata fedha hizo halafu mradi haukukamilika, basi wanayo haki na kila sababu ya kutuhoji juu ya uaminifu na utendaji kazi wa taasisi hiyo. Lakini bila ya kutupa fedha basi wasitarajie kama barabara ile itakamilika na bila ya kukamilika barabara ile, ina maana hata kile ambacho tumekitumia hakioneshi tija, kwa sababu yale malengo ambayo yamekusudiwa na serikali yatashindwa kufikiwa.

Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Ismail Jussa Ladhu, Mwakilishi wa Wananchi wa Jimbo la Mji Mkongwe, atumie busara zake, hekima zake, uadilifu wake na uungwana wake ili aturuhusu tuendelee na bajeti yetu na kama kuna *concern* nyengine ya kufanya masahihisho, basi tunakubaliana naye mia fil mia.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nia yetu siku zote sisi ni kusaidia, lakini nia yetu kubwa kabisa iliyotuleta hapa ni kutekeleza kazi zetu tulizojiundia katiba kuchunga fedha za wananchi maskini wa Zanzibar, wanaokwenda hospitali wakaambiwa dawa hazitimii kwa sababu serikali haina fedha, wanaowapeleka watoto wao maskuli wakashindwa kukaa juu ya ma-*desk*, kwa sababu wanaambiwa serikali haina pesa, wanaoshindwa kupata maji safi na salama kwa sababu wanaambiwa serikali haina pesa na kadhalika, na orodha inaendelea ya vitu vingi tu. Kumbe fedha zipo zinatafunwa na watendaji wetu wasiokuwa waaminifu Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, bahati nzuri katika kunijibu kazizungumza hoja zote mbili na mimi naomba nizizungumze hoja zote mbili, halafu nitowe ninachodhani mimi kama itakuwa ni sawa. Mhe. Mwenyekiti, nilisema hapa. Hili Mhe. Mwenyekiti, halimalizikii hapa tu, nitaingia leo mpaka kwenye fedha za maendeleo katika miradi ya ujenzi wa barabara, kwa sababu huu ni mfano dhahiri uliokuwepo hapa. Kwa sababu jana nilipochangia nilichangia kwa ujumla wake nikatoa mfano wa barabara hii Mhe. Mwenyekiti, kwamba haiwezekani kwamba fedha hizi asilimia 30 ya fedha iliyoletwa ikaambiwa itumike katika matengenezo ya magari na vifaa vyengine vilivyokuwa vimetumika.

Mhe. Mwenyekiti, kama hawajui, nawaambia Mhe. Waziri na Naibu wake wakaangalie hili katika pahala ambapo wanatafunwa pesa zao nyingi tunazowaidhinishia hapa katika idara hii ni kila bajeti ya ujenzi wa barabara. Kila bajeti ya ujenzi wa barabara mpya inayokuja, asilimia 30 mpaka asilimia 40 Mhe. Mwenyekiti, ni matengenezo ya vifaa na wakaangalie wataenda kuyaona.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, huu ni mfano tu shilingi milioni 406,000,000 jumlisha na shilingi milioni 91,000,000 wanazolipana wakubwa juu hapo maposho yao kwa kutengeneza barabara. Zaidi ya shilingi milioni 500,000,000 katika bilioni 1.6 takriban theluthi nzima ya pesa iliyoletwa imeliwa na wajanja wachache Mhe. Mwenyekiti, kwa kuburutana kwa mwaka mzima kwa 0.8 kilomita palipobakia Mhe. Mwenyekiti. Tunachezea pesa. Hata kama zimetoka katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano Mhe. Mwenyekiti, lakini hizi zimeletwa kwa wananchi wa Zanzibar.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, nasema nilipotoa hoja hapa zipunguzwe. Mimi nimemsikia hoja yaka hapa kwamba tuangalie ongezeko la mishahara. Hii nimeitolea mfano tu wa usimamizi mbovu wa matumizi ya fedha tunazoziidhinisha na wanazopewa wizaa hii Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, nikiangalia ili unielewe na anielewe Mhe. Waziri na Naibu wake. Fungu la Mishahara Mhe. Mwenyekiti, utalitazama hapo limetoka shilingi milioni 318,000,000 limekuja shilingi milioni 566,000,000. Lakini kuna posho maalum hapo shilingi milioni 181,000,000, kuna malipo ya kujikimu na malazi shilingi milioni 16,000,000. Huku kuna fungu Mhe. Mwenyekiti, la safari. Hizi za kujikimu tu shilingi milioni 16,000,000. Kuna posho la vikao na kamati 48,000,000, kuna kodi ya nyumba hii nilidhani labda tulikuwa tunadai walipwe wale nyumba ya wakfu waliokuwa wamechukua labda ndio hiyo nilikuta shilingi milioni 54,000,000. Lakini ukenda katika viburudishaji Mhe. Mwenyekiti, ilitoka shilingi milioni 8,000,000 na mwaka huu milioni 15,000,000, ukienda katika gharama za safari ilikuwa milioni 41,000,000 mwaka jana na mwaka huu milioni 78,000,000.

Hizi zote Mhe. Mwenyekiti, ni za kupungua. *Stationary* imepandishwa mara mbili kutoka milioni 12,000,000 imekuwa milioni 25,000,000 mwaka huu, uimarishaji wa mpango wa bajeti ulipunguzwa, ulikuwa umeongezeka ukapunguzwa. Lakini kuna matengenezo madogo ya ofisi milioni 41,000,000, matengenezo madogo tu hayo milioni 41,950,000, kuna gharama za mafunzo Mhe. Mwenyekiti, milioni 26,300,000, kutoka milioni 16,000,000 mwaka jana, kuna ununuzi wa vifaa kule imetoka milioni 7,000,000 mwaka jana na mwaka huu milioni 19,000,000.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, bado yako maeneo makubwa katika idara hii ya kukatwa. Labda kwa sababu sitaki kulifikisha Baraza katika kamati hii, likafika pahala tupitie fungu moja moja, tukasema tukate kiasi gani. Mimi nilisema kwa sababu hawawi wasikivu kwa mawaziri wetu pia tukiwatetea sisi wanatuona sisi ndio wabaya wao na wanaendelea kuwatetea watendaji wao, basi ndio nikasema tutumie *rule* ya *habitual* kwamba tukate tu kiasi kadhaa au milioni 300,000,000 tupunguze, ndio unaotumika utaratibu huu.

Mhe. Mwenyekiti, nasema tena na bahati nzuri serikali hii ina mtu ambaye mimi namuheshimu, ambaye ni Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Sasa kwa sababu mwisho wa hadithi itakuja kwake na asubuhi katuambia kwamba katika wizara yake ikifika atakuja kuonesha ni maeneo gani kayakata. Mimi namuomba Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendele, ambaye katika wizara hii, mbali kwa mawaziri wote ambao wanamuwakilisha Rais katika dhamana zao, lakini kwa yeye hii ndiye waziri wa nchi ndiye anayemwakilisha Rais hasa katika wizara nyeti kabisa.

Kwa hivyo, naomba hili wakalitazame halafu wakalifanyie kazi. Mimi siridhiki kwamba fedha zilizokuwa zimeidhinishwa kwa ujumla wake, nitakuja idara nyengine bilioni 500, zitakuwa zinahitajika, hizi fedha zitakwenda kuliwa, mimi siwezi kukubali. Kwa hivyo, nataka nikubali tuendelee kwa hoja moja tu, kwamba Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais atakwenda kukaa na wenzake ili waone mafungu haya na mengine ni kiasi gani yanapunguzwa ili wizi uliotopea katika Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ukomeshwe. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, tuendelee. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, mimi nimemsikiliza kwa vizuri sana nasema siku zote Mhe. Mwakilishi wangu wa Jimbo langu la Mji Mkongwe, Mhe. Ismail Jussa Ladhu. Mhe. Mwenyekiti, nataka nirejee yale niliyoyasema asubuhi, kwamba nataka aniamini. Vifungu hivyo wamenionesha wao na nimevitaja vifungu 19. Narudia vifungu 19 na hivyo vifungu 19 miongoni mwao amevitaja asubuhi na vyengine amevitaja sasa hivi. Vifungu hivi vyote 19 tumeviangalia kwa kina. Nataka niwaambie vyengine tumevipunguzia kuanzia asilimia 20 na vyengine mpaka asilimia 75. Tumeona uzito wa ujazo wa vile vifungu, tumeona na sababu za msingi za kujazwa vile vifungu hazipo tumevipunguzia mpaka asilimia 75.

Kwa hivyo, nataka niwaahidi Waheshimiwa Wajumbe, kwamba nitaleta orodha hapa siku nitakaposoma bajeti yangu, wataviona vifungu vyenyewe na kila kifungu wataona ni asilimia ngapi nimevipunguza ili fedha hizo, mwanzo nilisema zitakwenda katika huduma ambazo zinahitajia fedha. Lakini namshukuru sana Mhe. Rais amenipa kazi wiki moja nitowe fedha, nitatoa wapi fedha za kununulia meli basi eneo moja ni hili ambalo Waheshimiwa Wawakilishi wamenisaidia. Ndio maana asubuhi kabla ya swalat Ijumaa nilisema kuna vifungu jamani buti tupunguze, kwa sababu tayari nimeshavifanyia kazi, tupigeni buti kwenye vifungu vyengine.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Ismail Jussa, mawazo yake vile vile. Idara hizi za utumishi na uendeshaji ni idara muhimu na idara hizi ndio kiungo cha katibu mkuu na idara nyengine ndani ya wizara. Idara hizi zikiwa legelege basi wizara nzima itakuwa legelege, idara hizi zikiwa *corrupt* basi wizara nzima itakuwa *corrupt*. Kwa hivyo, mimi nasema kwamba idara hizi na hasa nawasisitiza mawaziri wenzangu kwamba idara hizi tuzitupie macho kweli kweli ili hapa tunasakamwa sisi. Namuomba sana Mhe. Mwakilishi wangu aturuhusu basi hii idara ipite halafu atakuja kuona mwenyewe, nitaleta hapa orodha ya wizara kwa wizara baadae, wataona kila wizara kazi hiyo tumeshaifanya, kila wizara wataona tunatoa kiasi gani na tunazipeleka katika maeneo ambayo tunayahitajia.

Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Mji Mkongwe aruhusu hiki kifungu kipite ili kumruhusu Mhe. Rashid Suleiman Waziri wetu mpya wa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano aweze kufanyakazi na kusaidiana na Baraza lako tukufu. Mhe. Mwenyekiti, yangu ndio hayo namuomba sana Mhe. Mwakilishi aturuhusu tuendelee.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nimeshatoa idhini kabla hajanipa mkono, tuendelee tu Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia nilizungumza maslahi ya wafanyakazi wetu wa *Signal Tower* wanaoongoza minara, siku za sikukuu huwa hawapati haki zao ni hilo tu dogo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, *concern* ya Mhe. Mjumbe tumeielewa, naomba nimuhakikishie kwamba sio katika eneo hilo tu la *signal tower*, lakini wafanyakazi wote wa Shirika la Bandari utaratibu wa mapato yao, maposho na mafao mengine yote yanayostahiki watapewa baada ya kuimarishwa na kuwa mazuri zaidi, kama vile *management* ya wizara tumeagiza shirika kwa kupitia bodi na bodi imekubali, kwa hivyo ni imani yetu kwamba utekelezaji wa jambo hili utaanza mara baada ya hao wenyewe kuendelea na

mchakato wao wa utaratibu wa uongozi wa shirika. Kwa maana kwamba mafao ya *signal tower* na mafao ya wafanyakazi wengine wa Shirika la Bandari wote watakuwa wamezingatiwa, katika kuona ile azma ya vikao vyetu na maafikiano yetu ya uongozi wa wizara na watendaji wa Shirika la Bandari yatakuwa yamezingatiwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, mimi nimeshazowea kusikia mara tu au wakati wowote. Lakini mimi nataka anipe muda ni muda gani, kama kesho au keshokutwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, utaratibu tunaouzungumza hapa ni utaratibu wa serikali, kwa maana kwamba sisi wizara tumezungumza na utendaji na viongozi wa Shirika la Bandari. Shirika la Bandari wamekubaliana katika bodi yao, maamuzi na mapendekezo ambayo tumewapa wameyakubali, kilichopo ni utekelezaji.

Kwa hivyo, ninachomuhakikishia Mhe. Mwakilishi ni kwamba katika bajeti hii suala la utekelezaji huu litaanza na miongoni mwa mambo ambayo tumekubaliana ni suala la posho kwa kipindi hiki cha Ramadhani na skukuu na wamesema watatekeleza. Pia suala la *bonus* wameshaanza kulitekeleza kwa wafanyakazi wetu hao.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Sawa Mhe. Mwenyekiti, naomba tuendelee.

Kifungu 0901 Idara ya Uendeshaji na Utumishi 1,279,000,000

Kifungu 1001

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa najaribu kuangalia baada ya kunibana kwa muda mrefu wapi nitaweza kupata nafasi. Kwanza Mhe. Mwenyekiti, nataka nimshukuru sana Mhe. Mwanasheria Mkuu na mwanzo inaonesha walikuwa hawatuelewi, wanatuona wakorofi. Lakini tunashukuru katika maoni tuliyokuwa tukiyatoa mbali mbali niliona barua yake, ambayo ni ya utekelezaji wa haya ambayo tunayoyafanya hapa, hivyo tunakushukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nipate maelezo, lakini kabla ya kupata maelezo nataka nimshukuru sana Mhe. Waziri pale alipozishukuru Ripoti za Kamati Teule katika hotuba yake. Vile vile leo wakati alipokuwa akitoa maelezo alitaja majina ya manabii, maswahaba, tunamshukuru sana kwamba anajua kwamba yale majina hayafanyi kazi hivi hivi tu. Mimi nashukuru kwamba katika wale maswahaba basi na Hamza yumo na miwani leo nimeisahau. *(Makofi)*

Lakini Mhe. Mwenyekiti ninavyojua mimi kwa sisi mashehe tunasema kwamba wale wanaopigana Vita vya Jihadi hawafi wanabakia shahidi, sasa Hamza amekufa, lakini yuhai. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti nataka kumwambia kwamba sisi tutamsaidia na tunaamini kuwa atafanikiwa. *(Kicheko/Makofi)*

Baada ya hayo mimi nataka nianze na ushauri kwanza. Kwa kweli sisi tunayo nia kubwa sana ya kumsaidia Mhe. Waziri pamoja na wizara nzima, kama alivyotaja yale majina matukufu pale

asubuhi, basi na sisi tunaomba atusikilize ushauri wetu. Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Mhe. Waziri anayo kazi kubwa sana na kitu ambacho tunachomuomba hasa kwa upande wa Mamlaka ya Anga nafikiri kuna haja ya kufanya marekebisho makubwa na hii hoja yangu ambayo nitakayokuja nayo hivi sasa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nimekamata katika Idara ya Mawasiliano, najua kwamba idara hii nadhani na Mamlaka itakuwa inaingia. Mhe. Mwenyekiti, kuna tatizo kubwa la utawala na hata hili suala ambalo waliokuwa wanajibizana baina Mwanasheria Mkuu na Maalim Saleh ukija kuangalia chanzo ni hii mamlaka yenyewe inaichanganya Serikali na wala sio hili tu. Vile vile kuna yule mzee niliyemtaka wakati nilipokuwa nikipeleka mchango wangu kwa maandishi Mwinyichande.

Mhe. Mwenyekiti, tulipokwenda kwenye Ripoti ya Kamati Teule basi yule Mzee tulikwenda tukaikuta nyumba yake imo ndani ya Uwanja wa Ndege na nyumba ile ipo muda mrefu sana zaidi ya karibu si chini ya miaka 40 au 50 iliyopita, yaani pale wako asili na hapa Mhe. Waziri ametuambia ameshalipwa.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, kima alicholipwa ni shilingi milioni 35,000,000/= na sisi ile nyumba tulikwenda kuangalia kwa wakati wa hivi sasa na sisi tulipendekeza tena tulikuwa pamoja, kwamba huyu mzee hii nyumba yake nadhani thamani yake, ili aweze kuondoka hapa apate sehemu nyengine astirike basi angalau si chini ya shilingi milioni 100.

Sasa nadhani wangelichukua asilimia 75, lakini wamekwenda kumlipa shilingi milioni 34 au 36 na tulipoangalia orodha ya watu wengine waliolipwa Mhe. Mwenyekiti kuna watu wengine orodha aliyoitaja jana Mhe. Ismail Jussa Ladhu sijui kama itakuwa Mhe. Waziri ameitolea ufafanuzi, kwamba kuna watu wamefanyiwa makisio walipwe karibu shilingi milioni 60 na zaidi, ambapo hata maeneo yakulipwa hawana.

Jambo jengine Mhe. Mwenyekiti, viongozi wamekwenda katika matatizo ya uwanja wa Ndege na suala la ulipaji wa fidia. Mhe. Mwenyekiti, kuna agizo lilitolewa kwamba Mamlaka wakae na wale wananchi, ili angalau kutoa mwelekeo na kitu hicho bado hakijafanyika. Sasa hili ni tatizo la utawala Mhe. Mwenyekiti na tutakuja kusokotana. *(Makofi)*

Kwa hivyo, mimi namuomba Mhe. Waziri na mwenzake ameondoka kwa Mamlaka ya Usafiri wa Baharini na yeye atakuja kuondoka kwa Mamlaka ya Usafiri wa Angani. Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri aangalie Ripoti ya Meli ya MV. Fatih halafu aisome tena yote na wala asiibakishe, pia Ripoti ya Meli ya MV. *Spice Islander* aangalie ukurasa wa 95 unasemaje, maana na yeye asijekusema amejiuzulu mwenyewe. Lakini Ripoti ya Meli ya MV. *Spice Islander* Ripoti ya Kamati ya Rais ukurasa wa 95 inasema na Mhe. Mwenyekiti naomba kunukuu kidogo.

> Ripoti ya Kamati ya Rais kuhusu Meli ya MV. *Spice Islander* ukurasa wa 95 unaeleza hivi:-
>
> > “Kwa upande wa wanasiasa katika nchi za Jumuia ya Madola waziri anatakiwa awajibike kwa matendo waliyofanya watendaji wake aidha kwa makusudi au kwa bahati mbaya”.

Mhe. Mwenyekiti, ile ni Ripoti ya Rais na sio maneno yangu mimi. Kwa kweli Mamlaka ya Anga kuna tatizo Mhe. Mwenyekiti. Kwa hivyo, hivi sasa ule uwanja bora ubadilishwe jina na wala usiitwe Abeid Amani Karume tunamtia aibu, wanadhalilishwa mpaka Mabalozi, yaani gari ya Balozi leo inafungwa tairi.

Kwa mfano, Balozi aliyepelekwa Misri Balozi Moh'd Hamza pale alikwenda na gari yake anatokea kijana pale haraka anamwambia toa gari nje, ni aibu Mhe. Mwenyekiti ule uwanja ubadilishwe jina badala ya kuitwa Abeid Amani Karume uitwe jina la huyu Mkurugenzi wa Mamlaka aliyekuwepo hivi sasa. Mhe. Mwenyekiti, naomba maelezo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, nimemsikiliza kwa makini sana Mhe. Hamza Hassan Juma na nadhani mambo aliyoeleza yana msingi mkubwa. Sasa amegusia suala la fidia ya nyumba. Naomba suala hili ni vyema tukaona limemalizika na naomba iwe hivyo kwa sababu sisi kama Wizara tulipatiwa maelekezo na taasisi za Serikali ambao walifanya tathmini na wajibu wetu sisi ilikuwa ni kulipa fidia na tumekamilisha wajibu wetu.

Sasa kama kiwango kilikuwa kidogo hii ni *concern* mpya tunaweza tukaipokea, lakini kwa kushauriana na hao ambao walifanya tathmini kuona namna gani kama kuna uwezekano wa kumsaidia basi iweze kufanyika hivyo.

Jambo jengine amezungumza kwa sehemu kubwa sana juu ya suala la utendaji, mapungufu, kadhia, matatizo, dharau, ubabe unaotokea *Airport*. Mhe. Mwenyekiti, napenda kumhakikishia Mhe. Mwakilishi pamoja na Baraza lako kwa jumla kwamba tumeyasikia sisi kama viongozi tutakaa na wahusika, ili kuweza kuwaambia kwamba utaratibu wa nchi hii watu huheshimiana, kuelekezana, kukosoana pamoja na kuambizana. Imani yetu kwamba watendaji kazi wetu hawa ni watu wazima, hivyo watafahamu *concern* ya Serikali na *twabaan* maelekezo hayo yatawarejesha kwenye mstari. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mategemeo yetu ni kwamba kama kutakuwa na sababu ya mapungufu ya kiutendaji hasa masuala ya nidhamu basi hilo litakaa sawa. Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Hamza Hassan Juma atuunge mkono na tupitishiwe bajeti yetu, sisi na wewe ni kiongozi tutawaita hao watendaji na kuwaelekeza na kurudi kwenye mstari, ili kujenga haiba na uungwana wa kizanzibari kwamba Uwanja wa Ndege ndio taaswira ya nchi yetu na wala si jambo zuri kwamba wageni wanaokuja pale wakawa wanapokewa kwa viroja na vituko. *(Makofi)*

Kwa kweli wageni wanaokuja pale wanataka kupokewa kwa lugha pamoja na tabia nzuri ya kizanzibari. Hata hivyo, wale wananachi wetu wanaokwenda katika maeneo yale wanahitaji kuheshimiwa nalo hilo pia tutalifanyia kazi. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, namuomba sana Mhe. Mwakilishi ajenge imani kwamba suala hili sisi, yeye pamoja na viongozi wengine wowote wa Barazani humu tutakaa na watendaji wetu, kwa ajili ya kuwaelekeza na warudi katika mstari. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, maelezo ya ziada.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo mazuri ya Mhe. Naibu Waziri ningependa niseme maelezo yafuatayo. Lakini kwanza nataka niwashukuru sana Wajumbe wa Baraza hili la Wawakilishi waliotoa maelezo ya kina, ili kuonekana nidhamu ya matumizi ya fedha za Serikali zitumike kwa uadilifu mkubwa, nawashukuru sana.

Vile vile nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe kwa kuonesha kila ambapo pana kasoro, ili pasawazishwe. Mhe. Mwenyekiti, nataka nilihakikishie Baraza lako Tukufu kwamba huo ndio unakuwa mwenendo wetu, Serikali hii ni sikivu yale wanayoyasema Waheshimiwa Wawakilishi ndio mwisho wa siku tunayachukua na kwenda kuyafanyiakazi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sasa inatubidi tufanye juhudi zaidi, ili kila pale ambapo pamejitokeza kasoro, basi kasoro hizo zirekebishwe, ili Waheshimiwa Wawakilishi waridhike pamoja na wananchi wetu waridhike, maana nia ya Serikali hii ni kuwatumikia wananchi kwa uadilifu na kila chao kitumike kwa utaratibu ulio mzuri.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti kama kumetokea jambo hasa la Balozi zetu kupata usumbufu pale *Airport*, kwanza ningependa niombe radhi sana kwa niaba ya Serikali kwa kitendo hicho. Lakini tutawahakikishia ndugu zetu hawa Mabalozi waliopo hapa Zanzibar na kwengine kwamba jambo kama hilo halitotokezea tena katika *Airport* yetu na vijana waliofanya hivyo tutawashughulikia kwa mujibu wa taratibu zetu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, lazima heshima iendelee kuwepo hasa kwa viongozi wetu hawa ambao wameletwa na nchi zao kuja kutumikia nchi zao wakiwepo hapa kwa mashirikiano mazuri ya mahusiano.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Hamza Hassan Juma pamoja na Waheshimiwa Wawakilishi kwamba watukubalie na yale yote ambayo wameyaona ni mapungufu Serikali imeyasikiliza kwa makini na itayafanyiakazi na kila mtendaji ambaye anayeonekana na kasoro basi hatua za kinidhamu zitachukuliwa, ili kuondosha uoza katika serikali yetu na wala hatutamuogopa mtendaji yeyote. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, kila aliyefanyakazi na kutumia vibaya fedha za Serikali au madaraka yao, pia wale wanaotumia vibaya wajibu waliopewa na Serikali basi wote tutawashulikia na mtaona matokeo yake. Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, naendelea kutoa shukurani sana kwa Serikali yetu imeanza kuturidhisha kwa baadhi ya hoja zetu. Sasa haja yangu Mhe. Mwenyekiti, kabla sijakaa kitako namuomba sana Mhe. Waziri, katika mtu aliyekuwa anamsumbua Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali alikuwa ni Mhe. Rashid Seif Suleiman ambaye hivi sasa ni Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, tokea tuko Kikwajuni Baraza lako la zamani kabla hatujaja hili hapa alikuwa akisisitiza *post* hizi tunazozitengeneza katika sheria lazima sifa zinatakiwa ziheshimiwe. Sasa Mhe. Mwenyekiti, ndio maana nikamwambia na hili pia namuomba sana Mhe. Mwanasheria

Mkuu, kwamba Sheria tuliyoipitisha Nam. 8 mwaka 2011 ya Mamlaka ya Anga, Mhe. Mwenyekiti tulitumia zaidi ubinafsi na wala hatukuangalia sifa.

Mhe. Mwenyekiti, katika ile sheria inaeleza pale kwamba Mkurugenzi wa Mamlaka anatakiwa awe na sifa fulani, sasa leo tukaja tukasema hii maana yake kwa kuwa anao uzoefu wa hivi na vile na tukaacha *CV* iliyokuwemo kwenye sheria na tukatafuta uzoefu ambao hauko katika sheria na matokezeo yake ndio haya. *(Makofi)*

Kwa mfano, tukiangalia katika Ripoti ya Kamati Teule kuna mambo ambayo hata watoto wadogo hawawezi kufanya na leo yanaendelea kuliko yale. Mhe. Mwenyekiti, tunawaamini na Waheshimiwa Mawaziri na sasa tunasubiri utekelezaji. Mhe. Mwenyekiti, tuendelee. *(Makofi)*

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, mimi naamini kwanza kwamba baada ya uchambuzi ambao Waheshimiwa Wajumbe wameufanya tokea juzi mpaka leo, mwenye mamlaka ya uteuzi ametusikia na mimi naamini atakisikia kilio chetu na atavunja Wizara hii aiunde upya yote kuanzia Katibu Mkuu mpaka Wakurugenzi wote. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu ni Idara ya Mawasiliano wakati nilipokuwa nikichangia nilimuomba Mhe. Waziri atakapokuja anisaidie Zanzibar inavyofaidika na mapato yanayotoka katika zile Mamlaka za Kimuungano na kwa hapa nimezitaja tano.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, mimi ni mtu wa kuheshimu taratibu na hapa nazitaja tano kwa sababu ndizo zinazohusika na mawasiliano na zile mbili kwa sababu idara yake imeshapita naziacha haidhuru nazo natafautiana na Mhe. Naibu Waziri kwamba nazo zinaingiza mapato pia. Kwa mfano, Mamlaka inayosimamia *Civil Aviation* wanaotumia anga wanalipa Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo mapato yapo, lakini hizo naziacha kwa sababu haheshimu taratibu na sio idara yake.

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Mawasiliano katika hotuba ya Mhe. Waziri ukusara wa 57 imetaja mamlaka tatu katika idara hii Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TCRA*), Shirika la Simu Tanzania (*TTCL*) na Shirika la Posta Tanzania (*TPC*). Sasa nilimsikiliza Mhe. Naibu Waziri hoja alizonijibu, lakini la msingi sikulipata kwa sababu nilitaka nisaidiwe ndivyo nilivyotaka maelezo, tunapata kiasi gani?

Kwa hivyo, kama kawaida Mhe. Mwenyekiti tumepata maneno, yaani kama kawaida ya taasisi zote za ndugu zetu wa damu tunapigwa maneno mpaka wengine wanasema waachiwe wapumue, maana yake wameshachoka na maneno. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba hili najua hivi sasa pengine hawezi kunisaidia, lakini nataka Mhe. Naibu Waziri aniambie. Kwa mfano, mimi naelewa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TCRA*) inapata mapato mengi sana, kwa sababu makampuni yote ya simu na katika biashara kubwa hivi sasa Tanzania moja wapo ni biashara ya simu.

Mhe. Omar Yussuf Mzee alikuwa Naibu Waziri wa Fedha anajua, katika watu ambao wanachangia ukuaji wa uchumi wa Tanzania moja ni sekta hii ya simu alitwambia wakati alipokuwa Bungeni kipindi kile.

Kwa hivyo, kuna simu Mhe. Mwenyekiti, pia kuna usajili wa Vituo vya *Television* na *Radio* zote unazozijua za *FM* na nyengine mbali ya mambo mengine, hivyo kuna mapato mengi.

Lakini kwenye Simu na Posta Mhe. Mwenyekiti kama nilivyosema sisi tulikuwa na hisa na baadaye kwa mfano suala la *TTCL* likauza hisa zake na kuunga ile Kampuni ya *Celtel* na baadaye ikaunda ikawa *Zain* na baada ya *Zain* imekuja *Airtel*, Mhe. Mwenyekiti hapa wenzetu wamepata mapato.

Vile vile hata kwenye Posta Mhe. Mwenyekiti, mimi ninao ushahidi wa *stamp*, kwamba pamoja na suala la Posta kuingizwa katika mambo ya Muungano awali kabisa katika yale mambo 11 yale ya asili, haidhuru juzi Mhe. Mwanasheria Mkuu alitusaidia akatuambia sio mambo 11 ni kontena 11 na ninashukuru kwa kutusaidia ile istilahi nzuri. Sasa Posta Mhe. Mwenyekiti, ilikuwemo lakini Zanzibar inaendelea kutoa *stamp* zake kwa muda mrefu baada ya Posta kuingizwa katika mambo ya Muungano.

Kwa hivyo, nilikuwa nataka hili Mhe. Waziri anisaidie, kama hana takwimu hivi sasa badi mimi naomba nitoe fursa tu kwamba kikao kijacho cha Baraza lako Mhe. Mwenyekiti, basi Mhe. Waziri afanye utafiti na aje atutajie mapato ya mamlaka hizi kila moja ni kiasi gani kwa Tanzania nzima na sisi tulipaswa tupate kiasi gani aje atuletee katika kikao kijacho na nimuombe hilo tu Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Kwa kweli najua kwa hivi sasa nitamuhangaisha bure na kutaabishana bure, yeye na mimi tuko damu moja hapa na sote wazanzibari hapa, tunanyonywa na ndugu zetu wa damu kama anavyonyonywa mtu mwengine yeyote Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo nataka hili anisaidie akafanye kazi kikao kijacho aje atuletee. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TPC*), (*TCRA*) na haya mengine niliyoyataja yote akatufanyie utafiti na baadaye aje atuambie yanaingiza kiasi gani na kiasi gani kilipaswa kiwe cha Zanzibar, tukija tukijaaliwa Kikao cha mwezi wa Oktoba aje atuambie, ili hapo Mhe. Mwenyekiti tutajua maamuzi gani ya kufanya. Mhe. Mwenyekiti, naomba hilo tu kwa Mhe. Waziri na Mhe. Mwenyekiti nakushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, *concern* ya Mhe. Mjumbe tumeisikia na ninachoweza kumuahidi ni kwamba sisi kama Wizara ya kisekta tutalifuatilia suala hilo katika taasisi husika na tunamuahidi katika kikao kijacho cha mwezi wa Oktoba Mwenyezi Mungu akitujaalia tutamletea taarifa hizo kwa maandishi. *(Makofi)*

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru na kama nilivyosema hapo atakapotuletea taarifa yake na naomba isije kama kauli ikawa hatuwezi kuijadili, isipokuwa ije kama Taarifa ya Serikali kwa mujibu wa Kanuni zetu na tuweze kuichangia na tuone mapato ya taasisi hizi ni kiasi gani na sisi tunakosa kiasi gani na wakati huo ukifika tutafanya maamuzi nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti na naomba tuendelee. *(Makofi)*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, tuko katika Kifungu cha Idara ya Mawasiliano na wakati nilipokuwa nikichangia kuhusu Mnara wa *Signal Tower* nilisema kwamba

mawasiliano hakuna na hichi kitengo ni muhimu kuhusu mawasiliano hasa kwa wakati wetu huu wa hivi sasa. Je, wizara imeshindwa kupeleka mawasiliano kule?

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, katika shughuli za utendaji kazi wa kawaida Shirika la Bandari linalazimika kuwa na maeneo ya njia za mfumo wa mawasiliano, ili kuweza kukidhi kuweza kuwasiliana na vyombo mbali mbali vinavyoingia na kutoka katika eneo la bandari.

Katika eneo la Mnara wa Beit-el-Ajab eneo la juu tumeweza kukodishwa na wenzetu wa Mji Mkongwe, kwa ajili ya kupata huduma ya kuweka *Signal Tower*. Kwa hivyo, ni kweli kwamba katika eneo lile kule juu kuna chombo chetu maalum kinachotumika kwa lengo la mawasiliano kwa vyombo mbali mbali vya kimawasiliano hasa katika shughuli za usafiri. *(Makofi)*

Lakini suala analolisema Mhe. Mjumbe anaulizia kuhusu simu ya *TTCL* katika eneo lile. Mhe. Mwenyekiti, sote ni mashahidi kwamba matumizi ya simu hivi sasa yametanuka wigo na twabaani matumizi makubwa hivi sasa yamekuwa katika simu za mkononi. Kwa hivyo, matumizi ya simu yanayotumika kule kwa watendaji kazi wetu ni kwa ajili ya huduma za mkononi na simu ya *TTCL* kweli haitumiki kutoa huduma kule. *(Makofi)*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, hiyo simu iliyokuwepo kutizamika haitizamiki tena ni ya mtu binafsi tu, yaani kwa ufupi mawasiliano hakuna na hichi kitengo ni muhimu Mhe. Mwenyekiti, linapotokea jambo lolote na Mwenyezi Mungu asijekujaalia kutokea kitu cha mwanzo ni *Signal Tower* kwa lengo la kutoa taarifa, sasa ikawa hakuna mawasiliano hivi ndio tunakwenda au tunarudi Mhe. Naibu Waziri ni kitu kidogo tu hichi.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, kitu muhimu katika eneo hilo analolizungumza Mhe. Mwakilishi ni ile mashine ya *Maritime Distance Signal*, ambacho chombo hicho kipo na kinafanyakazi.

Suala la simu tumesema matumizi makubwa ya simu hivi sasa yameondoka katika simu za *landline* ya *TTCL* na matumizi makubwa ya wananchi wetu wanatumia simu za mkononi. Kwa hiyo, ukitaka mawasiliano kwa njia ya simu ya mkononi unapata kwa watendaji kazi wote walioko kule wanazo simu zao za mkononi. Lakini unapohitaji mawasiliano kwa njia za mawasiliano kwa vyombo vya usafiri unatumia *Maritime Distance Signal* ambacho ndicho chombo kinachohusika na taratibu za usafiri kwa vyombo vya baharini.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, anachokizungumza Mhe. Naibu Waziri hakiingii kichwani na wala mtu hawezi kufahamu ni kitu rahisi tu. Kwa kweli yule mtu analia na posho zake na simu aliyokuwa nayo mkononi wakati mwengine hata hawezi kupiga *missing call* limetokea tatizo atasema vipi, kwa sababu wao wanalia na posho yao Mhe. Mwenyekiti na bado anakuja kutujibu hivyo Mhe. Naibu Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, hichi ni kitu kidogo tu Mhe. Naibu Waziri na huu ni Mwezi wa Ramadhani tuwe wazi, yaani wale hali zao ni dhiki *hoi bin taabani* leo unategemea watapiga simu zao za mkononi kwa ajili ya kuwasiliana na mtu na wengine hawajui kile chombo ni muhimu namba

zake zikawekwa wazi inapotokezea dharura wakawasiliana. Mhe. Mwenyekiti, sijui Mhe. Naibu Waziri ananijibu kitu gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, nadhani kabla ya hoja hii Mhe. Jaku Hashim Ayoub aliulizia suala la mafao na tumemuahidi kwamba tayari tumeshawaelekeza wenzetu wa Shirika la Bandari kwa ajili ya kurekebisha mafao. Vile vile kama kuna tatizo la posho kwa ajili ya mawasiliano ya watu wetu wanaokaa katika *Signal Tower* basi tutalifanyiakazi na watapatiwa hilo posho, ili kuleta ufanisi katika shughuli zao za kazi. *(Makofi)*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, sikuuliza habari ya posho hivi sasa na posho tumeshafunga ukurasa ule, isipokuwa nimeuliza kuhusu mawasiliano na kama hapana uwezo basi mimi Mhe. Mwenyekiti, nitamkabidhi Mhe. Naibu Waziri japo simu tatu na wala si tatizo kuitumikia Serikali yangu.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, tumesikia *concern* ya Mhe. Jaku Hashim Ayoub tokea ya hali ya mahala palivyo kwenye *Signal Tower*, huduma zake na mawasiliano yanayotakiwa. Kwa hivyo, nachukua ahadi kwamba ndani ya kipindi cha miezi sita inayokuja mambo mengi yatakuwa yamerekebishwa kwa kushirikiana na Shirika la Bandari. *(Makofi)*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kauli aliyoitoa Mhe. Waziri ni nzito na sisi tutakwenda kuulizwa kwa kauli zetu. Kwa hivyo, mimi naheshimu kauli yake na itakapofika kiasi cha miezi mitatu tutaanza kukwaruzana tena. Kwa maana hiyo, naomba tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, tunaendelea.

Kifungu 1001	– Idara ya Mawasiliano	175,000,000/=
	Jumla ya Fungu	**5,111,000,000/=**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 26 – WIZARA YA MIUNDOMBINU NA MAWASILIANO

Kifungu 0301 – Ofisi Kuu Pemba

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, ahsante na mimi wakati nilipokuwa nikichangia nilitaja sana barabara ya Ole/Kengeja na nilisema kwamba barabara ile ina historia kubwa na barabara ile wananchi wa Ukanda wa Mashariki ya Kisiwa cha Pemba wanaihitajia sana, lakini mpaka leo maendeleo yaliyokuwepo hayaridhishi.

Kwa kweli nilikuwa nikitafuta sana kwenye Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara, lakini nimeikuta kwenye hichi kifungu cha 0301 Ofisi Kuu Pemba. Sasa naomba Mhe. Waziri anipe maelezo kwa sababu hata hapa sione fedha isipokuwa ni shilingi milioni 50,000,000/= tu ambao

ni mchango wa Serikali na wala hakuna fedha za wafadhili na shilingi milioni 50,000,000/= haziwezi kujenga.

Mhe. Mwenyekiti, ukisoma kitabu cha bajeti barabara hii ilifikia hatua mpaka zabuni zikatolewa na ninavyofahamu mimi ukitoa zabuni maana yake fedha za kufanyia mradi tayari umeshakuwa nazo. Lakini mwisho wa maelezo tunaambiwa fedha hazitoshi na mradi huo au barabara hiyo inataka kujengwa kwa ile lami ya kukorogwa, jambo ambalo mimi siridhiki nalo. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri anipe maelezo na hiyo ni hoja yangu ya kwanza.

Vile vile nilichangia pia barabara za jimboni kwangu. Sasa Mhe. Naibu Waziri alinijibu kwamba katika jimbo lako kuna barabara ya Matangini/Kilindi, Mhe. Mwenyekiti nimetafuta mpaka nimechoka sikuona humu. Kwa hivyo, naomba maelezo hizi fedha za kujengea barabara ile ziko wapi?

Halafu niliomba pia nipewe vigezo vinavyostahiki kwamba ili wananchi wafike idadi gani ndio wapelekewe barabara, naomba nielezwe nilikuwa sijaelezwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Mhe. Mjumbe *concern* yake aliyoeleza kwamba ukiangalia katika kitabu kikubwa hichi kuna shilingi milioni 50,000,000/= katika ujenzi wa barabara ya Ole/Kengeja na barabara hii ina urefu wa kilomita 35. Lakini sehemu kubwa ya mradi huu tunategemea kukamilika kwa ufadhili kutoka katika Mashirika za nchi za *OPEC* na takriban Dola za Kimarekani bilion kumi na moja zitatumika katika ujenzi huo.

Mhe. Mwenyekiti, mradi huu kama alivyoeleza Mhe. Mwakilishi ni wa muda mrefu na *concern* ya Serikali kwa muda huo walikuwa wanajaribu kuzungumza na wenzetu wa *OPEC,* ili kuona namna gani tunaweza kuutekeleza. *Concern* ya *OPEC* wao hawana uwezo wa kuongeza cha ziada katika ukamilishaji wa barabara hiyo.

Kwa hivyo, serikali ilichokuwa inajaribu kufanya tathmini ni kuona kwamba tukitaka kujenga barabara hii katika gharama za kawaida katika ile lami ya moto kwa gharama ya chini kilomita moja itatugharimu takribani shilingi milioni 800,000,000/= Serikali ikaona haina fedha za ziada za kuongezea, ili kufanikisha ujenzi wa kilomita zote 35.

Kwa maana hiyo, Serikali itatuma ujumbe maalum kwenda kuzungumza na wenzetu wa *OPEC,* katika mazungumzo hayo Serikali ilikuwa na *option* tatu. *Option* ya kwanza ni kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami ya moto na *OPEC* waongezee fedha na wakakataa, *option* ya pili kwamba tupewe Idara yetu ya UUB ijenge na halafu Serikali iongezee fedha pia *OPEC* nao walikataa kuonesha ile *concern* yao wanahofu.

Lakini *option* ya tatu serikali iliwashauri kwamba tunao uwezo wa kujenga barabara hii kwa njia ya *Labour Base* kama tulivyojenga miradi ya Kusini Pemba na wenzetu wa *OPEC* walikubali. Sasa limekuja serikalini na Serikali tunaendelea kulitafakari namna gani tunaweza kuufanikisha mradi huu, ili kuwa na mambo mawili.

Jambo la kwanza kuhakikisha kwamba mradi huu tunaupata, kwa ajili ya kunusuru hizi fedha kwa lengo la kurahisisha maendeleo. Lakini *concern* ya pili uimara na umadhubuti wa barabara nalo ni jambo muhimu ambalo serikali tunajaribu kulitafakari kabla ya kufikia maamuzi katika mradi huu.

Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Mwakilishi kuwa alichokiona hapa ni *concern* ya Serikali katika huo mradi husika na fedha za mradi huu zitatoka kwa Washirika wa Maendeleo Shirika la *OPEC*.

Jambo jengine ambalo ameuliza Mhe. Mwakilishi ni kuhusu idadi ya watu kujengewa barabara. Mhe. Mwenyekiti, tumejaribu kueleza kwa mara nyingi kwamba kilichopo ni tatizo la umasikini ndio unaotusumbua. Lakini barabara ambazo kama Wizara au serikali tunapaswa kujenga moja kwa moja zimeelezwa ni zile barabara kubwa na barabara ndogo ndogo ni jukumu la wenzetu wa Halmashauri.

Hivyo, kwa kutambua changamoto walizonazo wenzetu wa Halmashauri ufinyu wa fedha, teknolojia, vifaa vya kutendea kazi ikiwa pamoja na wataalamu Idara yetu ya UUB imekuwa ikishirikiana nao.

Kwa maana hiyo, ndio pale tulipomwambia Mhe. Mwakilishi kwamba kwa kupitia Mfuko wetu wa Barabara, ambapo jukumu lake la msingi ni kuzikarabati barabara, lakini tumekuwa tukitumia fedha hizo kujenga barabara ndogo ndogo kwa kushirikiana na hawa Viongozi wa Majimbo, Halmashauri na Kitengo chetu cha UUB, ili kutoa zana, wataalamu pamoja na vitu vyengine.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimfahamishe Mhe. Mwakilishi pamoja na Baraza lako kwa jumla, kwamba hakuna idadi maalum inayolazimisha kuwa idadi hii ndio wanapaswa kupewa barabara. Jambo la msingi ni kwamba kuwepo kwa zile fursa, fedha, teknolojia pamoja na vifaa vikiwepo basi tutasukumu tu huduma ya barabara kwa wannachi wetu.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na maelezo mengi tena ya kina ya Mhe. Naibu Waziri, lakini bado mimi nafikiri kuna usiri maalum wa barabara hii.

Mhe. Mwenyekiti, mradi wa barabara hii ilianza tokea miaka wakati serikali inajenga barabara ya kutoka Kaskazini mpaka pale Ole meli tano ikakatishwa na hapo katikati wakati wa Dkt. Salmin Amour Juma kukatokea sijui mizingwe gani barabara hii haikuendelea na leo tumefika pahala mpaka maelezo ya wenyewe Wizara wameshafanya mpaka zabuni.

Mhe. Mwenyekiti, ukifika hatua ya kuitisha zabuni maana yake umeshafanya mpaka *feasibility study*, umeshajua gharama na tayari umeshakuwa na fedha ndio unaitisha zabuni kwa ajili ya kutafuta *contractor*.

Sasa leo mpaka maelezo ya zabuni, ambapo zilikuwa tayari zimeshakamilika, lakini leo tunaambiwa fedha hazipo mpaka kwanza wakazungumze na wafadhili na huu ni utaratibu gani au kuna usiri gani, hebu twambieni Serikali kuna usiri gani mpaka barabara hii ikawa haikamiliki maisha na wala mimi sijaridhika.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, suala la fedha za mradi tulichokieleza kwamba wenzetu wa *OPEC* wamekubali kutusaidia na fedha hizi kiasi cha *dollar million* 11, ambapo wenzetu wa *OPEC* tayari wameshatusaidia hizi fedha.

Kwa hivyo, kilichopo changamoto iliopo ni kwamba *distance* ni kilomita 35 kama Serikali haiku-*top up* hatuwezi kujenga kwa kiwango cha lami ya moto, kwa sababu gharama zake ni kubwa.

Kwa maana hiyo, tulichokuwa tunajaribu kushauriana kwamba tunaweza kujenga kwa mfumo wa *Labour Base* kama Mradi wa Barabara za Kusini Pemba, lakini sisi wenyewe wizarani tukasema hapana twende tukashauriane na serikali, ili kuzingatia mambo mawili suala la kuupata mradi na jengine ni kuhusu uimara wa huduma za barabara kwa wananchi wetu, kwani jambo hili limekuwa likipigiwa kelele sana. Sasa bado tunaendelea kushauriana serikalini fedha tayari tumeshazipata kwa wenzetu wa *OPEC.*

Mhe. Mwenyekiti, kilichopo ni kwamba kama serikali itakuwa na uwezo wa ku-*top up*, basi jambo hili litakwenda mara moja, lakini kama Serikali itakuwa haina fedha basi lazima tutaendelea kushauriana na Serikali, ili tufikie maamuzi gani katika utekelezaji wa mradi huu na wala sio kweli kusema kwamba mradi huu umekwama kwa kusema labda serikali haina nia, isipokuwa kilichopo ni ukosefu wa uwezo.

Kwa hiyo, tumepata huu msaada kutoka kwa wenzetu wa *OPEC* na tunaamini kwamba kama tungekuwa na uwezo wa kuongezea basi tungeongezea na mradi ukenda.

Mhe. Mwenyekiti, pengine ni *concern* yetu kwa kuzingatia kwamba barabara yenyewe haiko moja kwa moja isipokuwa inakwenda kwa vipande na ujumla wake ndio unakuja hiyo kilomita 35 na ikiwezekana hata tunaweza kujenga na tukaanza na vipande husika, lakini bado tunaendelea kushauriana serikalini, ili kufikia maamuzi sahihi katika utekelezaji wa mradi huu.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, bajeti imechukua muda mrefu sana na ninahakika Waheshimiwa Wajumbe wameshachoka. Mimi nitaachia fungu hili liendelee, lakini *at least* Mhe. Naibu Waziri atwambie huo mdahalo wa mazungumzo utamalizika lini na hii barabara hata kama ni kilomita tatu itaanza lini kujengwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, tunachoweza kukiahidi hapa sisi kwamba tutakwenda kushauriana serikalini. Maamuzi ya serikali yote yatakayoamuliwa tutawajuilisha Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu na wananchi wa ujumla.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, na mimi niwatoe shaka Wawakilishi wenzangu kwamba kijana hachoki, Mhe. Gavu hachoki na yuko makini, wala msimuonee huruma kwa sababu yuko makini sana.
Mhe. Mwenyekiti, nataka niseme kwamba nilihoji barabara ya Mgegedu Kiwani. Miye nataka niishukuru SMZ kwamba kwa muda wa miaka 12 barabara yangu inatiwa fedha tangu mwaka

2000 mpaka leo sisi tunabahatika. Mwaka jana barabara zote Zanzibar zilinyimwa fedha kwa sababu ya Kiwani ingawa mafanikio hakuna.

Kwanza Mhe. Mwenyekiti, ningemuomba Mhe. Waziri asahihishe. Kwenye kitabu fedha ambazo zimepatikana ni milioni 150 alivyokuwa ananijibu Mhe. Naibu Waziri alisema milioni 200 kwa hiyo ni ipi ya kwenye kitabu au ile aliyotoa majumuisho. Pili mara kadhaa barabara hii fedha zikitengwa baadae huhamishwa. Mwaka jana sehemu ya fedha yake ilihamishwa kupelekwa Unguja. Mara hii ameomba milioni 400 kwa ajili ya barabara hii. Barabara hii imekuwa kama kichwa cha mwendawazimu watu wanajifundishia. Teknolojia zote mpya ROMIX ya Mhe. Michano ilikwenda Kiwani ikafeli.

Mwaka juzi milioni mia ngapi na kidogo zikenda Unguja. Mara hii Mhe. Waziri ametoa milioni 400 tumpe. Hebu atwambie mara hii fedha itapelekwa wapi itakwenda Kiwani moja kwa moja na **kujengwa** au kuna mwengine anatafutiwa msitu aje achukue fedha. Naomba anijibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, kwanza napenda kumtoa shaka Mheshimiwa Mwakilishi kwamba suala la usahihi wa takwimu ambazo tumezieleza. Ukisoma vizuri kitabu chetu tumeeleza hadi mwezi Machi zilikuwa zimetumika shilingi milioni 150, lakini hadi Juni tayari shilingi milioni 200 zilikuwa zimeshatumika katika shughuli za ujenzi wa kifusi katika barabara husika.

Nadhani ukisoma au ukisikiliza kwa makini hakuna tofauti ya maelezo yetu. Kuna moja imeeleza mpaka Machi kuna ya pili imeeleza hadi Juni.

Suala la pili ameuliza barabara yake ya Kiwani. Ninachomuahidi kwamba kama lile panga alilolieleza Mhe. Omar Yussuf Mzee halikufika huko Kiwani fedha hizi zote zikiingizwa tutaendelea na ujenzi katika barabara yako ya kiwani.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, Waziri wa Fedha alitufundisha Semina moja alitwambia kwamba mradi wowote unatakiwa uangalie value for money. Barabara hii kama wataangalia wenyewe wa Miundombinuu imetumia zaidi ya bilioni mbili. Maana yake kila mwaka tunapata fedha kwenye makisio. Mimi wasi wasi wangu Mhe. Mwenyekiti kwamba tumekuwa na utaratibu wa kuwanyima wengine fedha kwa msitu wa Mgegedu Kiwani.

Mhe. Mwenyekiti, mimi bado nina wasi wasi kwamba barabara hii imekuwa kama kichwa cha mwendawazimu watu wanajifundishia kazi, watu wanatafuta fedha. Nataka Mhe. Waziri na Naibu Waziri hetu anitoe wasi wasi. Kwa sababu kila mara ninavyofatilia Pemba msitu mkubwa ni kwamba doza bovu na Mhe. Waziri anasema limeshabovuka tena. Mara hii mkipata sababu nyengine mtupe. Mara hii nina hakika watasema kuna masika huko mbele.

Mhe. Waziri hebu anambie hasa, tatizo ni nini. Naomba anielimishe kwamba kila mwaka Wizara ya Fedha wanatenga fedha na wanaingiza na kama ni kichwa cha mwendawazimu basi tena iwe basi. Isichukuliwe fedha ya serikali kila siku ikasukumwa kule kinadharia wakati haifiki. Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Waziri anisaidie hasa, tatizo nini, tatizo jina. Mhe. Jussa ananambia watu bado hawajachinja ng’ombe au nini hasa, kama jina tubadilishe na kama ng’ombe nitoe tuchinje ili kazi ifanyike.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, nimuombe Mhe. Hijja, hana haja ya kubadilisha jina wala hana haja ya kuchinja hata sungura seuze ng'ombe. Barabara hii mwaka jana tuliomba fedha shilingi milioni 300, fedha ambazo tulipata milioni 200 na fedha zote milioni 200 tumezitumia katika ujenzi wa barabara husika.

Ninachomuomba Mhe. Mwakilishi yeye na Baraza lako tukufu kama kuna sehemu yoyote ya hofu kwenye mradi huu basi tuombe wenzetu wakakague ili ile *value for money* ionekane. Msingi wangu mkubwa ninachomuomba Mhe. Mwakilishi atupitishie fungu hili shilingi milioni 400 hizi zinakwenda kuwatumikia wapiga kura wake watu wa Kiwani. Akizuia fedha hizi huo mradi wake wa Kiwani utakuwa haufanikiwi. Mimi imani yangu kwamba mimi na yeye kama kiongozi azma yetu ni kuwatumikia wananchi.

Tulipofika ni hatua nzuri, uwekaji wa kifusi tabaka la kwanza, tabaka la pili, tumeufanya vizuri sana. Namuhakikishia Mhe. Mwakilishi yeye mwenyewe pembeni huwa anakuja kutupongeza. Lakini nashangaa sana kwamba hapa kwenye hadhara anatufuja. Anatupongeza kwamba kazi imekwenda vizuri, imemjenga matumaini, wananchi wamepungukiwa na usumbufu, vilime vile safari zinafanyika vizuri sana.

Nimuombe sana Mhe. Mwakilishi kwamba aendelee kutuamini. Kazi hii tunaifanya kwa azma moja tu ya kutaka kuwatumikia wananchi wa jimbo la Kiwani ili waendelea kumpa imani yeye kama kiongozi wao na kuendelea kujenga imani kwa serikali yao.

Mhe. Hijja Hassan Hijja: Mhe. Mwenyekiti, mimi ningetegemea sahaba Omar pengine angetusaidia maelezo. Kwa sababu sahaba wengine wameshindwa maelezo.

Mhe. Mwenyekiti, tuangalie fedha ya wananchi jinsi inavyopotea kila mwaka. Si kweli kwamba kule *value for money* imezingatiwa. Mwaka juzi walitia teknolojia ya *ROMIX* mpaka kuku awalikufa, sasa kama *value for money* mpaka kuku kufa ndio *value for money* sawa. Lakini kwa kweli kuna haja ya umakini wa serikali.

Mimi niseme kwamba Serikali Kuu hapa sasa iingilie kati, Wizara hii imeshindwa. Haiwezekani mradi miaka 20 barabara ya kilomita saba mpaka hii leo iwe ni hadithi. Mhe. Mwenyekiti, tuendelee kwa imani kwamba Serikali Wizara hii imeshindwa na barabara ile. Labda pengine mzee wangu Waziri wa Fedha pengine afikirie huko mbele. Lakini wa watendaji hawa na Idara hii kwa Pemba hawawezi. Hata kama ingekuwa mimba basi ingezaliwa na mtu akaowa.

Tuendelee kwa imani kwamba ujumbe umefika kwamba wameshindwa na nia hawana na wakitaka leo barabara nyengine watafanya. Kuna barabara wanafanya bila hata ya mipango. Tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Hivi tuendelee katika sura kwamba wameshindwa, hebu Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, mimi nahakikisha kwamba Baraza hili la Zanzibar kwa jumla Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano haijashindwa wala haitoshindwa kuijenga barabara ya Kiwani.

Namuomba Mhe. Mwakilishi avute subra na kuona nini kitafanyika.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi nilipokuwa nikichangia kuhusu suala hili la barabara nilionesha wasi wasi wangu juu ya barabara zote zilizojengwa Mkoa wa Kusini. Pamoja na hivyo mali nyingi za wananchi zilikatwa kwa kujenzi wa barabara hizo na hadi hii leo hakuna fidia yoyote iliyotolewa. Nimemuomba Waziri hapa anithibitishie lini wananchi waliokatiwa miti yao kutoka Mtambile Mwambe, mtambile Kangani watalipwa fidia zao

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Mwakilishi akubaliane na miye kwamba suala la fidia bado ni changamoto kubwa katika miradi yetu ambayo tunayoitekeleza kwa Unguja na Pemba.

Katika suala la mradi huu Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na ubalozi wa Norway tuliweza kutekeleza miradi hiyo na kila sehemu ilikuwa ina *component* ya kutimiza wajibu wake. Suala la fidia liliendelea kuwa bado katika mikono ya SMZ na kwa kujiona ufinyu wa bajeti tumeshindwa kulitekeleza kwa wakati. Namuomba Mhe. Mwakilishi atupe muda ili tuangalie kama kuna *component* yoyote iliyobakia kwa upande wa ufadhili katika mradi huu, tuweze kuitumia *component* hiyo ili kuweza kuwalipa fidia ili wananchi hao wapungukiwe na changamoto hii waliyokuwa nayo.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Mhe. Mwenyekiti, barabara hii haikujengwa jana wala juzi ni zaidi ya miaka mine sasa na zaidi Mtambile/Mwambe. Kwa hivyo muda wizara imepata wa kutosha na juu ya hivyo mnataka muda hadi lini?

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, nadhani Mhe. Mwenyekiti, amekuwa akifuatilia mjadala huu vizuri. Hapa imeelezwa kwamba kuna baadhi ya maeneo ambayo tunadaiwa fidia karibuni miaka 6, miaka 7, miaka 8, hii ni changamoto kwa serikali. Kinachotupelekea kufanya hivyo ni kunusuru miradi, mradi unapokuja *component* ya serikali tunategemea kwamba tutapata fedha za kufanya hivyo.

Lakini kama tunavyotambua kwamba uchumi wetu ni kikwazo. Kutaka nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba kesho tutafanya hilo sina nguvu ya kulisema. Ninachomuhakikishia kwamba azma ya serikali ni kulipa na italipa kwa sababu inadaiwa. Utaratibu kama huu hauko sehemu moja tumekuwa na sehemu nyingi ile fedha zinafidiwa tunapopata hali inapoturuhusu tunalipa.

Nilichomuomba Mhe. Mwakilishi kwamba tutakwenda kuangalia *component* ya upande wa wenzetu wafadhili katika mradi huu kama kuna chochote kilichobaki tutakwangua ili tuweze kwenda kulipa fidia. Miongoni mwa watu wake yupo mzee mmoja huko huko mwambe katika mradi huu, alikuja tukatafuta pahali tukakata pua tukainga wajihi tukamlipa. Sasa ninachomuomba Mhe. Mwakilishi aendelee kujenga imani kwamba sisi tunaijua hii kero, atupe muda tuendelee kupekua pekua mkoba huko, tukikuta chochote kilichobaki tutakwenda kuwalipa fidia wananchi wetu.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Mhe. Mwenyekiti, miembe na minazi iliyokatwa kama ingelikuwa ipo wenyewe wangelikuwa wanavuna embe, wanauza pamoja na kwamba zinamafunza lakini wangelipata. Nazi Pemba moja shilingi 1000 minazi imekwenda kwa ujenzi wa barabara hii. Lakini bado serikali au wizara inatwambia kuwa hatuna uwezo tuvumilie. Mimi nataka tu ahadi hata kwa 2014 lakini uniahidi ni lini watu hawa watapewa fidia zao

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, tumefahamu uzito wa jambo hili kwa *concern* ya Mhe. Mwakilishi, ninachomuhakikishia kwamba kwenye hili tutajifunga kibwebwe kuona kwamba tunaharakisha upatikanaji wa fedha hizi. Ili tuweze kuwalipa fidia wananchi wa jimbo la Mtambile.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Mhe. Mwenyekiti pamoja na kuwa wakati umekuwa mkubwa kwa sababu hapa kuna mpango wa kutafuta pesa katika baadhi ya mafungu ningemuomba Waziri wa Fedha anigaiye kidogo ili watu hawa walipwe fidia zao katika hizo alizokusanya kwa ajili ya meli.
Kifungu 0301 Afisi Kuu Pemba 17,240,000
Kifungu 0401

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, wakati nachangia hoja hii nilielezea umuhimu wa uimarishaji wa Uwanja wa Ndege Pemba Karume Air Port na hasa katika suala zima la kuweka taa. Nilisema kwamba tangu niingie katika Baraza hili serikali mara zote ilikuwa ikija na mpango mahsusi inayoelezea kuweka taa katika kiwanja cha ndege cha Pemba.

Suala hili linaumuhimu mkubwa sana kuifungua Pemba kiuchumi. Lakini vile vile linaumuhimu kuiwekea suala zima la usalama na mipango mengine ya serikali. Suala hili sasa hivi linaonekana linaanza kugeuka badala ya kutekeleza mpango mahususi wa kuweka taa, inaonekana linashindikana sasa hivi inawekwa tu uimarishaji wa huduma za ndege Pemba, halitajwi tena lile. Mimi nilitaka hii ajenda niirudishe kwamba kuna umuhimu wa uwanja wa ndege Pemba kuwekewa taa ili kiwanja kile kiwe na uwezo wa kufanya kazi kwa saa zote. Nilisema kwamba hoja si kuwekwa fedha. Kwa sababu katika bajeti zote fedha inawekwa lakini hoja ni ile dhamira halisi au ni suala la kisera kwamba serikali bado haijaona umuhimu wa suala hilo.

Nilimtaka Mhe. Waziri atakapokuja anihakikishie kwamba ni vipi tutakapolidhinisha fungu hili serikali itaona umuhimu wa kuzitoa fedha hizi katika mwaka huu wa fedha ili kiwanja kile kiwekewe taa kwa maslahi ya kisiwa cha Pemba, kwa maslahi ya serikali kwa ujumla.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na napenda nimpongeze Mhe. Omar Ali Shehe kwa *concern* yake ambayo kabla sijaingia hapa na miye ilikuwa nia yangu hilo. Nakubaliana na *concern* hiyo na naomba nimuhakikishie kwamba mimi nitasimamia kikamilifu katika bajeti ya maendeleo iliyopangwa mara hii kuna shilingi milioni 900, milioni 400 zimewekewa kwa ajili ya uanzishaji wa taratibu za kuweka taa.

Lakini hata hivyo kwa sababu tunazungumza na Mamlaka basi tutaendelea na mazungumzo ili ule mradi ukamilike katika kipindi hichi cha 2012/2013. Baadhi ya matengenezo ambayo yanatakiwa pale Mamlaka yachukue nafasi katika bajeti yake ya matumizi ya kawaida.

Kwa hivyo namuhakikishia Mhe. Omar Ali Shehe katika kipindi hichi cha 2012/2013 tutajitahidi kama inavyowezekana ili ile ndoto ya kuwekwa taa pale iweze kuzaliwa.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru Waziri wa Miundombinu kunioneshea utayarifu wake. Lakini katika hili ili niridhike zaidi ningelikuomba Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu yeye Mhe. Waziri wa Mindombinu ni mpewaji lakini katika mambo kuna mpikaji na mpikaji wa mambo haya yupo katika Baraza hili. Sasa yeye atakaponidhihirishia kwamba atampelekea mpakuzi mimi nitafurahi zaidi.

Kwa hiyo namuomba, kwa sababu nilisema suala hili linahusiana na suala la Kisera kwa Serikali. Ningelimuomba Mpikaji ambaye ni Waziri wa Fedha na Uchumi naye ni somo yangu na yeye angalau anipe uhakikisho kwamba mpakuzi naye atampelekea ili sisi walaji tuweke tamaa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, kwanza mimi nataka nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri. Vile vile namuielewa *concern* ya Mhe. Omar Ali Shehe, somo yangu Mwakilishi wa Jimbo la Chakechake.

Nataka nimwambie kwamba tunampango mkubwa sana kwa ajili ya Uwanja wa Ndege wa Pemba. Kama alivyosema mwenyewe lengo letu ni kuifungua Pemba na hatutoweza kuifungua Pemba bila ya kuwa na Uwanja wa Ndege ambao utaweza kukidhi haja ya wageni wanaotaka kwenda katika Kisiwa cha Pemba. Nataka atuamini sasa hivi tayari tumeshaandaa *concept note* kwa ajili ya Uwanja wa Ndege wa Pemba na tunayo *Pre Feasibility Study* kwa ajili ya Uwanja wa Ndege wa Pemba.

Jana nimepokea maelekezo juu ya miradi ambayo tunatakiwa kuiwasilisha kwa ajili ya kupata msaada kutoka kwa serikali ya China. Nimeongea na wenzangu pale ofisini miongoni mwa miradi ambayo tumeiorodhesha ni Uwanja wa Ndege wa Pemba. Kwa hivyo haja hiyo ipo ni kumuongezea tu majibu ya ziada ambayo Mhe. Waziri amempa somo yangu. Lakini kama alivyoomba kwamba basi hali kila itakapokuwa nzuri, kila tutakapopeleka fedha miundombinu nitamkumbusha Waziri mwenzangu kwamba Uwanja wa Ndege wa Pemba.

Nitajitahidi kufanya hivyo ili niwapatie fedha. Lakini kila nitakapopata nafasi nitamkumbusha *responsibility* yake kwamba Uwanja wa Ndege wa Pemba katika hizo fedha basi angalia na Uwanja wa Ndege wa Pemba. Nitafanya hivyo na tutashirikiana. Namuomba Mheshimiwa somo yangu atuamini. Na yeye katika wale Maswakhaba waliotajwa Omar yumo. Kwa hivyo nataka atuamini. Tutafanya hivyo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mheshimiwa kwa kuwa kataja jina kubwa la Swakhaba basi tuendelee.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru. Katika mchango wangu jana nilizungumza kwa urefu sana *concern* niliyonayo katika miradi hii ya maendeleo inayokuja kwa njia ya mkopo wa nduguu zetu hawa sio wa damu sijui niwaite vipi, hawa Wachina.

Sasa hivi Mheshimiwa rafiki yangu kaka angu Mhe. Omar Yusuf Mzee kanitajia tena. Mimi nikija nikipandisha hatari yake maana chano chake hatari maana nataka mkataba wa Muungano

wanye saini ya Mzee Karume na Mzee na Mwalimu Nyerere haupatikani, kwa hivyo inakuwa tabu kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nataka nipate maelezo tu kwamba katika miradi hii kuna ujenzi wa jengo jimpya la abiria Karume Air Port kuna mia tano milioni ambayo ningeomba *contribution* lakini halafu kuna bilioni thalatini na tano na milioni mia mbili ambazo ni mkopo.

Mhe. Mwenyekiti, alipokuwa akijibu hoja yangu, nadhani alikuwa ni Mhe. Naibu Waziri aliyejibu, alitutolewa wasi wasi na baadaye Mwanasheria Mkuu aliponyanyuka na yeye ajaekezea kadhia. Nataka nimwambie kwa heshima na taadhima sikubaliani naye maelezo yake, lakini sitaki kuingia katika malumbano hayo saa hizi juu ya mikataba miwili na kilichotokezea.

Hoja yangu kwa sasa inahusu suala hili na hili nadhani labda kuliko kuwasumbua watu wa Wizara ya Mawasiliano nimtake Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Kwamba tunahaja ya kuridhishwa kwamba hii mikopo tunayoingia inakuwa ni shubiri inayopakwa shira nzuri sana, kwamba *interest rate* ni ndogo sana, lakini ukitizama gharama zenyewe za shughuli inayohusika zinakuzwa kupita kiasi.
Mhe. Mwenyekiti, jana nilitoa mfano hai hapa kwamba nilipomuuliza Mhe. Naibu Waziri alinijibu kwamba mfano mradi huu wa Gati walipopewa hawa walikuja na makisio ya dola milioni 800. Lakini wao walipokwenda kufanya utafiti wakagundua kwamba wanahitaji dola milioni 400 na nikasema mimi naamini pengine chini ya hapo Mhe. Mwenyekiti.

Hoja yangu Mhe. Mwenyekiti, mradi huu tumeshauingia na mimi najua athari za kuvunja mikataba tumeona kwa wenzetu, mnaweza mkashtakiwa mkapata adhabu. Lakini ninachopata wasi wasi kwamba tunaendelea mpaka leo kutaja miradi ambayo tunaendelea kuwakumbatia hawa. Hawa kama nilivyosema jana *Exim Bank* ya China *policy* yake maalum imewekwa kazi yake ni kutafuta miradi kama hii. Utapewa mkopo lakini sharti lake ni kwamba lazima uchukue kampuni zao. Matokeo yake ndio kama yaliyotukuta.

Nilikuwa nataka maelezo ya Mhe. Waziri wa Fedha kwamba tunausalama gani wa fedha hizi ambazo tunazipata kutoka katika *foreign loans* ambazo zinakuwa ni mzigo kwa wananchi kwa miaka mingi ijayo kuendelea kulipwa wakati utekelezaji wa miradi yenyewe kwa Kampuni ambazo wakopeshaji wanalazimisha zinatuingizia mashaka kama ambavyo tumeshaona katika mifano michache ukiwemo mradi huu wa Air Port. Nilikuwa naomba maelezo.

La pili Mhe. Mwenyekiti kwa sababu hakuna mwenye hoja nyengine katika Idara hii nimalizie kabisa ya tatu nilikuwa naomba kauli ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano. Hapa pana mradi wa ujenzi wa *taxiway* ambao ni muendelezo ya ule mradi wa uzio uliotajwa mwaka jana, ambao wananchi wengi wameathirika kama nilivyosema jana na kwamba wamebidi wahamishwe pale na walipwe fidia.

Mhe. Mwenyekiti, hili bado. Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akijibu hoja yangu alisema kwamba wengi wameshalipwa bado watu wanne. Nilikuwa naomba kusaidiwa hapa. Mimi ninazotaarifa kwamba wengi hawakuridhika na malipo hayo. Jana baada ya kuliibua suala hili Mhe. Mwenyekiti, baadhi yao walinipigia simu, wakasema kwamba umeliwasilisha sivyo na kwamba

wao walikataa hizo fedha, kwamba haya makisio ya awali yaliyoletwa ndio ambayo waliyokuwa wakidhani kuwa ndio sahihi kuliko ya Kamati ambayo yaliyokuja.

Nikuwa naomba hebu Mhe. Naibu Waziri na hili pia anijibu lini watalimaliza suala hili na hasa akitambua kwamba hata kamati ambayo imeundwa na Makamo wa Pili wa Rais wananchi wa pale hawana imani nayo Kamati ya kina Mhe. Abdalla Rashid na wenzake. Nilikuwa naomba nipatiwe maelezo kuhusu mikopo na hilo Mheshimiwa linalohusu ujenzi wa uzio ambao umepelekea hasara kubwa kwa wananchi waliohamishwa pale wakiwa bado wanadai fidia zao. Lini watalipwa fidia zao kwa kiwango ambacho kinaridhisha. Naomba maelezo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi wa Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu vizuri sana Mhe. Ismail Jussa Ladhu, hasa ile concern juu ya usalama wa fedha hizi ambazo tunazozikopa kutoka katika Exim Bank. Amekuwa *very specifically* amezungumzia *Exim Bank* ya China.

Nataka nimueleze tu kwamba kiutaratibu ni kwamba *Exim Bank* yoyote ima iwe ya China, ya Uturuki, ya India, ya Amerika, wanapokukopesha moja ya sharti lao kubwa ni kwamba wajenzi watoke katika nchi zao, *(Contractors must come from there own countries)*. Hilo ni moja ya sharti lao, tumezungumza na *Exim Bank* ya Uturuki, tumezungumza na *Exim Bank* ya China, tumezungumza na *Exim Bank* ya India, hilo ni moja ya sharti lao.

Uzuri wake ni kwamba wanakupa katika *rate* ndogo kabisa ambayo chini ya asilimia 2 ya ule mkopo ndio riba. Lakini ukenda kwenye *commercial bank* unaweza ukapata kwenye asilimia nne mpaka nane, inategemeana na nguvu zako za kujadili na kuba-gain lakini hizi

Concessional Loan na jengine ambalo nilikuwa nataka nimwambie ni kwamba benki ya dunia na shirika la Fedha la Dunia IMF wao wanazielekeza nchi maskini zikope consetional loans hawazielekezi ziende commercial kwa hivyo ndio ukaona nchi zetu nyingi tunakopa kuelekea huko. Lakini jambo zuri tu katika mkutano uliokuweko kule China/Afrika serikali ya China imeweka *about 20 bilions dollars* kwa ajili ya kuzisaidia nchi za Afrika na ndio maana nikasema kwamba sisi kama Tanzania lazima tuchangamkie angalau na sisi tupeleke basi sehemu ya miradi kule tupate hizo fedha.

Lakini hili alilolizungumza Mhe. Jussa nataka niseme tu kwamba fedha tunapokopa kupitia exim banks kwa sababu wakondorasi wajenzi ni wao wenyewe nchi hizo lazima sisi tunaokopa tuwe na utaratibu mzuri wa kuzisimamia fedha zile kwa usalama wa fedha zetu. Moja ambalo mimi ninalisisitiza lazima tuwe na design au mtaalam anayetutayarishia *feasibility study* awe ni mtaalam tofauti na wale. Hili litahitajia fedha zetu zenyewe za ndani au litahitaji kupata fedha kutoka taasisi nyengine. Ndio maana nikasema kwamba na Mhe. Waziri amezungumza hapa moja tuliloweka humo ni kufanya physibility study kamilifu kwa ajili ya uwanja wa ndege wa Pemba. Ukiwa na *physibility* study ambayo umeifanya wewe mwenyewe utakuwa na mtu ambaye amekufanyia tathmini ya ule mradi una-cost kiasi gani.

Kwa hivyo unapokwenda kuomba mkopo unajua kwamba ule mradi wako una-cost kiasi gani na mkopo wako kiasi gani na utakapomwita mjenzi, mjenzi yule utakuwa unajuwa wewe kiasi gani

kinachoku-bind wewe uweze kumpa ile contruct ya ujenzi. Vyenginevyo tunavyokifanya sasa hivi utakuta mchina huyo huyo ndio anapewa yeye afanye *feasibility study*, yeye ndio aje ajenge, kwa hivyo unakuta hizi bei zinakuwa kubwa kama alivyo-raise concern ndugu yangu hapa Mhe. Jussa. Mimi ninaiomba sana Serikali ya Mapinduzi Zanzibar tuweke fedha kwa ajili ya kufanya wenyewe *feasibility study* halafu ndio twende tukatafute mkopo kulingana na ile *feasibility study* ambayo tuliyoifanya wenyewe badala ya kumpa yule yule ambaye anatoka nchi ile ile, halafu yeye anakwenda kukusaidia pesa kutoka nchi za nje zile zile hii inakuwa ngumu kidogo na ndio gharama alivyosema Mhe. Jussa inakubwa kubwa.

Kwa hivyo hiyo concern ya Mhe. Jussa sisi tumeiona pale Wizarani ndio kwa maana sasa hivi tunakuwa *very careful* tunataka tutafute fedha zetu wenyewe ili tufanye physibility study sisi wenyewe. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti nataka nimuhakikishie Mhe. Jussa kwamba tutakuwa waangalifu sana katika hilo.

Mradi wa *terminal building* mpya historia yake nadhani waziri na manaibu husika wanaielewa na nadhani sina haja ya kuieleza hapa kwa sababu mimi ninaielewa juu juu tu kwa sababu nimekuta wakati tunaingia nimekuta tayari vuguvugu, mchakato unaendelea. Kwa hivyo hawa wanaelewa zaidi kuliko mimi. Lakini ninachotaka kusema kwamba sasa hivi bora ni vyema tukafanya *feasibility study* sisi wenyewe kwa gharama zetu wenyewe halafu tutafute fedha ili tuweze kusimamia haya maelezo ambayo anasema Mhe. Jussa.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti Mhe. Jussa amejaribu kukumbushia hoja yake inayotokana na suala la fidia kwa ujenzi wa tax and apron katika uwanja wa ndege wa Abeid Amaan Karume *International Airport*.

Mhe. Mwenyekiti, wakati wa mwanzo hili jambo kutangazwa ile azma na serikali wananchi wengi ambao walisikia maneno ya kiembesamaki walihamanika, walishtuka na kupelekea zogo na makelele pengine kukaribia hata uvunjifu wa amani. Na wengi walikuja na kauli kwamba maeneo yao yamevamiwa, wamenyang'anywa, wamedhulumiwa na kauli nyengine kama hizo.

Mhe. Makamo wa Pili alitumia busara zake akenda akatembelea eneo akaahidi siku ya Jumamosi kufanya kikao pamoja na wananchi wote maeneo husika Kiembesamaki katika hall la Chuo cha Karume hapo Mbweni. Lakini baada ya kufanya hivi serikali ikaamua kutengeneza kamati ndogo ya wazee wa Kiembesamaki. Baada ya kamati ile kupitia kwa kina ikakuta ni watu ambao hawatozidi 22 ndio watakaoguswa na kadhia hii moja kwa moja. Katika tathmini hiyo, awali ya hapo wakati mradi huu unaombewa fedha World Bank kulifanywa tathmini na ma-*urgent* wa World Bank ambao walifanya tathmini kubwa. Baada ya serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupatiwa tathmini ile na baada ya kamati hii kuundwa kuliratibu hili suala na kulifanyia uhakiki kwa kina ikabainika kwamba kuna watu wengi ambao waliandikishwa kwamba anastahiki kulipwa fidia watu ambao hawana nyumba, hawana maeneo, wala hawana kitu ambacho kinapaswa kulipwa fidia.

Hivyo kamati hii kutoka ile tathmini ya kwanza ambayo ilikuwa takriban shilingi milioni mbili ikaweza kunusuru karibu nusu ya gharama hizi kwa msingi kwamba kutoka bilioni 2.1 imeshuka hadi bilioni 1. Sasa msingi mkubwa kwamba kamati hiyo kwa upande wa serikali imetusaidia sana na serikali pia imeonesha concern vizuri katika suala hili. Maana miongoni mwa watu

ambao walitakiwa kuliwa fidia kulikuwa kuna sehemu ya uondoshaji wa makaburi. Serikali ikakubali kugharamia uondoshaji wa makaburi hayo, lakini pia kulikuwa kuna watu walikuwa na kijiji chao pale, serikali ikakubali kubeba gharama ya kuwatafutia viwanja. Sasa kama kuna mtu ambaye amehusika katika kadhia hii *task way* na apron kwamba analalama fidia haikuwa vizuri hilo mimi sijalipata. Na kama tutalipata basi tutasema mwananchi huyo atakuwa hatutendei haki kama serikali. Kama analalama kwa maeneo mengine hilo siwezi kuwa na hakika nalo. Lakini katika utaratibu wa task na apron serikali ime-*concern* vizuri sana imejiridhisha juu ya watu ambao wana mali zao, viwango ambavyo wamepewa, umuhimu wa kuheshimu dini na taratibu ziliopo, namna ya kuhamisha makaburi, mashekhe wamehusishwa, familia za pale pia zimetengenezewa viwanja ili kupata kutengeneza vijiji vyengine katika eneo ambalo litatumika kuzika jamaa zao.

Sasa nimuombe Mhe. Mwakilishi kama kuna watu wengine katika eneo hili watakuwa wanalalama inawezekana taarifa zao si sahihi. Kwa sababu tathmini iliyofanywa ni watu 22 serikali imejiridhisha na wameanza kulipwa takriban bado watu wane ambao hawajenda kuchukua fedha zao. Na hawa wamelipwa kwa kuridhika, kuna watu wamelipwa kwa njia ya hundi. Baada ya kuridhika kamati imemfata mtu mmoja mmoja kwa kwenda kuonesha eneo husika kwa kuhojiwa na yeye mwenyewe atakuwa ameridhika, hakuna sehemu yoyote iliyofanywa kazi hii kwa njia ya udanganyifu. Sasa kama kuna jambo jengine naomba Mhe. Mwakilishi aweze kutuarifu kama kuna hatua za serikali tuweze kulifatilia zaidi.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, ninashukuru kwa hoja zangu zote mbili kupata majibu. Kwanza ninamshukuru Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa kuielewa concern yangu na kukiri kwamba wataizingatia na kuifanyia kazi kuingia katika miradi hii hasa ambayo inajumuisha mikopo na ninashukuru mwenyewe kakiri kwamba, Mhe. Mwenyekiti, niombe suala moja hii mitambo bado inatusumbua sana tunaumia sana katika kusikiliza unaweza ukaona labda simu iko wazi lakini huko huko kwenye mitambo. Sasa kuna tatizo linalia ovyo lakini bado echo zinatusumbua sana Mhe. Mwenyekiti hasa kama hujazoea kufunga kama Mhe. Mwenyekiti inakuwa tabu kweli kweli saumu inazidi kunikaa.

Mhe. Mwenyekiti, naendelea hoja yangu nilikuwa nasema ninamshukuru Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa sababu kama nilivyosema kaielewe concern yangu na kanambia ataifanyia kazi. Yeye kakiri kwamba hizi taasisi zinazosimamia mikopo zinashajiisha kuangalia *Concessional Loan* baada ya kuangalia commercial loans. Lakini anafurahi kasema kwamba interest ambayo ilikuwa ndio hoja yangu ni ndogo si zaidi ya 2%. Lakini kakiri kwamba kuna tatizo hilo la ku-inflect kuongeza kupita kiasi gharama za miradi na mfano hai ni mradi wa bandari lakini nina hakika katika kila mradi uko hivyo hivyo. Mimi ninaamini hata huu tukenda tukiufanyia tathmini upya tutajua kwamba hapa tumeunoa hapa maneneo ya Mzee Moyo tumeunoa hapa.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nasema nakubali kaliona ninaamini kwamba watachukua kila hatua kuepusha nchi yetu tusiingizwe katika madeni ambayo kwa miaka mingi wananchi wataendelea kuyalipa huku kwa sababu tu tulikuwa tunafanya vizuri katika kufanya upembuzi yakinifu ya miradi hiyo.

Sasa nije katika hili la mwisho Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti ninamshukuru Mhe. Naibu Waziri vile vile kwa maelezo yake, nilichokikusudia nimekiunganisha hapa Mhe. Mwenyekiti kwa sababu katika kitabu chenyewe mradi wa tax way na apron umeunganishwa na mradi wa uzio ambao bado wananchi wengi wana malalamiko yao. Katika kitabu hiki hata nilihoji mimi lakini ninashukuru nikapewa maelezo ya kutosha. Sasa mimi Mhe. Mwenyekiti sitaki tuendelee kusumbuana sana katika suala hili la fidia. Ninachokiomba nimesema hapa concern. Leo Mheshimiwa hapo juu sasa asubuhi walikuja miongoni mwao watu bwana wana malalamiko yao na hili limechukua muda mrefu mno Mhe. Mwenyekiti wanasumbuliwa sana . Na mimi ninaiomba hii Wizara iangalie na serikali kwa ujumla wake sijui nani anaeshughulika kulipa fidia hizi kama Wizara ya Mawasiliano au na Wizara ya Fedha inaingia. Lakini hebu alitazame kwa ujumla na Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais, wananchi hawa Mhe. Mwenyekiti wanalalamika kwamba hii kamati ambayo kaiunda Makamo wa Pili wa Rais waliopewa kamati hii wamegeuza dill, hii masuala ya kufatilia ndio maana unaambiwa wako 22 wananchi wenyewe wanalalamika kwamba wametoa nyaraka zao zote na watu wenyewe waliochanguliwa katika kamati hii tunawajua rekodi zao, uaminifu wao na uadilifu wao ni wa kutiliwa mashaka makubwa katika nchi hii Mhe. Mwenyekiti. Hakuna asiyejua Mhe. Abdalla Rashid na wananchi walikuwa na malalamiko makubwa dhidi yake. Watu kama hawa Mhe. Mwenyekiti unapokwenda kuwapa kazi ya kuwasimamia wananchi na haki zao wanakuwa na mashaka.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti ninachosema mimi hebu hili Mhe. Makamo wa Pili, Wizara ya Fedha, Wizara inayohusika walifatilie hawa watu waliowapa dhamana kuwasimamia wananchi, wananchi hawana imani nao na ndio maana mpaka leo wanaendelea kusumbuka malalamiko hayamaliziki miradi inasonga mbele haki za wananchi hatuzitoi. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti kama nilivyosema sitaki tuendelee kupiga kelele, nataka nipate kauli ya serikali hebu hili walifatilie hii kamati waliyoiunda waitazame upya, hii kamati ndio tatizo.

Hii kamati imekuwa kamati ya kufanya dill la kushughulikia malalamiko ya wananchi na ukiwaangalia wajumbe wake unawaona kwamba wenyewe si waadilifu kwa maumbile yao Mhe. Mwenyekiti na historia zao katika nchi. Kwa hivyo nilikuwa naomba hili nilimalizie hapa nikubali tuendelee lakini niiombe serikali hili walifanyie kazi iaangalie tena madai haya ya wananchi wapewe haki zao. Mhe. Mwenyekiti ninakushukuru sana.

Mhe. Naibu Waziri Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, concern ya Mhe. Mwakilishi tumeisikia concern ya serikali tumeipokea tutaifanyia kazi.

Kifungu 0401 Idara ya Mipango na Sera 79,100,000,000

Kifungu 0701

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti nilipokuwa nikichangia niliuliza kuhusu barabara ya bwawani, barabara ya bwawani imefanya mashimo makubwa na muda mrefu haijafanyiwa marekebisho. Isitoshe kuna barabara jimboni kwangu Jambiani Mfumbwi hati kibigija, tokea ukoloni barabara ile haijapata jicho la rehema je Mhe. Waziri unaniambiaje.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti kwa heshima kubwa namuomba kaka yangu Mhe. Jaku Hashim Ayoub ende akaangalie eneo la bwawani hivi sasa hiyo barabara ambayo akilalama ina mashimo mimi jana usiku saa tatu baada ya kumaliza mazungumzo mimi na yeye, nilikwenda kuikagua barabara tayari mashimo hayo yamefanyiwa kazi hayapo.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, mpango wa Wizara yetu chini ya mfuko wetu wa barabara, barabara hii yenye urefu wa mita 270 tutaijenga kwa *overlay* tena ili kuonesha kwamba hili tatizo linaondoka moja kwa moja. Lakini hatua ya kwanza ya kuziba yale mashimo yote katika barabara ya bwawani imefanyika jana na mimi mwenyewe nimekwenda kushuhudia usiku kwamba kadhia hiyo haipo tena.

Suala la pili alilouliza Mhe. Mwakilishi ni kuhusu barabara ya Mfumbwi hadi Kibigija. Tulichomjibu Mhe. Mwakilishi kwamba tulichokuwa na uwezo nacho ni kwenda ku-grade ile barabara na tumesema hivyo kwa sababu kama serikali tayari tumejenga mradi mkubwa wa barabara iliyotoka Michamvi, Paje hadi Makunduchi. Sasa tunaposema kwamba serikali tunachukua fedha nyengine za wananchi kwenda kujenga barabara nyengine ndani mitaani, aa hili halipo. Ninachomuomba Mhe. Mwakilishi yeye kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Kusini aje Idarani kwetu tutashirikiana kwenda kuwasaidia wananchi wale kwa barabara yake kuwekwa kifusi na huduma nyengine hatujakataa, lakini haziko katika mpango wetu wa Serikali kwamba kuna fedha ambazo tumetenga. Aje na vichoche vya maendeleo kwa kupitia mfuko wa Jimbo, Halmashauri tutachoweza kumsaidia sisi vifaa, utaalam ili kwenda kuifanya huduma hiyo wa wananchi katika barabara hiyo kwa kiwango cha kufusi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Sawa Mhe. Mwenyekiti nimemsikia Mhe. Naibu Waziri tuendelee.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti mpaka nimeweka shingo upande. Mhe. Mwenyekiti kuna waheshimiwa sikuwapa heshima yao nataka niwaombe radhi nataka niwape sasa hivi. Tulimsifu Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa kuanza kutekeleza kwa haraka yale ambayo tunayoyashauri. Lakini ninamsifu sana rafiki yangu na mwalimu wangu wa pentagon Mhe. Shamuhuna na yeye katika ushauri tulioutoa haukuchukua muda mrefu tayari tunashukuru vijana wameanza kufurahi salamu zako Mheshimiwa.

Lakini Mheshimiwa nyumbani kwangu kidogo hali si nzuri vikosi safari hii wamekatwa pesa zao. Sasa ninasifu wizara nyengine wizara yangu Mhe. Waziri naomba watakuangusha hawa tusaidie kidogo. Lakini kwa upande wa Manispaa wanaanza kujirekebisha.

Mhe. Mwenyekiti ninakuja katika hoja, sasa hivi unajua tunatumiwa message mnasinzia Mheshimiwa huwa tunakaa kama hivi kwenye mike hatusikii vizuri sasa hili la kwako tunaomba watu wako waangalie utaratibu wa kutufanyia zile za humu masikioni ili waziri anaposema tumsikie vizuri, kwa sababu unaweza kuja kumuuliza swali pengine ameshalijibu. Sasa tunaomba hili ingawa liko nje kidogo lakini za masikioni utusaidie.

Nakuja katika hoja, Mheshimiwa Waziri katika majumuisho yake alizungumzia barabara ya Shaurimoyo nimeangalia kwenye 750031 lakini vile alivyonijibu kidogo isijekuwa kama tukishapitisha hapa mambo ndio yameshamaliza, kwenye kitabu chake cha bajeti sikuiona,

kwenye buku kubwa haimo, baadae kaniletea karatasi mkononi imo lakini ile karatasi ya mkononi. Sasa nilikuwa ninaomba Mheshimiwa barabara ile kuna ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Sita, kuna ahadi ya Rais huyu aliyekuwepo wa Awamu ya Saba, barabara ile iliwahi kufanyiwa majaribio katika lami ya mwanzo ya Romis ilikuwemo ikafanyiwa majaribio, mpaka leo bado haijaingia katika mpango.

Kwa hivyo hili Mheshimiwa nilikuwa nataka tu nipate angalau ile kauli wananchi wa Kwamtipura wasikie, naamini Mhe. Waziri kajiandaa lakini kujiandaa kwakwe mimi hakunisaidii kama wananchi na wao hawajajua ile barabara iko katika utaratibu gani. Nilikuwa naomba kidogo maelezo Mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hamza ile kuchomeka chomeka kwenye hoja hii mambo yanayohusu wizara ambayo tumeshaipita tungeacha na tutajitahidi kuona kwamba tunaweka vitu vya kuweza kusikia. Lakini mnisaidie vile vile msipige sana mabao tunaharibu hizi mike.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, naomba tu Mhe. Hamza ajenge imani ya maelezo ambayo nimempatia kwamba kulikuwa kuna makosa kidogo ya typing error kutoka katika kitabu chetu cha bajeti. Maamuzi yetu wizarani ni kwamba ile miradi yote ambayo itatekelezwa na wenzetu wa mfuko wa barabara tuliona ni vyema tukawa tumei-*attache* kama *annex* kule nyuma. Lakini bahati mbaya eneo lile ambalo barabara yake imo likawa halikutokezea. Lakini ninachomuhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba, barabara hii ya kwa Abass Husein hadi Shaurimoyo tutaijenga kwa kiwango cha kifusi na mimi ninachomuhakikishia kwa usahiba wetu nitaiondoa katika third quarter tutaijenga katika second quarter. Ninamuomba Mhe. Mwakilishi atupitishie fungu hili twende tukafanye kazi na mfuko wa barabara utakapokuja, wapitishiwe fungu lao ili tukafanye ya kuwapelekea maendeleo wananchi wetu.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nimeridhika lakini si sana na katika hatua ya mwanzo nitakubali ile barabara itiwe kifusi lakini ninamuahidi akitia kifusi na mwakani itabidi aje atie kifusi tena. Mheshimiwa ile barabara kubwa, sasa hivi inatumika zinapita daladala yaani kila kitu kinapita katika barabara ile. Mheshimiwa katika mpango wa mwanzo hapo ilipokuwa inafanyiwa majaribio ya romis ilikuwa si kifusi, ilikuwa lami. Sasa nilikuwa ninamuomba Mheshimiwa sawa mwache atie kifusi lakini katika lile eneo sugu hilo alilolifanyia majaribio ya romis kutoka kwa Abass Hussein mpaka kule juu kwa sheha wa Shaurimoyo kwa sababu Mheshimiwa pana mteremko mkubwa wa maji. Itakuwa kila siku kama hivi tumepata fedha za mfuko wa maendeleo wa jimbo milioni tano sishakwenda, ina maana na mwakani milioni tano nyengine zitakwenda, mbali nyengine tulotoa mifukoni ukiacha vifusi tunatia kila siku.

Sasa serikali ikija ikitwambia inatia kifusi ile barabara kubwa sio barabara ndogo kama inavyofikiriwa. Kwa hivyo nilikuwa ninamuomba tu Mheshimiwa waziri kama hali itaruhusu maana yake unajua Mheshimiwa, barabara yangu mimi ninasikitika kwamba sisi ndio tuliokuja mwanzo mjini, leo zinatiwa wapi huko Nyarugusu, kule kwa mchina watu wamekuja juzi leo watu wa mjini mwanzo tunaachwa leo ndio kwanza kunatiwa vifusi kwa mchina mwanzo kote kunangara. Mheshimiwa mimi hili jimbo ninalitaka bado. Mimi nadhani ajaribu kuangalia uwezekano kwa sababu kifusi kila siku mtakuja kutia kifusi mpaka lini? Au mnataka kila siku

niizuie bajeti, mwaka jana nimeizuia, mwaka huu nazuia, mwakani nizuie itakuwa kazi yangu hiyo tu.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti concern ya Mhe. Hamza nimeisikia na ninachomuahidi kwamba kwa mwaka huu akubali tumuwekee kifusi, tutazungumza na wenzetu wa mfuko wa barabara ili concern ya kuona hasa yale maeneo kama alivyoeleza Mhe. Mwakilishi na kwa Abass Hussein kwenye mteremko kilima kukinusuru, kwa ajili ya kuweka lami tutawaomba wenzetu wa mfuko wa barabara sisi tutaangalia hali ikiwa hali inaruhusu basi tutalifanya. Lakini kwa mwaka huu tunamuomba Mheshimiwa aruhusu kutupitishia fungu letu tukafanye kazi.

Mhes. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti kwa kuwa safari hii nitapakwa wanja jicho moja na hii wanja iliobakia bajeti ya mwakani lami mpaka mwisho namba tuendelee.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Ninakushukuru Mhe. Mwenyekiti kunipa nafasi ya mwisho kichinja mimba ninajua mambo yangu yatanyooka vizuri hapo. Mhe. Mwenyekiti katika mchango wangu nilizungumzia suala la ulipwaji wa fidia kwa wananchi wa vijiji vya Shingwi, njaro, kibuyuni na baadhi ya maeneo ya Jimbo la Mkwajuni, ambao waliathirika kutokana na upasuaji wa miamba huko kiashangwe wanakochujia kifusi. Kuna Kampuni ya Meco walipokuwa wanajenga barabara ya Mkwajuni Nungwi walikuwa wanapasua miamba kule kwa ajili ya kifusi. Sasa wanapopasua ile miamba mtikisiko unakuwa mkubwa sana.

Kwa hivyo baadhi ya nyumba za wananchi wangu pale ziliathirika. Nilitoa taarifa hiyo kwenye Wizara, tukatoka na uongozi wa wizara tukakagua, wakamtafuta na yule mkandarasi tukenda tukagua pamoja, tukakubaliana kuzifanyia tathmini zile nyuma. Tukafanya tathmini ile wakaondoka kwamba watatuletea jawabu, lakini jawabu lile Mhe. Spika, mpaka leo zaidi ya mwaka wa pili huu hakuna jawabu linalokuja. Kila nikiuliza napigishwa kalenda, wananchi wale wamekosa subira sasa, wameshavumilia mpaka wamechoka maana kuna wengine kuna wengine mabati, wengine kuta, kuna wengine vyoo vimeanguka tatizo limekuwa kubwa.

Sasa mara ya mwisho nilipokwenda pale wizarani nikaambiwa tumeshakubaliana na mkandarasi tutawalipa. Ninafikiri mara ya mwisho ilikuwa ramadhani kama hii ya mwaka jana nilikwenda tena kusikiliza, nikaambiwa nivumilie kidogo wanakuja kulipwa lakini mpaka hii leo hawajalipwa. Nilikuwa naomba Mhe. Waziri anieleze ni lini wananchi hawa watapewa fidia zao kutokana na uharibifu ule uliofanyika.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti naiona sana concern ya Mheshimiwa Mwakilishi lakini kwa kuwa kazi yetu sisi ni kuratibu na mlipaji ni mkandarasi, tunamuhakikishia kwamba kazi hiyo tutaifanya katika muda ambao si mrefu na yeye pamoja na sisi tushirikiane ili tushirikiane ili kazi hiyo iende kwa wepesi.,

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri mpya lakini nimepata wasiwasi maana hapa sababu ya kuzuia hili fungu Mhe. Mwenyekiti nimeona kuna ujenzi tena hapa wa barabara wa Matemwe Muyuni ujenzi wa Mkwajuni Kijini hawa watakwenda kupasua tena miamba pale, ikiwa watakwenda kupasua wale wa mwanzo hawajalipwa, kuta zile zina nyufa si watakwenda kuziangusha zile nyumba. Sasa nilikuwa

ninamuomba sana Mhe. Waziri yeye kama mratibu, sisi hatuwatambui hao, tunaitambua serikali ndio inaowaleta pale. Maana yake hao Meco watakuwa wamepewa tenda na serikali, sisi hatuijui Meco tunaijua serikali yetu. Kwa sababu wananchi wangeamua wangekwenda kuwazuia wasifanye ile kazi ninafikiri ingekuwa si kitu kizuri. Lakini waliwaacha waendelee na kazi kwa makubaliano kwamba wao serikali watahakikisha kwamba wananchi wale wanalipwa fidia zile. Sasa leo wakisema wao wanaratibu tu hawawezi kulipa mimi kidogo nitakuwa sijamuelewa Mhe. Waziri, ninamuomba anieleweshe vizuri ili wananchi wangu wale, hivi sasa wamekaa wananitizama huko. Maana wamenambia nisipolisema hili basi pale kwanza nisiende, lakini nasema na wenyewe wananisikia sasa ninamuomba Mhe. Waziri atoe kauli juu ya jambo hili.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Ninashukuru Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu yeye mwenyewe anajua kwamba sio serikali ni mkandarasi hiyo ni sehemu moja ya maendeleo ya kulitatua hili suala, ingawa alisema hawajui lakini yeye inaonesha katika maelezo yake kwamba anajua ni mkandarasi ndie anayelipa. Sasa ndio nilimuomba yeye mwenyewe baada ya kumaliza bajeti na kuanza shughuli zetu pale tushirikiane nae ili sisi tufanye ile kazi yetu ya uratibu na kuweza kushirikiana ili wapate malipo yao. Kwa hivyo ninamuomba sana Mhe. Mwakilishi ushirikiano wake na wizara ndio utakaoleta mafanikio.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti ninamshukuru sana Mhe. Waziri kwa sababu amekubaliana kwamba tukimaliza bajeti hii, labda sasa hii dhima aibebe yeye. Lakini dhima hii siitaki yende kwa watendaji wake kwa sababu wameshadanganya sana ndio yale ninayoyakataa ya kudanganywa, mimi ninamuhushim sana Mhe. Waziri ninamuomba hili suala alichukue yeye kama yeye waziri nitoke mimi na yeye twende kwa wananchi tukakae nao tuelewane tulimalize hili suala, akikubali hilo Mhe. Mwenyekiti tuendelee kama hilo anahisi ni zito basi bado ninaendelea kuzuia fungu hili.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Katika utaratibu ambao tutakubaliana mimi na yeye natoa ahadi hiyo.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu 0701 Idara ya Ujenzi na Utunzaji Barabara 36,015,000,000
Jumla ya Fungu 132, 355, 000, 00

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati bila Ya mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha makadirio ya fedha ya wizara yangu pamoja na mabadiliko, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza liyakubali makadirio hayo.

Naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa wajumbe tunapofanya maamuzi lazima Spika, ahakikishe kama maamuzi yale yanakuwa sahihi na ni ya haki. Kwa hivyo nilikuwa nataka uthibitisho kama kweli waliokubali wameshinda au vyenginevyo. Waliokubali wameshinda.

Waheshimiwa Wajumbe mimi nichukuwe nafasi hii kuwashukuru sana waheshimiwa wajumbe pamoja na mawaziri wote kwa mashirikiano makubwa na kuonesha umakini katika kusimamia matumizi ya serikali. Na haikuwa kwa sababu ya kuhangaisha hapana ni kwa sababu ya kuweka matumizi sahihi ya serikali ambayo ndio kazi ya baraza hili.

Basi waheshimiwa wajumbe baada ya hayo nichukuwe nafasi hii sasa kuahirisha kikao hiki hadi tarehe 6/8/2012 mwaka huu saa tatu barabara za asubuhi.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Saa 11.00 jioni Baraza liliakhirishwa hadi
tarehe 06/08/2012 saa 3.00 asubuhi)